Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Arobaini na Moja - Tarehe 7 Agosti, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. JUMA J. AKUKWETI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KANUNI ZA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE:**

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Bunge la Afrika Mashariki *(The Annual Report on the Activities of the East African Legislative Assembly).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 399

**Athari za Kiuchumi Kutokana na Vita vya Iraq na Marekani**

**MHE. LYDIA T. BOMA (k.n.y. MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA)** aliuliza:-

Kwa kuwa vita kati ya nchi na nchi huleta madhara ya kiuchumi kwa nchi nyingine na kwa kuwa vita vya Taifa kubwa la Marekani dhidi ya Iraq lazima vitaleta madhara makubwa ya kiuchumi karibu ulimwenguni kote hasa kwa nchi maskini kama Tanzania:-

Je, Serikali inaweka mikakati gani ya tahadhari dhidi ya athari hizo ikiwa zitajitokeza?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kuwa vita baina ya nchi na nchi, mara nyingi huleta madhara ya kiuchumi kwa nchi nyingine hususan, katika mwenendo wa kibiashara na ushirikiano wa kimaendeleo. Ni dhahiri basi kuwa vita vya Iraq vilivyohusisha Taifa kubwa la Marekani na mshirika wake, Uingereza, viliashiria athari kadhaa za kiuchumi kwa nchi mbalimbali ulimwenguni hasa nchi jirani na eneo la vita (Mashariki ya Kati na ya mbali) na nchi maskini za Afrika kama Tanzania. Mungu Ibariki, vita hiyo haikuchukua muda mrefu kama ilivyohofiwa. Pamoja na kwamba vita hiyo imeisha sasa, itachukua muda mrefu kuainisha kikamilifu athari zote za vita hivyo.

Napenda kulifahamisha Bunge kwamba mara hali ya vita ilipoanza kujitokeza mwanzoni mwa mwaka huu, Serikali iliunda Kamati ya Wataalam kubainisha athari za vita hiyo kwa uchumi wa Tanzania. Athari zilizobainishwa ni katika maeneo makuu sita, bei ya mafuta, mauzo nje, uagizaji bidhaa, misaada, utalii na ulinzi.

Katika kukabiliana na athari hizo, Serikali imeshachukua hatua kadhaa muhimu, ili, ama kupunguza makali ya athari hizo, au kuondoa kabisa uwezekano wa athari hizo kutokea. Hatua hizo ni pamoja na:-

(a) Serikali imefanya tathmini thabiti, juu ya hali ya mafuta nchini pamoja na bei zake, mpaka kwenye vyanzo vyake. Pamoja na kuridhishwa na matokeo ya tathmini hiyo, kwani tayari bei zimeanza kushuka, hasa baada ya vita kwisha, lakini hali itaendelea kufuatiliwa kwa karibu na kuchukua tahadhari muafaka, ikiwa ni pamoja na kuongeza udhibiti wa waagizaji wa mafuta. Kuondolewa kwa vikwazo dhidi ya mafuta ya Iraq na kuteuliwa rasmi kwa Marekani na Uingereza katika uendeshaji wa biashara ya mafuta hayo katika ujenzi wa Iraq mpya ni dhahiri kutaleta unafuu wa upatikanaji na bei ya mafuta katika soko la Kimataifa.

(b) Kwa kuchelea kupungua kwa fedha za misaada katika Bajeti ya Serikali, hasa kwa kuzingatia kuwa mshirika mkubwa katika vita hiyo, ni Uingereza, iliahidi msaada mkubwa kabla ya vita, Mwongozo wa Mipango na Bajeti kwa mwaka 2003/2004, uliagiza Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa kupanga Bajeti zao katika njia mbili.

(i) *Scenario* ya kwanza, ni kama fedha zote zitapatikana.

(ii) *Scenario* ya pili, ni kama fedha zitapungua kwa asilimia 10.

(c) Ili kuongeza hali ya usalama nchini, ulinzi umeimarishwa katika sehemu zote muhimu, ikijumuisha viwanja vya ndege, bandari, mahoteli yote makubwa, majengo ya Serikali, Balozi na kadhalika. Pamoja na kuchukua hatua hizo, kwa kutumia Idara husika, Serikali imeendelea kuwahakikishia wageni wetu wote usalama wao na mali zao wawapo nchini mwetu.

(d) Serikali na mashirika mbalimbali ya utalii, imeendelea kutangaza biashara ya utalii kwa kushirikiana na wadau na watu binafsi, wa nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kumalizika kwa vita na mpango wa ujenzi wa Iraq ambao unaungwa mkono na Umoja wa Mataifa, utaleta nafuu ya dhahiri katika athari za baada ya vita, lakini Serikali itaendelea kuwa macho kufuatilia hayo yote kwa makini, wakati ikitekeleza mikakati hiyo niliyoielezea.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa athari za vita hii kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba kumekuwa na ongezeko la bei za mafuta ambayo ni nyenzo kubwa katika kusaidia kuongoza nchi kiuchumi.

Je, kwa tatizo hili kwa haya mafuta kutokushuka kama vita yenyewe ilivyokwenda haraka, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza kuna mikakati ambayo inaweza kusaidia ili mpango halisi wa Bajeti uweze kwenda sawasawa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi tulikuwa na wasiwasi mkubwa kwamba vita hii ikiendelea bei ya mafuta itapanda sana. Lakini inavyojionyesha ni kwamba vita hii haikuchukua muda mrefu bei ya mafuta haikupanda sana.

Vile vile katika Bajeti yetu tuliweka *scenarios* mbili kwamba moja kama ni misaada haitapatikana na nyingine kuipunguza kwa asilimia 10. Kwa hali ilivyojionyesha sasa hivi nadhani Bajeti ambayo tumeipanga tutazidi kuendelea nayo tukiifuatilia jinsi tunavyoendelea.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa katika maelezo yake amesema upo uwezekano wa Bajeti kuyumba kwa asilimia 10 kutokana na msaada wa Uingereza. Je, Serikali ina mpango gani wa kujiwekea mikakati ambayo itaiwezesha Serikali yetu na nchi yetu kutokuwa na Bajeti tegemezi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, narudia tena kama nilivyosema katika jibu langu la msingi tulianza kuweka hisia kwa maana tuliweka *assumption* kwamba kama vita itaendelea tuwe na *scenarios* mbili. *Scenario* ya kwanza tunaweka kwa ku-*assume* kwamba vita haitatuathiri na *scenario* ya pili tukasema kama vita itatuathiri tutapunguza Bajeti yetu kwa asilimia 10. Sasa hilo halikutokea, wakati tukilizungumzia suala la kuondokana na Bajeti tegemezi tumezungumzia kila siku ni kwamba tufanye kazi kwa bidii tuongeze uzalishaji, tusindike mazao yetu, tuuze bidhaa nje katika hii tutapata fedha nyingi za mapato, hatimaye Bajeti yetu kuondokana na utegemezi. *(Makofi)*

Na. 400

**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (k.n.y. MHE. FATMA SAID ALI)** aliuliza:-

Kwa kuwa mfuko wa maendeleo ya Jamii umeleta mafanikio Tanzania Zanzibar.

Je, ni lini wananchi wa Jimbo la Mlandege watafaidika na huduma za mfuko huo ambao waliahidiwa kupatiwa Mradi wao wa Ujenzi tangu mwaka 2002?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mbunge wa Mlandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba maamuzi juu ya wapi huduma za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* zipelekwe, hufanywa katika ngazi ya Wilaya kwa upande wa Tanzania Bara na Ofisi ya Waziri Kiongozi kwa upande wa Tanzania Visiwani. Uteuzi wa maeneo huzingatia vigezo vilivyokubalika katika eneo husika kufuatana na maombi ya Kamati ya Usimamizi ya eneo hilo. Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe wa Kamati za Usimamizi *(Steering Committee)* katika maeneo yao husika. Kwa jimbo la Mlandege, Mwenyekiti wake ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri uongozi wa *TASAF* wa Mkoa wa Mjini Magharibi umekwishatoa uamuzi wa kuingiza jimbo la Mlandege kwenye programu ya *TASAF* wakati wowote kuanzia sasa. Hivyo, ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi pamoja na Ofisi ya Waziri Kiongozi ili aweze kupata maelezo zaidi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais itakuwa ikifuatilia kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Kiongozi Zanzibar kwa madhumuni ya kufanikisha suala hili.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa *TASAF* inafanya vizuri katika Visiwa vya Zanzibar yaani Watendaji wake wanafanya vizuri. Lakini kuna ucheleweshwaji mkubwa wa fedha hizi kufika kule Zanzibar. Je, ni lini Serikali itaamua kupeleka haraka haraka fedha za *TASAF* ili wananchi wajiendeleze kufanya miradi yao kwa haraka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, ni kweli mafanikio ya *TASAF* yanategemea upelekaji haraka wa fedha katika maeneo husika na jambo hili la kuchelewa utolewaji wa fedha lililetwa hapa wakati wa hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais na tulilitolea maelezo.

Ningependa kurudia kusema kwamba kwa upande wa Zanzibar lilijitokeza tatizo hilo lakini uongozi wa *TASAF* umekwishafanya mawasiliano na Benki ya Wananchi Zanzibar na kuweka utaratibu wa namna ya kuharakisha utolewaji wa fedha hizo ili ziweze zikafanikisha miradi hiyo.

Lakini nisisitize hapa kwamba fedha hutolewa awamu kwa awamu. Kwa hiyo awamu inayofuata inategemea jinsi mlivyotekeleza awamu ya mwanzo pamoja na kutolea taarifa haraka kupitia ngazi zinazohusika ili awamu ya pili ndiyo iweze kutolewa fedha. Hata hivyo, tutafuatilia ili kusudi tatizo lililojitokeza nyuma liweze kutatuliwa.

**MHE. HADIJA K. KUSAGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa *TASAF* inaendelea kutandaa kwa nchi nzima na katika Mkoa wa Dar es Salaam Wilaya ya Temeke ilipewa nafasi kwa majaribio na kwa kuwa tumeonyesha kufanya vizuri katika miradi hii ya *TASAF;* je, Serikali ina mpango gani wa kutuongezea muda wa kuendelea kuwa katika mpango huu wa *TASAF* na kwa kiasi kikubwa cha fedha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza wananchi wa Jimbo la Temeke katika maeneo yale ambayo wametekeleza *TASAF* wamefanya vizuri kwa sababu Kamati yetu ya maliasili na mazingira ilipata nafasi ya kukagua miradi hiyo na mimi nilikuwepo na Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, alikuwepo wamefanya kazi nzuri.

Kuhusu Temeke itaendelezwa au *TASAF* itaendelea kutoa fedha kwa upande wa Temeke ni kwamba zile Wilaya 40 ambazo zilikuwa za majaribio sasa tumemaliza awamu ya kwanza. Awamu ya pili mwaka 2003 tunakwenda kwenye Wilaya zote na kwa hiyo wale wa awamu ya kwanza watakuwa sasa pamoja na hao wenzao wa awamu ya pili. Hakuna suala la kusema kwamba wataendelea au wataachwa. Watabakia katika awamu ya pili na natumaini utoaji wa fedha unategemea jinsi wananchi wenyewe wanavyoshiriki na kumaliza miradi ile katika awamu kwa awamu. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba Temeke kama Wilaya zingine wataendelea kufaidika na mradi huo wa *TASAF*.

Na. 401

**Sarafu za Shilingi Mia Moja na Hamsini**

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa toleo la sarafu ya shilingi mia moja na shilingi hamsini ndizo sarafu zinazotumika sana na wananchi vijijini na tangu sarafu hizo zilipotolewa zimeonyesha dosari ya kushika kutu na nembo zinafutika na maandishi kutoka haraka na kwa kuwa matumizi ya sarafu hizi ndiyo yanayojenga mzunguko wa kiuchumi kwa wakulima vijijini na kwa kuwa kitendo cha kufutika nembo na maandishi kinapunguza kasi ya mzunguko wa sarafu hizo kwa sababu hazikubaliki katika mzunguko wa biashara.

Je, Serikali itakubaliana nami kuona umuhimu wa kubadilisha sarafu hizo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulijibu swali la Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mbunge wa Kilosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu hutengeneza sarafu kwa malengo ya kusaidia upatikanaji wa chenji ndogo ndogo pale inapohitajika wakati wa kufanya malipo na ndiyo mana thamani zake zimekuwa ndogo zaidi ya thamani ya noti zinazotumika kwenye mzunguko wa fedha.

Ni kweli kwamba sarafu za shilingi mia moja na shilingi hamsini zina mzunguko wa kasi zaidi kuliko sarafu nyingine kwani zinatumika sana vijijini. Mzunguko wa kasi huzifanya kupitia mikononi mwa watu wengi zaidi na pengine kupitia mazingira magumu pia.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu kwa muda mrefu ina utaratibu wa kubadilisha sarafu na noti zilizochakaa kwa kuziondoa kwenye mzunguko wa fedha na kutoa sarafu na noti mpya badala yake. Ili utaratibu huu uweze kufanikiwa, wananchi wanaombwa kurejesha fedha zote zilizochakaa kwenye benki zao za biashara au kuzipeleka Benki Kuu Makao Makuu Dar es Salaam ama kwenye matawi yake yaliyopo Arusha, Mwanza, Mbeya na Zanzibar, ili kuzibadilisha. Aidha, mabenki ya biashara na taasisi za fedha yanahimizwa kupokea fedha zilizochakaaa na kuzibadilisha na kisha kuziwasilisha Benki Kuu ili fedha mpya zitolewe kufidia zile zilizochakaa.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa swali la msingi linahusu sarafu na kwa kuwa sarafu huwa zinatengenezwa kwa kutumia madini ya *Nickel* na *Copper.* Je, kwa nini nchi yetu isifikirie kuvutia wawekezaji ili kuanzisha kiwanda ambacho kitatengeneza sarafu hapa nchini kwa kutumia *Nickel* yetu na hata kwa kutumia *Copper* kutoka nchi jirani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutaufanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Labda Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini ana nyongeza? Hana! Basi tunaendelea. *(Kicheko)*

Na. 402

**Utengenezaji wa Noti Mpya**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa ubadilishaji wa noti mpya umekabiliwa na matatizo mengi yakiwemo ya upungufu wa noti mpya katika benki zote nchini na kuzagaa kwa noti bandia nchini kote.

Je, Serikali inachukua hatua gani katika hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal C. Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha zoezi la kubadilisha noti linafanikiwa, Serikali kupitia Benki Kuu, ilichapisha noti kulingana na noti zilizoko kwenye mzunguko pamoja na ziada. Takwimu zinaonyesha ya kwamba kufikia tarehe 02 Februari, 2003 yaani siku moja kabla ya kuanza rasmi zoezi la kubadilishwa noti, noti zenye thamani ya shilingi bilioni 305.750 zilikuwa tayari zimechapishwa, ikilinganishwa na noti za zamani zenye thamani ya shilingi bilioni 500.92 zilizokuwa kwenye mzunguko siku hiyo. Kiwango hiki ni asilimia 61 ya kiwango cha noti za zamani zilizokuwepo kwenye mzunguko wa fedha wakati zoezi la kubadili noti lilipoanza tarehe 03 Februari, 2003.

Kufikia tarehe 07 Mei, 2003 noti mpya za thamani ya shilingi bilioni 767 zilikuwa zimechapishwa na kati ya hizo noti za shilingi bilioni 414.263 zilikuwa zimeshaingizwa kwenye mzunguko. Noti za zamani za thamani ya shilingi bilioni 70.275 zilikuwa bado ziko kwenye mzunguko kufikia tarehe hiyo.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinaonyesha kwamba, Serikali ilikuwa na uwezo wa kuzibadilisha noti zote za zamani na kutoa noti mpya. Kwa hiyo, matatizo yaliyojitokeza katika zoezi la kubadilisha noti hayahusiani na upungufu wa noti mpya kwani noti mpya zenye thamani ya shilingi bilioni

352,737 zilizokuwepo nchini kiasi ambacho ni mara tano zaidi ya kiwango cha shilingi bilioni 70,275 cha noti za zamani zilizobaki kwenye mzunguko mnamo tarehe 07 Mei, 2003.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja kwamba noti za bandia zimezagaa nchini kote, napenda kufafanua kwamba, tatizo hili linazikabili nchi zote ulimwenguni, siyo Tanzania peke yake na ndio maana Serikali iliamua kuchapisha noti mpya ambazo hazigushiki kwa urahisi. Ni vizuri pia ikaeleweka kwamba kipindi cha kubadilisha noti kilitumiwa na baadhi ya watu kama mwanya wa kupenyeza noti bandia, Benki Kuu ilitoa matangazo kupitia vyombo mbalimbali vya habari yakiwemo magazeti, redio, *television* na vipeperushi kuelezea sura na alama za noti mpya kabla na baada ya kutolewa kwa noti mpya. Matangazo hayo yalitangazwa kwa muda mrefu kwa nia ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanazielewa vyema alama muhimu zinazowawezesha kuzitambua noti halali ili kuzitofautisha na noti za bandia kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wameelimishwa vya kutosha kutambua alama za usalama zilizomo kwenye noti mpya, Serikali inaamini kwamba itakuwa rahisi kwa wananchi kuzitambua noti bandia kila mara wahalifu wanapojaribu kuzigushi na hapo ndipo vita dhidi ya noti bandia itaweza kupata mafanikio. Hivyo, Serikali inawaomba wananchi kuwa waangalifu wanapopokea noti hasa sehemu isiyokuwa na mwanga wa kutosha. Ikibidi, wazichunguze alama za usalama kama ilivyoelezwa kwenye mabango na vipeperushi vilivyosambazwa na Benki Kuu nchini kote. Aidha, pale wanapogundua noti za bandia watoe taarifa kwa vyombo vya usalama ili wahalifu waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri kwa Naibu Waziri wa Fedha, naomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa noti bandia ambazo zinazagaa nchini zinatengenezwa na ziko mashine ambazo zinatumika kutengeneza. Je, Serikali imefanya juhudi gani na itafanya juhudi gani kuhakikisha kwamba hizi mashine zinakamatwa na utengenezaji wa noti bandia unadhibitiwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna noti bandia zipo lakini siyo kweli kwamba zimezagaa, ingekuwa zimezagaa zingekuwa nyingi sana. Watu wachache ambao wanasambaza fedha hizo na wapo wamewahi kukamatwa na wamepelekwa Mahakamani na Serikali inasaidiana na Polisi wa Kimataifa yaani *Interpol* kuwakamata watu wanaohusika na *Network* inayofanya uhalifu huu na napenda kulihakikishia Bunge lako na wananchi kwamba Serikali inalifuatilia suala hili kwa karibu sana na kubaini mbinu wanazotumia na mahali walipojificha.

Lakini tunaamini kwamba pia noti hizi inawezekana zinatengenezwa siyo nchini, zinatengenezwa nje ya nchi na ndiyo maana Serikali, Polisi nchini inasaidiana na Polisi wa Kimataifa ili kuweza kuwakamata wahalifu hao na kuondosha tatizo hili. Lakini kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi tatizo la noti bandia siyo tu liko Tanzania lakini hata dola ya Marekani pia inagushiwa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Fedha. Kwa kukiri kwamba hili tatizo la watu kuchapisha noti inaonekana litatuletea balaa kwa sababu linaongezeka na inaonekana liko sehemu nyingi za nchi Mwanza, tunasikia habari hizi za magazeti, Arusha hata jana watu wamekamatwa. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kutoa rai kwa wananchi watupe habari Serikali iko tayari kutoa zawadi ya shilingi milioni tano kwa mtu yeyote atakayetupa habari za kukamata watu wenye mitambo hiyo, shilingi milioni tano kwa mtu yeyote atakayetupa habari za kukamata mitambo hiyo. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa lilipita Azimio la kuwaenzi waasisi wetu wote wawili katika noti mpya zinazotengenezwa. Lakini kwa bahati mbaya tumemwona mwasisi mmoja tu. Je, tatizo ni nini hata mwasisi wa pili asiingizwe katika noti mpya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri leo umeniruhusu kutoa taarifa juu ya suala hili mara baada ya maswali kwa hiyo nitatoa ufafanuzi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akalieleza Bunge hili na wananchi wanaotusikiliza kwa nini noti ya shilingi 10,000/= imekuwa ni haba katika mzunguko hasa sehemu za mijini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi nilisema kwamba hadi kufikia tarehe 7 Mei, 2003 kulikuwa kumebaki shilingi bilioni 70 kwenye mzunguko. Lakini kulikuwa na shilingi bilioni 325 ambazo zilikuwa zimechapishwa tayari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuendelea ku-*pump* hela kwenye mzunguko kwenye uchumi kungeongeza mzuko kabla ya hizi hela ambazo ziko kwenye mzunguko hazijatolewa na zoezi la kubadilisha noti ama fedha za zamani limeongezwa mpaka mwisho wa Septemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bado kuna fedha kwenye mzunguko na tunafanya tahadhari tusiingize hela nyingi kwenye mzunguko halafu zikaathiri uchumi wetu. Kwa hiyo, tunaamini kwamba baada ya zoezi hili kukamilika noti za shilingi 10,000 zitaingizwa kufidia hilo pengo lililopo.

Na. 403

**Mbolea na Madawa ya Kuulia Wadudu**

**MHE. SEMINDU K. PAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na mtindo wa nchi yetu wa kupokea dawa ya kuulia wadudu na mbolea ambazo ni mbovu na kwamba dawa hizo zimehifadhiwa kwenye maghala yetu nchini.

Je, kwa nini Serikali haiyateketezi madawa hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Semindu Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu haina mtindo wa kupokea madawa ya kuulia wadudu na mbolea ambayo ni mabovu. Uingizaji wa madawa na mbolea nchini unasimamiwa na Sheria Na. 5 ya mwaka wa 1997 *(The Plant Protection Act, 1997).* Shirika la Viwango Tanzania *(Tanzania Bureau of Standards - TBS)* linahakikisha kwamba mbolea inayoingizwa nchini inafikia viwango vya virutubisho vinavyotakiwa.

Aidha, *TPRI* hufanya uchunguzi wa madawa yote ya kilimo kabla hayajaanza kutumika ili kuhakiki ubora wake. Kwa hiyo, Serikali inachukua tahadhari zote kuhakikisha kwamba madawa ya mimea na mbolea zinazoingizwa nchini zinakidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo.

Serikali kupitia *TPRI, NEMC, TBS,* Maabara ya Mkemia Mkuu na Idara ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais, imefanya tathmini na kugundua kuwa kuna takriban tani 1,000 za madawa ambayo yanahitaji kuteketezwa. Madawa hayo yaliingizwa nchini yakiwa na viwango vya ubora vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria, lakini yalikwisha muda wake kutokana na ama kukaa kwa muda mrefu bila kutumika au kusitishwa kutumika duniani baada ya kubainika kuwa yana madhara katika mazingira na viumbe hai. Hivi sasa madawa hayo yamehifadhiwa kwenye maghala 300 katika maeneo mbalimbali nchini. Madawa hayo hayajateketezwa kutokana na gharama kubwa za kuyateketeza na kukosekana kwa utaalam.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuyateketeza madawa hayo kupitia Mradi wa *African Stockpile Program (ASP)* unaofadhiliwa na *Global Environmental Facility* kupitia Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa *(FAO)* na Muungano wa watengenezaji wa madawa ulimwenguni unaojulikana kama *Crop Life International.*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula. Lakini kwa hili naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba ile *survey* tuliyoifanya ya *environmental* nilipokuwa katika Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambapo tuligundua tani 50 za pale Vikuge ambazo bado zipo mpaka leo za *DDT* ambayo imefutwa lakini iliingizwa wakajengea pale kwa gharama zaidi badala ya kuteketeza; je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akatoa taarifa ya uteketezaji wa dawa hizo kabla ya mwaka huu kwa sababu inaonyesha kwamba dawa hizo zinauzwa katika maduka?

Mheshimiwa Spika, pili, Nigeria katika miaka ya 1976 iliagiza dawa na ikapata tani kama 80 kutoka nchi za Italia zilizokuwa zimekaribia ku-*expire* baada ya miezi sita, ikaamuru kurudisha dawa hizo huko huko Italia kwa gharama za ile nchi iliyozileta, sasa Tanzania kama imeleta dawa hizo zilizokuwa zinakaribia ku-*expire* kwa ajili ya kufanya kwamba hapa ni *dumping place,* wanaweza wakazitambua nchi hizo na kuzirudisha kwa gharama za nchi hizo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, yapo mawasiliano na hawa wenye utaalam wa kuyateketeza, tunaamini tutashughulikia kuyateketeza madawa yote yaliyopo nchini mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, pili, hatujapokea dawa hapa *over cure dumping,* hatujapokea dawa hizo. Kama nilivyoeleza ni kuwa dawa nyingine zilikuja na zikaisha muda wake kwa maelezo niliyoyatoa kwa sababu nilizozitoa. Kwa hiyo, napenda kumwondolea wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba nchi yetu haitumiki kama *dumping place.*

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kwa vile katika jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza habari ya tani karibu 1,000 za madawa ambayo hayafai tena kwa kazi ambayo ilikuwa imekusudiwa; na kwa maana hiyo anasema haya yanasubiri kuteketezwa lakini hayateketezwi kwa sababu ya gharama.

Napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba gharama hiyo anayoihofia kuhusu uteketezaji wa dawa hizi, dawa hizi hazijafikia mahala ambapo hali hiyo iliyo na dawa hizo sasa hivi inaweza kuleta athari kwa binadamu kiasi kwamba aone gharama ya maisha ya binadamu kwamba ni afadhali kuziteketeza dawa zile kwa gharama yoyote kuliko kuziacha kwa sababu anahofia fedha nyingi zitatumika kwenye zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, madawa haya yote ya hatari yamehifadhiwa katika maghala ambayo yapo mbali na makazi ya wananchi yaani hayapo jirani kiasi kwamba yanaweza yakawadhuru. Lakini papo hapo tunatambua athari za kuwepo kwa madawa haya ndiyo maana majadiliano yanaendelea na mara tupatapo huo msaada wa kuyateketeza kwa sababu utaalam hatuna, tutayateketeza kwa manufaa ya nchi yetu.

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, aah, samahani.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Wakati mwingine si vibaya kufanana na watu wengine. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuongeza majibu ya nyongeza kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, kuhusu uteketezaji wa madawa chakavu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulipowasilisha hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais, moja ya mradi ambao nchi yetu inatekeleza kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani ni hili suala la madawa chakavu ambayo ni kweli katika nchi yetu hatuna utaalam wa kuyateketeza wala hatuna zana za kufanya kazi hiyo lakini tunashirikiana na Shirika la Chakula Duniani katika Mradi unaoitwa *African Stockpile Program* kukusanya madawa yote chakavu na kuweza kuyasafirisha nje ya nchi ambako kuna huduma au *facilities* za kuyateketeza bila kuleta madhara kwa afya ya binadamu na mazingira.

Na. 404

**Uboreshaji wa Kilimo cha Zao la Mahindi**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma ni wazalishaji wakubwa wa zao la mahindi; na kwa kuwa hivi sasa Mikoa hiyo imeruhusiwa kuuza zao hilo nchi za jirani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuboresha kilimo cha zao hilo kwa ajili ya Mikoa yetu iliyokumbwa na baa la njaa ikiwa ni pamoja na nchi za jirani?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga hifadhi maalum *(Selo)* ya zao hilo katika kila Mkoa?

(c) Iwapo Serikali haina mpango wowote katika sehemu (a) na (b) ya swali hili; je, imeishirikishaje sekta binafsi katika hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mpango wa Serikali katika kuboresha kilimo cha mahindi kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ni pamoja na kufanya utafiti ili kupata mbegu bora zinazoweza kutoa mavuno mengi kwa eneo na zinazostahimili ukame na visumbufu vya mazao, kutoa mafunzo kwa wakulima na wataalam juu ya mbinu na teknolojia bora ya uzalishaji mahindi, kuendeleza kilimo cha wanyamakazi na kufufua vituo vya maksai nchini na kuelekeza mbolea kwa wingi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kuhakikisha kwamba inapatikana na kwa bei nafuu.

Katika msimu wa 2003/2004, Serikali itatoa ruzuku ya kufidia sehemu ya gharama za kusafirisha mbolea. Kamati maalum ya Makatibu Wakuu inashughulikia suala hili.

(b) Serikali haina mpango wa kujenga *Silos* katika kila Mkoa. Utafiti uliofanywa mwaka wa 1978 ulibaini kuwa Kanda saba za hifadhi ya mahindi ambazo ni zifuatazo, Kipawa, Dar es Salaam kwa ajili ya Mikoa ya Dar es Saalam, Morogoro, Lindi na Mtwara, Dodoma kwa ajili ya Dodoma na Singida, Shinyanga kwa ajili ya Mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Tabora, Mwanza, Mara na Kagera, Arusha kwa ajili ya Mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga, Makambako kwa ajili ya Mikoa ya Iringa na Mbeya, Sumbawanga kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa na Songea kwa ajili ya Mkoa wa Ruvuma. Vituo vya Songea, Makambako na Rukwa ni vyanzo vya mahindi kwa ajili ya Kanda za Kaskazini. Katika Kanda zote saba yapo maghala yenye uwezo wa kuhifadhi tani 241,000 za mahindi. Hakuna mpango wa kujenga *Silos* au maghala mapya.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema, Serikali ina mipango ya kuboresha kilimo cha mahindi kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kisichokuwepo ni mpango wa kujenga *Silos* kwenye kila Mkoa na kutokana na gharama kubwa za kujenga *Silos* hizo, sekta binafsi haitegemewi kuzijenga na hakuna mpango wa kuihimiza kufanya hivyo.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuipongeza Serikali kwa hatua ambayo imeanza kuchukua ili kuboresha kilimo cha zao la mahindi katika nchi yetu. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa kuwa Tanzania imekuwa ikikabiliwa na baa la njaa mara kwa mara, je, Serikali au Wizara imejiandaa vipi kwa ununuzi na uhifadhi wa chakula kila mwaka wa mavuno ili kutosheleza mahitaji ya wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, kwa mwaka huu Serikali imejiandaa vipi kukabili kupanda kwa ongezeko kubwa la bei ya mahindi katika Mikoa iliyokumbwa na njaa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuzipokea pongezi zote ulizozitoa kwa niaba ya Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, pili, tunachofanya sisi ni kuweka akiba tuliyoidhinishiwa na Bunge ambayo ni tani 150,000 tu. Sasa hivi tunazo hizo tani, *capacity* ile tuliyoionyesha hapo 241,000 lakini hatununui mahindi peke yetu bila kutegemea mtu mwingine. Kuna aina mbili au tatu za kupata uwezo wa kuweka mahindi.

Moja, Serikali yenyewe inanunua ili kujiwekea akiba, pili, ni kuwahamasisha, kuwapa vibali wafanyabiashara binafsi kuingiza mazao kutoka nje na kuyaleta nchini kwa ajili ya kuwagawia wananchi. Njia nyingine ni Serikali yenyewe kuweka fedha za akiba. Lakini pamoja na hayo tunapokea vile vile msaada toka kwa nchi wahisani.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tumejiandaa kwa yote hayo kama nilivyosema wiki iliyopita ni kwamba, kuna wafanyabiashara kama 13 ambao wameruhusiwa kuingiza nchini tani zinazotakiwa kuliwa nchini. Aidha, *donors* wametoa baadhi ya vyakula nchini na Serikali imeweka hela za tahadhari, tatizo litakapopatikana tutanunua chakula cha kutosha ili kupambana na njaa. Zaidi ya hayo ni kuwa kuna Kamati ya Kitaifa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, huko tunakaa ili kutathmini athari za njaa nchini na kila inapowezekana msaada unatolewa. *(Makofi)*

Na. 405

**Barabara Zitakazotengenezwa Chini ya Mpango wa *NEPAD***

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA** aliuliza:-

Kwa kuwa kati ya barabara zilizopendekezwa na kufirikiwa kutengenezwa chini ya Mpango wa *NEPAD* kwa kiwango cha lami ni pamoja na barabara ya Itigi - Rungwa - Makongorosi - Mbeya yenye urefu wa kilometa 401; na kwa kuwa mpaka sasa fedha inayotafutwa ni kwa ajili ya upembuzi yakinifu; na kwa kuwa mpango huo ni mzuri na utasaidia ujenzi wa barabara nchini kwenda haraka:-

Je, mpaka sasa ni hatua gani zilizofikiwa katika kupata fedha kwa ajili ya kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fedha chini ya Mpango wa *NEPAD* hazijapatikana na juhudi zinaendelea kupata wafadhili kupitia mpango huo.

Wakati Serikali inafuatilia Mpango huo wa *NEPAD,* Wizara yangu itaendelea kutekeleza mradi huu kwa awamu kwa kutumia uwezo wake wa ndani. Awamu ya Kwanza ya utekelezaji mradi huu inahusisha

sehemu ya Mbeya hadi Makongolosi yenye urefu wa kilometa 115 ambayo ipo katika hatua ya usanifu kwa kiwango cha lami unaotarajiwa kukamilika mwaka wa fedha wa 2003/2004 na itafuatiwa na ujenzi mara baada ya kukamilika usanifu huo. Katika miaka ya fedha ya 2002/2003 na 2003/2004 sehemu hii ya mradi imetengewa jumla ya shilingi milioni 450 kwa ajili ya usanifu huo.

Awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huu baada ya kupata fedha itahusisha sehemu ya Makongolosi - Rungwa - Itigi - Mkiwa ambayo inalenga kuunganisha Ukanda wa Usafirishaji wa Magharibi Kati na Ukanda wa Usafirishaji wa Kati.

Aidha, katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004, jumla ya shilingi milioni 153 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum ya barabara ya Itigi - Rungwa na shilingi milioni 781.5 zimetengwa kwa ajili ya barabara ya Manyoni - Itigi - Rungwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo utaona ni jinsi gani Serikali inavyojitahidi kuhakikisha kuwa barabara hii pamoja na nyingine nchini zinajengwa kufikia kiwango cha lami.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Lakini vile vile naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Wizara yake kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa nia njema ambayo wanaionyesha katika kuishughulikia hii barabara.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa ile Awamu ya Kwanza ya kutoka Mbeya mpaka Makongolosi fedha kwa ajili ya usanifu imekwishapatikana na kwa majibu yake mwenyewe hatua inayofuata ni kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi, sasa kama lengo ni kushughulikia barabara yote, isingelikuwa vema sasa ili kazi iwe na mtiririko mzuri kwa Wizara kutafuta fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu kwa kipande kilichobaki cha kutoka Makongolosi - Rungwa - Itigi mpaka Mkiwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa ujenzi wa barabara ni vizuri tukaenda awamu kwa awamu kama nilivyosema. Awamu ya Kwanza tunaishia Makongolosi baada ya usanifu huo tunatia lami mpaka Makongolosi na wakati huo tunatafuta fedha za usanifu hadi Mkiwa. Hii itatusaidia sisi kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa kwa uhakika.

Na. 406

**Ujenzi wa Nyumba Kwenye Eneo la Hifadhi ya Barabara**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwananchi kutojua Sheria siyo kinga mbele ya hukumu; na ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba wananchi hawavunji Sheria kwa sababu tu ya kutozijua Sheria; na kwa kuwa Serikali inao Watendaji wake kuanzia kwenye ngazi ya Wizara, Mikoani na hata Wakaguzi wa barabara zote nchini:-

(a) Je, kwa nini Serikali inawaachia wananchi wajenge nyumba kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara huku ikielewa kuwa wananchi hao wanavunja Sheria kwa kufanya hivyo?

(b) Kwa kuwa suala la kuwavunjia nyumba wananchi siyo tu linaleta adha na usumbufu kwa familia husika bali linaathiri uchumi wa Taifa pia; je, Serikali inachukua hatua gani za kuwaelimisha wananchi badala ya kutumia nguvu?

(c) Je, Serikali haioni kwamba inahusika sana na mgogoro huo kwa kutosimamia Sheria zake ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufundi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa wananchi kuhakikisha kwamba hawavunji Sheria zilizowekwa na nchi. Hivyo wananchi kujenga kwenye hifadhi ya barabara ni kuvunja Sheria za Barabara *(The Highway Ordinance)* kwa sababu zao wenyewe na wala sio kwamba Serikali imewaachia kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, awali tatizo hili halikuwa kubwa lakini baada ya kuongezeka, Serikali ilianza kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuheshimu Sheria za barabara.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia madhara makubwa yanayotokana na kuvunja nyumba zilizojengwa kinyume na Sheria, Wizara yangu imekuwa ikitoa matangazo mbalimbali kupitia vyombo vya habari yanayolenga kuwaelimisha wananchi umuhimu wa hifadhi ya barabara na madhara yatokanayo na kujenga kwenye maeneo hayo. Wizara yangu inalenga kuimarisha elimu hii kwa wananchi kupitia kwenye magazeti, redio, televisheni pamoja na kusambaza vipeperushi. Pia, somo hili litazingatiwa katika mpango wa kutoa elimu ya usalama barabarani katika shule, mpango ambao uko kwenye majaribio. Pamoja na juhudi hizo, ujenzi wa mawe yanayoonyesha mipaka ya hifadhi ya barabara zetu umeanza kutekelezwa.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza awali, mgogoro huu unasababishwa na wananchi wasiopenda kufuata Sheria. Serikali haina haja ya kuwa na migogoro na wananchi wake, bali hulazimika kufanya hivyo ikiwa watavunja Sheria za nchi. Hata hivyo, Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kama nilivyoeleza hapo awali kuhakikisha Sheria hazivunjwi ili kuzuia migogoro hiyo.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali langu linasema kwamba Wizara ya Ujenzi inao mtandao wa wafanyakazi, inao Wakaguzi wa Barabara ambao wanapita maeneo mbalimbali ili kuangalia hali ya barabara; je, Wakaguzi hawa wao hawazijui Sheria kwa sababu wanamwangalia mwananchi akijenga msingi, anajenga ukuta, anapaua na baadhi ya wananchi wamekaa katika maeneo hayo miaka kumi bila kupewa taarifa kwamba wamevunja Sheria; je, tatizo hapa liko wapi? Hiyo ni sehemu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kwamba tunaishukuru Serikali kwamba inafanya kazi nzuri kwa kupanua barabara zake na sasa upanuzi huu unafanyika katika barabara kuu kwa sehemu kubwa na tunatarajia ya kwamba upanuzi huu pia utakwenda katika Halmashauri za Wilaya, barabara za Halmashauri za Wilaya; je, Serikali au Wizara hii inasaidia vipi ili kuhakikisha ya kwamba Sheria hii angalau inafika pia katika Mabaraza ya Madiwani ili yasaidie kuwaelimisha wananchi katika suala hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kweli kwamba tunao mtandao wa barabara na tunao watu wengi ambao wanapita kwa wafanyakazi wetu. Lakini kama nilivyosema hapo awali ya kwamba, tatizo hili halikuwa kubwa awali, kwa hiyo lilipokuwa limeanza kuongezeka tukaanza kutoa elimu, kusimamia kikamilifu na kwa sababu sasa tunasimamia kikamilifu unaona matatizo yanaanza kujitokeza, kama tusingeisimamia kikamilifu sasa hivi kusingekuwa na makelele hayo ambayo yapo sasa.

Hii ni kwa sababu tumewaelekeza wafanyakazi wetu hasa *Regional Managers* kwamba sasa *Regional Manager* atawajibika kwa kuhakikisha kwamba hifadhi ya barabara katika Mkoa wake imeeleweka na mawe ya kuonyesha hifadhi ya barabara yamewekwa ili wananchi wasisumbuliwe baada ya wao kuanza kujenga, wajue wanajenga wapi. Hii tumekwishaelekeza tayari.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa sheria uende kwenye kuwasaidia Madiwani ili nao wawaelekeze. Sheria hii ipo, Wakurugenzi wa Halmashauri na wa Manispaa wanajua na ninyi wenyewe mnaweza kuona kwamba wanaotoa vibali vya ujenzi ni Wakurugenzi hawa na Kamati zao. Inapofika Mjini Wizara ya Ujenzi inakwama, haiwezi tena kuchukua hatua ndani ya Miji. Kwa mfano, Dodoma mwisho wetu ni *keep*

*left* hii ya hapa mwanzo baada ya *keep left* hiyo inapoanza *petrol station* pale ni *CDA* na Manispaa ndiyo wanawajibika sasa kusimamia hifadhi hiyo na kusimamia upanuzi wa barabara.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii na pia naomba nipongeze majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Barabara ya Bunda - Kisorya wakati inajengwa iliwakuta wananchi wakiwa pale pale, sasa katika ujenzi wake linapokuja suala la kupanua barabara wale wananchi hawalipwi fidia, inaonekana wao ndiyo wameingia ndani ya eneo la barabara; je, Serikali haioni kwamba inapoanza kupanua barabara iwalipe wananchi kama hao fidia? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakubali kabisa kwamba barabara ya Bunda - Kisorya ilipojengwa wananchi walikutwa hapo, wakati inapanuliwa wananchi walikutwa hapo lakini wale ambao walikuwa na stahili ya kulipwa pale hawakuwepo isipokuwa baadaye walikwenda kutafuta hati, bahati nzuri tatizo hili limenikuta ninalo mimi, wamekwenda kutafuta hati ili kuja kudai haki zao. Kwa hiyo, walikuwa wametafuta hati za kumiliki viwanja baada ya sisi kupanua barabara na kwa misingi hiyo hatulipi.

Na. 407

**Watoto wa Wakimbizi Kwenye Jimbo la Kilolo**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO** aliuliza:-

Kwa kuwa katika sehemu ya Mgagao Kata ya Ukumbi kulikuwa na Kambi ya Wapiganiaji Uhuru wa Afrika ya Kusini na Zimbambwe; na kwa kuwa wakati huo wakimbizi waliweza kuzaa na wanawake wa Kitanzania na kuacha watoto ambao sasa wanapata taabu sana:-

(a) Je, Serikali itawasaidiaje watoto hao kwa kuwapatia huduma za msingi na kuona uwezekano wa kuwasiliana na nchi husika ili watoto hao wapatiwe huduma zinazostahili?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kufanya sensa ya watoto hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Mgagao kilichopo katika Jimbo la Kilolo, Mkoa wa Iringa, waliishi wapigania uhuru wa Chama cha *ANC* cha Afrika Kusini wakati wa harakati za kupambana na siasa za ubaguzi wa rangi katika miaka ya 1970. Aidha, Kambi hiyo ilifungwa baada ya kutokomezwa kwa siasa za ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini mwaka 1990 na wapigania uhuru hao wakarejea makwao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo la Kijiji cha Mgagao sio kubwa na idadi ya wakazi wake sio kubwa sana, tunawaomba viongozi wa Wilaya mpya ya Kilolo washirikiane na uongozi wa Serikali ya Kijiji cha Mgagao na Kata hiyo ili kuwatambua watoto husika na kupata idadi yao kamili na kuleta taarifa Wizarani kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kilolo.

Aidha, idadi ikipatikana Idara yetu ya Uhamiaji itafanya zoezi la kuthibitisha hadhi ya Utaifa wa watoto hao na iwapo itadhihirika kuwa kuna watoto ambao baba zao ni raia wa Afrika ya Kusini, Serikali yetu itaijulisha Serikali ya Afrika ya Kusini ili hatua muafaka za kuwaunganisha watoto hao na baba zao ziweze kuchulikuwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Venance Mwamoto, kwa kupigania haki za watoto katika Jimbo lake. *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika swali langu la msingi nimeuliza uwezekano wa kupatiwa wale watoto huduma; na kwa kuwa kambi ile imegeuzwa gereza; je, Serikali itakuwa tayari kubadilisha sehemu hiyo ya gereza ambalo uwezo wake ulikuwa ni kuchukua watu 3,000 na sasa hivi wamefungwa wafungwa 30 ili iwe shule ya sekondari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuja kuona hali ilivyo katika kambi ile ili wananchi wa sehemu husika waweze kuona uwezekano wa kujengewa gereza sehemu nyingine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baada ya wapiganiaji wa uhuru wa Afrika ya Kusini kurudi kwao ile kambi waliyokuwa wanaitumia kama kituo chao cha harakati, Serikali iliichukua na kuifanya kuwa gereza.

Mheshimiwa Spika, sasa ombi ambalo Mheshimiwa Mbunge analileta ni kwamba Serikali sasa tukubali gereza hilo likabidhiwe wananchi wa Kilolo ili liwe sekondari na wananchi wa Kilolo watoe eneo lingine kwa ajili ya kujenga gereza na anasema; je, tuko tayari kwenda ili kuona hali ilivyo?

Mheshimiwa Spika, wakati wa bajeti yetu suala hili lilijadiliwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mbele ya Bunge hili alitoa kauli kwamba atakwenda Kilolo, ataona hali ilivyo, atashauriana na viongozi wa Wilaya ya Kilolo ili kuona kama muafaka utafikiwa katika kukubaliana na maombi yao. Kwa hiyo suala hili linashughulikiwa na Waziri mwenyewe atafika Kilolo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha kwa hiyo, tunaendelea na agenda nyingine, lakini kwanza matangazo.

Vikao vya Kamati leo, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 4.30 asubuhi hii chumba namba 54. Kamati nyingine, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Sophia Simba, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa 6.00 mchana ukumbi Namba 81. Kamati ya Uongozi, Mwenyekiti anawaomba Wajumbe wa Kamati ya uongozi tukutane kwa muda mfupi baada ya kuahirisha kikao cha asubuhi ili kufanya majumuisho ya jinsi mkutano huu ulivyokwenda na kuhitimisha Mkutano wa Bajeti, saa 7.00 mchana. Chama cha Wabunge Wanaopambana na Ukimwi (TAPAC), Mheshimiwa Venance Mwamoto, Katibu Msaidizi, anaomba kuwe na kikao cha wanachama wote wa TAPAC saa 7.00 mchana na wabaki humu humu ndani kwa ajili ya kikao hicho.

Mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper.*

## KAULI ZA MAWAZIRI

## TAMKO LA WAZIRI WA FEDHA KUHUSU KUWEKA SURA YA HAYATI SHEIKH AMAN ABEID KARUME KATIKA NOTI MPYA ZA TANZANIA

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika Kikao cha Kumi na Moja cha Bunge niliahidi kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu tamko rasmi kuhusu kutowekwa kwa sura ya Hayati Abeid Aman Karume, katika toleo la noti mpya lililotolewa na Benki Kuu ya Tanzania. Hatua hii imefuatia maelezo binafsi yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mbunge wa Jimbo la Magomeni Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yake binafsi, Mheshimiwa Issa Suleiman Mohammed, alibainisha kwamba pamoja na kuwepo kwa Azimio la Bunge la tarehe 16 Aprili, 1997 alishangazwa kuona kwamba katika toleo jipya la noti hakuna noti yoyote iliyotengenezwa na kuwekwa sura ya Hayati Abeid Aman Karume.

Aidha, alipenda kufahamu kama kasoro hii ilitokana na wahusika kusahau uamuzi wa Bunge ama kwa sababu nyinginezo. Vile vile aliiomba Serikali iahidi kuchukua hatua za kurekebisha kasoro hii ili nia na azma ya Azimio la Bunge la tarehe 16 Aprili, 1997 itekelezwe kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, noti mpya zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania mnamo tarehe 3 Februari, 2003 ni toleo la kawaida lenye lengo la kubadili noti zilizokuwepo kwenye mzunguko. Toleo hili pamoja na mambo mengine lilizingatia mabadiliko ya teknolojia na umuhimu wa kuimarisha alama za usalama kwenye noti zetu katika kupambana na tatizo sugu lililoenea hapa nchini la uhalifu wa kughushi na kutengeneza noti bandia.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuweka picha za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika noti na sarafu ulianza mwaka 1966 ambapo Tanzania ilianza kutumia fedha zenye sura ya picha ya Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Aidha, mnamo mwaka 1985 kulifanyika mabadiliko katika sura ya fedha za nchi yetu kwa kuweka sura ya Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Alhaj Ali Hassan Mwinyi, sambamba na picha ya Baba wa Taifa kwenye baadhi ya fedha. Utaratibu umekuja kubadilika mwaka 1995 baada ya kumpata Rais wa Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ambaye kwa ridhaa yake mwenyewe hakupenda sura ya picha yake iwekwe kwenye fedha ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali iliyojitokeza mwaka 1995, Serikali iliona upo umuhimu wa kuweka utaratibu wa kudumu ambao utazingatia haja ya kuwaenzi Waasisi Wakuu wawili wa Muungano wa Tanzania. Aidha, Bunge lako Tukufu lilipitisha kwa kauli moja Azimio la Bunge Na.7 la mwaka 1997 na kuiagiza Serikali kama ifuatavyo na nanukuu. “Ili kuweka utaratibu wa kudumu ambao utazingatia haja ya kuwaenzi Waasisi Wakuu wawili wa Muungano wa Tanzania, Bunge linaiagiza Serikali ichukue hatua zinazostahili ili kuhakikisha kwamba kuanzia sasa:-

(i) Azimio la Bunge lililopitishwa mwaka 1985 kuhusu sura ya picha ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kuwekwa kwenye baadhi ya noti na sarafu za Tanzania linatekelezwa ipasavyo na Benki Kuu kwa kuzingatia mabadiliko yanayokwenda na wakati.

(ii) Serikali iangalie uwezekano wa kuweka sura ya Mwasisi wa Pili wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Hayati Abeid Aman Karume kwenye baadhi ya noti na sarafu za Tanzania zitakazotengenezwa.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo, mnamo mwaka 1998, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilitengeneza sarafu ya shilingi 200 yenye picha ya Hayati Abeid Aman Karume, Mwasisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sarafu hii bado inaendelea kutolewa na Benki Kuu na inaendelea kutumika hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, mnamo mwaka 2000, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa pia noti mpya ya shilingi 1,000/= yenye picha ya sura ya Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kufuatana na utamaduni wa utoaji noti na sarafu, noti hii itaendelea kutolewa na picha ya Baba wa Taifa kama ambavyo sarafu ya shilingi 200/= itaendelea kuwa na sura ya picha ya Hayati Aman Abeid Karume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa zoezi hili sasa limechelewa baada ya noti mpya kutolewa, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na hasa Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mbunge wa Jimbo la Magomeni Zanzibar kwamba Serikali imeikumbusha tena Benki Kuu ya Tanzania kuzingatia Azimio la Bunge la mwaka 1997 ili kuweka sura ya picha ya Hayati Abeid Aman Karume katika matoleo ya baadaye ya noti mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, kwa kutuzindua kwani usahaulifu huo haukuwa kwa makusudi au kwa nia mbaya kwa Hayati Abeid Aman Karume au Muungano wa Jamhuri ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

**Azimio la Kuridhia Hifadhi ya Makubaliano Mapya ya Matumizi ya Maji ya Kimataifa ya Mwaka *2000 (Revised Protocol on Shared Water Courses in the SADC Region)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika Kuhusu Makubaliano Mapya ya Matumizi ya Maji ya Kimataifa ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, sisi watu wa Mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara na majirani zetu wa Songea, tunapozungumzia matumizi ya maji ya Kimataifa, linalokuja mbele yetu kwanza ni matumizi mazuri ya maji ya Kitaifa.

Kwa hiyo basi, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kisarawe, napenda kuchukua nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi na hasa Mwenyekiti wake wa Taifa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kukamilisha daraja la Benjamin Mkapa ambalo limezinduliwa tarehe 2 Agosti, 2003. Hii inathibitisha azma ya Serikali ya kuondoa kero za wananchi kama ilivyowekwa katika Ilani zote mbili za Uchaguzi za mwaka 1995 na mwaka 2000. *(Makofi)*

Vile vile kwa wale ambao tulihudhuria sherehe za uzinduzi watakumbuka taarifa ambayo ilikuwa imetolewa na wazee wa Kusini iliyosomwa na Mheshimiwa Phillip Magani, kuwa harakati za ujenzi wa daraja hili zilianza tangu miaka ya 1960 pale wananchi wa Kusini walipounda Kamati ya kusimamia ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Mtwara chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Alhaj Nabahani, wakiwemo wajumbe maarufu kabisa kina Mzee Rashid Kawawa na aliyekuwa Waziri wa Ardhi siku hizo, Mheshimiwa Lawi Nangwanda Sijaona na wengine. Lakini Serikali ya *TANU* na baadaye Chama cha Mapinduzi, ikawashauri wakae pembeni kwa sababu jukumu hili lilikuwa la Serikali kwa hiyo basi wakalivalia njuga suala hili. Kwa maana hiyo, tangu Awamu ya Kwanza ya Chama cha Mapinduzi, Awamu ya Pili na Awamu ya Tatu wote wameshughulikia mpaka kufikia uzinduzi wa daraja hili. Kwa hiyo, napenda niwapongeze wote hao walioshiriki katika kuondoa tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndani ya *SADC*, Tanzania inahusika na vyanzo vingine viwili ambavyo ni vya Kimataifa navyo ni Mto Ruvuma na Ziwa Nyasa. Ninaamini kwamba itifaki hii itatusaidia sana katika kuendeleza vyanzo vya maji vya maeneo hayo mawili niliyoyataja. Kwa kutumia mfano ulioonyeshwa na Tanzania katika kujenga daraja la Rufiji, ninaamini kabisa kwamba itifaki hii itaweza kuwahamasisha wananchi wa *SADC* na Serikali zao kuhakikisha kwamba wanaleta maendeleo katika maeneo haya mawili ambayo nimeyataja.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, napenda niishauri Serikali ya Tanzania ichukue jukumu la kuwahamasisha Ndugu zetu wa Msumbiji pamoja na Serikali nyingine za *SADC* ili kinachofuata sasa baada ya daraja la Rufiji iwe daraja la Ruvuma. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewathibitishia Wakoloni kwamba ile ndoto ya Cecil Rhodes ya kuwa na *Cape to... Cairo Road* sasa inatekelezwa na wananchi wenyewe wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa naangalia kwenye hoja hii nimeona kwamba itifaki ilishakuwepo lakini sasa hivi tunachozungumzia ni marekebisho ya itifaki iliyopita. Sasa nilikuwa najiuliza labda ni sababu zipi zimefanya mpaka ije itifaki nyingine? Lakini kwa kusoma Kiambatisho Na.1 na Na.2 itaonekana wazi kabisa kwamba kulikuwa na mapungufu makubwa katika Kiambatisho Na.1 yaani maana yake ni kwamba ile itifaki ya kwanza ilikuwa na mapungufu.

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi mapungufu mawili niliyoyaona moja ni kwamba ile itifaki ya zamani ilikuwa na maeneo machache sana ya maainisho. Kwa hiyo, haikuwa rahisi kwa mtu yeyote anayeisoma itifaki ile na pia hata watekelezaji wangekuta kwamba kuna maeneo yasiyoeleweka. Kwa

mfano, ukiangalia katika itifaki ya kwanza kwenye ukurasa wa 2 hadi wa 4 utaona kwamba mpangilio sio mzuri sana lakini ukiangalia Sehemu ya Nne inaonekana kwamba pamefafanuliwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, la pili, katika itifaki ya kwanza hata sababu za kuileta itifaki ile zimefichwa chini ya mambo mengine *(general matters)* lakini katika itifaki ya pili lililofuata tu baada ya kuainisha ilikuwa ni kuonyesha objectives ya kwa nini itifaki hii ni muhimu kwa *SADC*.

Kwa hiyo basi, inaonekana kwamba uzito mkubwa umewekwa kwenye shabaha yenyewe ili utekelezaji utakapokuwa unafanywa watu wote waelewe maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kwa ufupi tu juu ya itifaki hii tunayozungumzia. Napenda sana kuwapongeza waliofikiria juu ya uundaji wa taasisi za pamoja kwa sababu bila ya hivyo ni rahisi kabisa kila nchi ikaweka mipango yake kukawa na tofauti na wakati mwingine tukafika mahali kama tulipo kidogo hivi sasa baina yetu sisi na Malawi kukawa na migogoro juu ya mpaka na tofauti za maendeleo ya Ziwa. Kwa mfano, katika Ziwa Nyasa ukija upande wa Tanzania, Bandari zetu kwa mfano ile ya Itungi hazikuendelezwa, hatuna vyombo vya usafirishaji vya kuaminika sana, hatukulitumia Ziwa vizuri kwa ajili ya kuvutia watalii.

Mheshimiwa Spika, ukienda pale Itungi wananchi pale wanatengeneza ile mitungi ya kizamani kabisa ambayo ni mizuri sana ambayo ingekuwa ni kivutio kikubwa sana kwa watalii lakini bado watu hawajavijua. Ukienda upande wa Malawi ni tofauti kabisa, Bandari zimejengwa, niliwahi kupata nafasi ya kufika *Mangochi District* ambapo wamejenga hoteli nzuri za kuvutia, wameweka vyombo vya majini vya kuvutia watalii na kwa kweli nchi inaingiza pesa nyingi za kigeni kwa ajili ya maendeleo ya Ziwa. Sasa basi kwa kutumia itifaki hii nchi kama Tanzania inaweza kuiga mfano wa Malawi na pia kwa kuweka taasisi za pamoja naamini kwamba kutakuwa na maendeleo yanayowiana baina ya upande mmoja wa Ziwa na mwingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika ukurasa wa 26 kunaelezwa juu ya usuluhishi wa migogoro. Ninaamini kwamba nchi yetu na nyingine zote katika *SADC* zinaweza kutumia mfumo huu kuondoa migogoro ambayo ingejitokeza. Napenda kuishauri Serikali ya Tanzania pamoja na uhusiano wetu mzuri sana na Malawi na juzi juzi tu hapa tumemkaribisha Rais wao lakini bado liko tatizo la kujua mpaka wa Ziwa letu unaishia wapi, lipo tatizo la jina la Ziwa hili sasa. Watanzania wanaliita Nyasa lakini Malawi wanataka waliite Ziwa Malawi. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kwamba kwa kutumia itifaki hii, Serikali yetu inaweza kuanzisha majadiliano na kuhakikisha kwamba hakutakuwa na migogoro baina yetu na nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikuwa na mengi, napenda kukushukuru kwa kuniruhusu kuchangia katika hoja hii, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kulikuwa na msemaji mmoja tu, lakini kabla sijamwita Mtoa hoja…

**MBUNGE FULANI:** Walikuwa wawili.

**SPIKA:** Aah, kwenye orodha yangu kulikuwa na msemaji mmoja, basi ngoja nitoe tangazo hili kwanza kwamba mjadala unaoendelea kwa hoja zilizopo kwenye Order Paper utakwisha saa 7.00 mchana ili saa 11.00 tuwe na hoja moja tu ya kuahirisha Bunge. Watu wa redio walishaniuliza hoja ya kufunga Bunge itatolewa saa ngapi, sasa ni vizuri na Waheshimiwa Wabunge wakajua kwamba ni saa kumi na moja kamili ndipo Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa hoja ya kufunga Mkutano wa Bajeti na kama kawaida hotuba yake hutangazwa moja kwa moja na Redio Tanzania.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie Azimio la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Makubaliano Mapya ya Matumizi ya Maji ya Kimataifa ya Mwaka 2000 *(Revised Protocol on Shared Water Courses in the SADC Region).*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake yote kwa kufanikisha ujenzi wa daraja kwenye Mto Rufiji, daraja ambalo limepewa jina lake, Mkapa Bridge*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuelezea kidogo adha ambayo sisi tunaotoka Mikoa ya Kusini tulikuwa tunaipata katika sehemu hii ya Rufiji kwa kukosa daraja. Kwa kweli ilikuwa ni usumbufu mkubwa na mara nyingi tulitakiwa tulale pale Mtoni sehemu ambapo pamejaa mbu lakini vile vile kiafya ni sehemu ambayo ilikuwa ya hatari zaidi. Sasa leo kwa kupata daraja lile, nina hakika hatutalala tena pale Rufiji lakini vile vile afya za wananchi wengi wa nchi hii zitakuwa zimenusurika.

Mheshimiwa Spika, daraja lile ni ukombozi sio kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini ya Pwani, Lindi, Mtwara na Ruvuma peke yao, bali ni ukombozi kwa wananchi wote wa Tanzania kuanzia Zanzibar – Kigoma, Tarime – Masasi. Mara nyingi tumezoea kuona Watanzania wa aina zote kuanzia wafanyabiashara, wakulima, wavuvi na hata wafugaji wakisafiri kuelekea Kusini kwenye barabara hii ya Dar es Salaam – Kibiti – Lindi kwa hiyo Watanzania hawa wote wakisafiri wao wenyewe, mizigo yao na hata mifugo yao, kwa hiyo daraja lile ni ukombozi kwa wote hivyo Rais Mkapa na Serikali yake wanastahili pongezi sana*. (Makofi)*

**SPIKA:** Sasa rudi kwenye Itifaki ya maji, hiyo tumesikia lakini sio hoja iliyo mbele yetu.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, samahani sana lakini niwapongeze Ndugu zetu ambao tumewachagua jana kutuwakilisha kwenye Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kipindi hiki. Waheshimiwa hao watatu ni Profesa David Mwakyusa…

**SPIKA:** Tunawajua, wewe changia maji!

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Nashukuru kama tunawajua. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye Itifaki yenyewe, suala la matumizi ya maji ya Kimataifa. Kwa sisi ambao tunatoka kwenye Mikoa ya Ruvuma na Mtwara tunalielewa vizuri zaidi hasa kwa kuelewa kuwa tupo kwenye mpaka na majirani zetu wa Msumbiji na mpaka wenyewe ni Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, Mto Ruvuma kama ilivyo Mito mingi una tabia fulani fulani kulingana na wakati fulani fulani wa mwaka. Kuna kipindi Mto Ruvuma hufurika zaidi na maji yake kusambaa kilomita kadhaa ndani ya nchi yetu halikadhalika ndani ya Msumbiji. Lakini kuna kipindi vile vile Mto huu hukauka hivyo maji yake hupita sehemu fulani tu ya Mto inaweza ikawa upande wa Tanzania na wakati mwingine upande wa Msumbiji. Mto huu vile vile una visiwa kadhaa vinaweza vikawa upande wa Tanzania hali kadhalika upande wa Msumbiji. Mto huu ni muhimu kwa wananchi wa kutoka nchi zote mbili kwa sababu maji yake yanasaidia sana kwa matumizi ya nyumbani, viwandani, uvuvi na usafirishaji.

**SPIKA:** Sasa husisha maneno yako na itifaki basi wewe unatueleza tu hadithi za Mto!

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Kwa hiyo, kama hakuna makubaliano, hakuna maelewano kati ya nchi hizi, maji haya yanaweza kuwa chanzo kikubwa cha migongano. Kwa hiyo, suala la kuwepo makubaliano ni suala muhimu sana ili kuondoa migongano kati ya wananchi wa Tanzania na Msumbiji.

**SPIKA:** Mmh!.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Kwa hiyo, mimi Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Unaunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mimi Mheshimiwa Spika, licha ya kuunga mkono hoja lakini ninapongeza sana Azimio hili na nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuliunge mkono moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nasema ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunikaribisha tena ili nihitimishe hoja yangu. Kwanza napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na wale ambao wamechangia kwa kukaa kimya. Wote nawashukuruni sana maana wote mmeunga mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Eeh, ndiyo.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge watano waliochangia nao ni Mheshimiwa Musa Lupatu, kwa niaba ya Kamati, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Aridi Uledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli suala hili limeungwa mkono na sikusudii kuchukua muda mrefu tena kwa sababu mambo yote yameungwa mkono lakini nakusudia nifafanue maeneo mawili matatu ambayo yaliuliziwa na Mheshimiwa Ngawaiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ngawaiya licha kuunga mkono aliulizia suala la Mto Nile na kwamba hali ikoje ili tujifunze kutokana na matatizo ya Mto Nile. Kwanza napenda kueleza Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli Serikali ya Uingereza na Misri waliwekeana mkataba mwaka 1929 na 1959 wa kutawala maji ya Mto Nile lakini baada ya uhuru tulitangaza kwamba hatukubaliani na mkataba ule na tukaendelea kutumia maji ya Ziwa Victoria kadri tulivyoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, lakini hivi karibuni kimeundwa chombo na nchi hizi kumi zinazotumia maji ya Mto Nile, chombo hiki kinaitwa Nile Basin Initiative na kinaongozwa na Mtanzania, Miraji Msangi ambaye anafanya kazi nzuri sana. Chombo hiki kimekuwa kinajenga asasi na jinsi ya kutumia vizuri maji ya Mto Nile. Hivi sasa mazungumzo ya kisheria yanaendelea ya kufanya cooperative legislation, the legal framework ya jinsi ya kutumia maji ya Mto Nile na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hapa sisi kwa kutokutambua ule Mkataba na Misri tumeanza kutumia maji ya Ziwa Victoria kuyapeleka Kahama na Shinyanga. Kwa hiyo, jambo hili halina matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameuliza vile vile tahadhari tulizoweka. Ningependa kumjulisha kwamba hii ni Itifaki kama mwongozo wa kusimamia matumizi endelevu ya raslimali za maji ya Kimataifa (Trans boundary) kwa nchi wanachama na tahadhari hizo zimewekwa katika vifungu (2), (3) na (4). Vitatu nivitaje, ni kuoanisha sheria na sera za nchi wanachama kuhusu matumizi ya raslimali za maji ili dhana muhimu zifanane. Pili, kuruhusu kuwepo Mikataba mingine kati ya nchi wanachama wa *SADC* au kati ya nchi moja au zaidi. Tatu, kuwa na miradi ya pamoja, ubadilishanaji wa taarifa na takwimu mbalimbali zinazohusu raslimali za maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika hoja ya Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, alisema fedha za kugharamia mradi zitatoka wapi. Sasa Mheshimiwa Ngawaiya huu si mradi ni Itifaki ya mashirikiano fedha zikihitajika wakati huo baada ya kutimiza hatua zinazopaswa zitapatikana kwa utaratibu lakini hii sasa hivi haihitaji fedha, ni Itifaki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, amezungumza sana juu ya Ziwa Nyasa na Mzee Athumani Janguo. Ningependa kuwajibu tu kwamba Ziwa Nyasa mazungumzo yanaendelea vizuri sana na mambo ni mazuri naomba tusiwe na wasiwasi, tusubiri hatua za Serikali mbili zitakapochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, pia amezungumzia umuhimu wa Mikataba ya kusimamia matumizi ya maji na tunakubaliana naye na kwa kweli tunatekeleza Mikataba hiyo ndiyo maana hata katika

Mto Songwe tuna fedha za *NORDIC Fund* ikizingatia Itifaki hii ya mwaka 1995 za kusawazisha. Kwa hiyo, tunauzingatia na inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la uhamishaji wa maji katika Mito limezungumzwa pia na Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, jana na Mheshimiwa Athumani Janguo, leo asubuhi. Lakini kama ninavyosema madhumuni ya Itifaki hii ni kufanya nchi zishirikiane na ziarifiane. Kwa mfano, sisi Serikali ya Tanzania tuna Mradi wa Umwagiliaji kwenye Mto Ruvuma, tumelazimika kuiarifu Serikali ya Msumbiji kwamba tunatumia maji kiasi fulani na hayatakuwa na athari na tumezungumza nao tunaelewana. Kwa hiyo, madhumuni ya Itifaki hii kwa kweli ni kuhakikisha kwamba nchi zinatumia raslimali za maji kwa mahusiano mazuri bila vita wala mapambano kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hoja zote zimeunga mkono. Napenda kuwashukuru tena kwa kutuunga mkono. Samahani, nimekosa jina la Executive Director ni Miraji Msuya siyo Miraji Msangi, ambaye nimesema anafanya kazi nzuri. Narudi tena kusema kwamba hoja imeungwa mkono. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tumetimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Matumizi ya Maji Kitaifa liliridhiwa na Bunge)

**Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha Kufuta au Kusamehe Madai au Hasara itokanayo na Upotevu wa Fedha au Vifaa vya Serikali**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa pamoja na wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu za Serikali kwa mchango wao mkubwa wakati wa kujadili hoja iliyo mbele yetu. Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri uliotolewa umezingatiwa kikamilifu na Serikali katika kuboresha Azimio.

Mheshimiwa Spika, naomba niwasilishe tena mbele ya Bunge lako Tukufu mapendekezo ya hoja ya kuliomba Bunge likubali kufuta au kusamehe madai na hasara ambazo hazilipiki zinazotokana na upotevu wa fedha au vifaa vya Serikali kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa fedha za umma ya mwaka 2001 (The Public Finance Act, 2001).

Mheshimiwa Spika, kabla ya Sheria mpya ya Fedha ya Mwaka 2001 kuanza kutumika, Waziri wa Fedha alikuwa na uwezo wa kufuta potevu za fedha na mali za Serikali, kusamehe madeni yasiyolipika na kufuta maduhuli yasiyokusanyika kwa kutumia Azimio la Bunge chini ya vifungu namba 7 na Namba 29 vya Exchequer and Audit Ordinance ya Mwaka 1991.

Kulingana na kumbukumbu za tangazo la Serikali Na. 210 yaani GN 210 la tarehe 1 Oktoba, 1971 Waziri wa Fedha amekuwa akiidhinisha na kukasimu mamlaka ya ufutaji kwa baadhi ya maofisa kwa viwango mbalimbali kwa mujibu wa Azimio la Baraza la Kutunga Sheria Legical la tarehe 19 Aprili, 1960 na kifungu Na. 29(3) cha Exchequer and Audit Ordinance mwaka 1991. Sheria mpya nayo ina utaratibu unaofanana lakini haikuendeleza kile kibali kilichokasimiwa chini ya Sheria ya zamani. Aidha, kanuni mpya za fedha zimeimarisha uwajibikaji wa maofisa na upotevu wanaosababisha.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika kikao cha Bajeti cha mwaka jana Serikali iliwasilisha mapendekezo ya Azimio kwamba Bunge likasimu madaraka kwa Waziri wa Fedha ili aweze kufuta hasara za Serikali.

Hata hivyo, Azimio hilo liliahirishwa kwa kuwa wengi wa Waheshimiwa Wabunge hawakuliafiki. Azimio ninalolitoa leo ni tofauti na lile la awali kwani safari hii tunaomba Bunge ndilo lifute au kusamehe hasara ambazo tayari zimekwishakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali na kujadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaani *PAC*. Tunazo potevu nyingine ambazo tunazifanyia kazi na mara baada ya kukamilika na kujadiliwa na *PAC* tutazileta ili Bunge liweze kufuta au kusamehe. Utaratibu huu utaendelea kila panapokuwa na haja ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetafakari kwa kina hoja za Waheshimiwa Wabunge na imezingatia ushauri wa Bunge kuhusu jambo hili. Aidha, Serikali inatambua kwamba mapato ya Serikali ni lazima yakusanywe kama yalivyopangwa. Fedha za Serikali ni lazima zitunzwe na zitumiwe kama zilivyopangwa na kwamba vifaa vya Serikali havina budi kutunzwa kwa mujibu wa sheria.

Hata hivyo, wakati mwingine inatokea bahati mbaya kwamba mapato yaliyopangwa hayalipiki au fedha na vifaa vya Serikali vinapotea katika mazingira fulani. Kwa mfano, kuna madai yanayotokana na kampuni au mashirika ambayo yameshafilisika au upotevu wa fedha ambazo ziliibiwa huko nyuma na walioiba ama wamefariki au walishachukuliwa hatua za kisheria lakini fedha hazikurudishwa Serikalini.

Katika kipindi cha miaka michache iliyopita matatizo ya namna hii yamedhibitiwa kwa kiwango kikubwa kwa kutunga Sheria mpya kama zile za Usimamizi wa Fedha za Umma na Ununuzi wa Vifaa. Usimamizi wa matumizi ya Serikali ni imara zaidi sasa. Udhibiti wa fedha za Serikali kupitia IFMS umeimarika kwa kiwango kikubwa na hatua nyingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mabadiliko hayo ya Sera, Sheria na usimamizi wa mali ya umma, wimbi la upotevu, hasara na malimbikizo ya makusanyo ya mapato ya Serikali imepungua kwa kiasi kikubwa. Kwa maana hii madai na potevu zinazopendekezwa kufutwa ni za zamani na hazilipiki na zisipofutwa zitaendelea kubaki kwenye vitabu vya Serikali na kuendelea kujitokeza kwenye taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali bila kuongeza tija katika shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetafakari kwa kina mapendekezo yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na kwa kuzingatia ushauri wa Bunge, Serikali imeandaa jedwali la orodha ya madai yatokanayo na upotevu wa fedha na vifaa ambayo imepitiwa na kukubaliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hatimaye kuwasilishwa katika Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), ili Kamati ichambue mapendekezo ya Serikali ya kufuta hasara hizo na kutoa mapendekezo yake.

Mheshimiwa Spika, msingi wa Azimio hili ni Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2001. Kifungu 43(1) cha Sheria hii ambacho kinasomeka, naomba kunukuu: *"The National Assembly may by resolution authorize the Minister to the extent specified in the resolution to abandon and remit any claims by or on behalf of the Government or any service thereof and to write off losses of money or stores belonging to the Government or provided for the public service."*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ambayo naiwasilisha mbele ya Bunge hili, hasara zimegawanyika katika sehemu kuu tatu. Mgawanyo huu umelenga kuainisha kwa uwazi zaidi hasara hizo ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuzielewa vizuri na hatimaye kufikia uamuzi ulio sahihi. Hasara hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Zile zinazohusu potevu za fedha na vifaa shilingi 16,853,734,726.61/=.

(b) Zile zinazohusu mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa ya shilingi 45,279,480,285.07/=.

(c) Zile ambazo zinahusu usawazishaji wa kumbukumbu katika vitabu shilingi 10,716,802,110.32/=.

Mheshimiwa Spika, jumla yote ni shilingi 72,850,017,122.30/=. Maelezo ya hasara hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, hasara zinazohusu potevu za fedha na vifaa. Katika eneo hili hasara zinazohusika hapa ni za kuanzia miaka ya 80 hadi Juni, 2002. Hasara hizi zimetokana na sababu mbalimbali zikiwemo wizi wa mali na fedha, kushuka kwa thamani ya shilingi kulinganisha na fedha za nje *(exchange rate losses),* ubadhirifu, kusinyaa kwa bidhaa kama vile chakula yaani shrinkage, vifaa kupitwa na wakati (*obsolute*), mhukizo (evaporation) kama vile mafuta na kadhalika na uzembe (*negligence*). Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 11,288,215,236/= ilikuwa ni hasara iliyotokana na shughuli za uendeshaji wa kitengo cha Taifa cha Hifadhi ya Chakula (*SGR*). Hii inatokana na ukweli kwamba madhumuni ya *SGR* ni kupunguza makali ya bei ya vyakula wakati wa upungufu na hivyo kuuza vyakula vyake kwa bei ambazo ni pungufu ya zile za soko huru ili walengwa waweze kumudu kununua chakula hicho. Wakati huo *SGR* ilinunua mahindi kwa bei kubwa kuliko bei waliyouzia na hivyo kupata hasara hiyo ambayo haiwezi kurudishwa.

Mheshimiwa Spika, pili, mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa. Hasara katika eneo hili ni ile inayotokana na Serikali kushindwa kukusanya mapato au maduhuli kutokana na sababu mbalimbali kama vile mabadiliko ya sheria za kodi, ubinafsishaji wa mashirika ya umma na gharama ya ukusanyaji kuwa kubwa kuliko kiasi kinachopatikana na maamuzi mbalimbali ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, hapa napenda nitoe mfano ulio hai ili kuwapa picha halisi. Moja ya benki za mwanzo kuanzishwa hapa nchini baada ya kuingia katika soko huria ni benki ya Meridian Biao, Serikali ilikuwa inaidai benki hiyo kodi ya mapato wakati ilipofilisika mwaka 1994. Baada ya taratibu za ufilisi kukamilika Serikali imejikuta haina inachokipata kwani mapato yaliyopatikana kupitia kwa mfilisi hayakutosha kulipa wadau wote ikiwemo Serikali yenyewe. Kwa msingi huo, Serikali haina jinsi ya kukusanya deni hilo kwani halikusanyiki.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji wa mashirika ya umma umechangia pia kwa Serikali kushindwa kukusanya mapato. Kufuatia kubinafsishwa au kuwekwa kwenye orodha ya kubinafsishwa madeni ya mashirika ya umma ya kodi na mengine, yamekuwa yakiwasilishwa Serikalini, kwa hiyo wawekezaji hawataki kurithi madeni ya mashirika wanayonunua. Kwa misingi hiyo, Serikali inalazimika kufuta madeni ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, tatu, hasara zinazohusu usawazishaji wa kumbukumbu katika vitabu. Katika eneo hili hasara zinazotokana na sababu za kutofuata taratibu kikamilifu, kukosekana kwa nyaraka au madai kati ya idara na idara za Serikali. Mara kadhaa yanakuwepo matukio ya dharura halafu Serikali hulazimika kutafuta fedha kutoka vyanzo vyake mbalimbali ili kukidhi mahitaji hayo. Katika hali kama hiyo taratibu za kifedha zinaweza zisifuatwe kikamilifu. Maafisa Wahasibu kuwajibika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001, kanuni za fedha namba 16 na 19.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, hasara na potevu hizi zinahusu kipindi ambacho Serikali haijaanza kuchukua hatua thabiti za kudhibiti na kusimamia mapato na matumizi ya Serikali. Sasa Serikali imerekebisha mapungufu mengi yaliyokuwepo kwa kuanzisha mtandao wa kompyuta IFMS na kutunga Sheria mpya ya Fedha. Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001, inaeleza wazi jinsi ya kushughulikia potevu au hasara za Serikali. Sheria hiyo inawawajibisha Maafisa Wahasibu katika kuhasibu hasara au potevu hizo kwa vile wao ndiyo wasimamizi wakuu wa makusanyo na mapato ya matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, sheria hii ya fedha inawawajibisha Maafisa Wahasibu wote katika kutoa hesabu kamili ya hasara au potevu ya mali zote za Serikali. Katika mwaka wa fedha kila Afisa Mhasibu anatakiwa kutunza daftari la matukio ya upotevu wa fedha na vifaa kwa mujibu wa kanuni za Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001. Mwisho wa mwaka wa fedha kila Afisa Mhasibu anatakiwa kutoa taarifa ya hasara hizo.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa zao kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, Maafisa Wahasibu wanahitajika kuelezea jinsi hasara hizo zilivyotokea na juhudi zilizofanywa katika kupunguza au kuepuka hasara hizo na vile vile hatua zilizochukuliwa dhidi ya mtumishi aliyesababisha hasara hizo. Kazi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ni kutengeneza jedwali linaloonyesha potevu zote zilizowasilishwa na Maafisa Wahasibu na hatimaye taarifa huletwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, jumla ya hasara isiyolipika inayowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ni shilingi 72,850,017,122.30 kama ilivyoonyeshwa katika jedwali ambalo nimeliambatisha pamoja na hotuba hii na ambalo limetolewa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Napenda nieleze tena kwamba kumbukumbu hizi za hasara au upotevu ni sehemu kubwa ya hoja za ukaguzi kwa Wizara na Idara za Serikali. Kufutwa kwa hasara hizi kutapunguza kwa kiasi kikubwa hoja za ukaguzi na papo hapo kuleta picha iliyo sahihi ya mahesabu ya Serikali na Taifa kwa ujumla sio tu mbele ya wananchi wetu bali hata mbele ya wadau wengine wa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa nisome Azimio husika kama ifuatavyo:-

KWA KUWA kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya Mwaka 2001, Waziri wa Fedha anayo mamlaka ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kugawa na kuidhinisha matumizi ya fedha hizo na baada ya kupata idhini ya Bunge kufuta hasara itokanayo na upotevu wa fedha, vifaa vya Serikali, madai ya kodi pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya Mwaka 2001, Bunge linaweza kwa Azimio kutoa idhini kwa Waziri wa Fedha kufuta hasara itokanayo na upotevu wa fedha, vifaa vya Serikali, madai ya kodi pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi;

NA KWA KUWA upo upotevu wa fedha na vifaa katika vitabu vya hesabu za Serikali ikiwa ni pamoja na usawazishaji wa kumbukumbu katika vitabu hivyo;

KWA HIYO BASI kwa mujibu wa kifungu 43(1) cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya Mwaka 2001, sasa Bunge hili linaazimia kuidhinisha Waziri wa Fedha kusamehe na kufuta upotevu wa Fedha na vifaa, kusawazisha kumbukumbu katika vifaa kama vifuatavyo:-

(a) Upotevu wa fedha na vifaa shilingi 16,853,734,128.91/=.

(b) Mapato au maduhuli yaliyoshindikana katika vitabu shilingi 45,279,480,285.07/=.

(c) Usawazishaji kumbukumbu katika vitabu shilingi 10,716,802,110.32.

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu upotevu huu yapo kwenye kabrasha ambalo limegawiwa kwenu Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Yale maneno ya mwisho kwamba maelezo kuhusu upotevu huu yapo kwenye kabrasha siyo sehemu ya Azimio. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*)atoe maoni ya Kamati yake. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba na mimi niungane na Wabunge wenzangu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge tuliowachagua jana ili kuliwakilisha Bunge letu katika Baraza la Chuo Kikuu. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Ruth Msafiri, lakini nitoe pongezi za pekee kwa Makamu Mwenyekiti wa *PAC*, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niungane na Waheshimiwa Wabunge kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kufanikisha ujenzi wa daraja la Rufiji. Lakini ili salaam hizi na shukrani hizi zikamilike hatuna budi kuwashukuru vile vile Kuwait Fund na Saudi Fund ambao bila mchango wao, daraja hilo lisingekuwepo. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Kamati ya Hesabu za Serikali naomba kutoa maoni ya Kamati kama ifuatavyo. Kwa mujibu wa Kanuni kifungu 43(5)(b) ya mwaka 2003, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Hesabu za Serikali juu ya Azimio lililotajwa hapo juu. Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mama Blandina Nyoni, Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa jinsi alivyowasilisha kwenye Kamati maelezo ya kina, yenye ufafanuzi juu ya madhumuni ya Azimio hili. Aidha, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, Manaibu wake Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib na Makatibu Wakuu kwa namna walivyoisimamia Wizara hii. Sisi sote ni mashahidi kwamba Wizara ya Fedha imejitahidi kuboresha mambo mengi kwa kipindi kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitawashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yangu kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wao. Naahidi nitashirikiana nao katika kutimiza wajibu wangu kwa niaba ya Bunge letu ambalo ndicho chombo kinachowawakilisha wananchi wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Naomba nichukue nafasi hii kuwatambulisha kwenu, kwanza ni Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, ambaye ni Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Abdulla Lutavi, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Asha Ngede, Mheshimiwa Leonard Shango na Katibu wetu Ndugu Anselm Mrema.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Waziri chimbuko la Azimio hili ni Sheria mpya ya Fedha pamoja na kanuni zake ambapo ni jukumu la Maafisa Wahasibu kuhakikisha kuwa mapato na matumizi ya Serikali yanakusanywa na kutumiwa kama ilivyokusudiwa na kuhakikisha kuwa hasara haitokei. Lakini kutokana na sababu mbalimbali hasara hutokea kutokana na wizi, upotevu wa vifaa na vile vile kushindwa kukusanya mapato ya Serikali. Kabla ya sheria mpya ya fedha, jukumu la kufuta lilikuwa ni la Hazina chini ya Waziri wa Fedha lakini kufuatia Sheria Mpya ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndilo lenye jukumu hilo. Sheria inatamka kuwa taarifa ya hasara, potevu za Serikali ziandaliwe na Mhasibu Mkuu wa Serikali na kuwasilishwa mbele ya Kamati ya Hesabu za Serikali ambayo itachunguza na hatimaye kutoa mapendekezo ya kufuta au hatua nyingine za kuchukuliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na utaratibu niliotaja hapo juu Kamati ilipokutana tarehe 4 Agosti, 2003 kwa idhini yako na kufanya kazi hiyo nataka kuchukua nafasi hii kumpongeza ndugu Thomas Kiama, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pamoja na wataalam wake kwa namna walivyoshiriki katika zoezi la kuchambua na kuzifanyia kazi hasara hizo. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ni matunda ya juhudi za pamoja za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa hasara, upotevu wa vifaa vya Serikali kwa jumla ya shilingi 216,170,205,090.85/=. Kamati iliridhika kuwa kiasi cha shilingi bilioni 16,853,734,726.91/= kinachohusu potevu za fedha na vifaa kifutwe hasa ukizingatia kwamba hasara inayohusika ni ya miaka mingi iliyopita kuanzia miaka ya 80 hadi Juni, 2001. Aidha, kiasi kikubwa cha hasara hii kimetokana na sababu mbalimbali zikiwemo wizi, kushuka kwa thamani (Exchange Rate Losses), ubadhirifu, kusinyaa na kupitwa na wakati, mhukizo wa mafuta na uzembe.

Mheshimiwa Spika, katika hasara hiyo ya shilingi 16,853,734,726.91/=, sehemu kubwa imechangiwa na Fungu 43 la Wizara ya Kilimo na Chakula ambapo kiasi cha shilingi 11,288,215,236/=

kinachohusu ununuzi na usambazaji wa mahindi ya njaa kinaombwa kufutwa. Kamati baada ya kufanya uchambuzi wa kina imeridhika kwamba hasara hiyo ilisababishwa na mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kifungu cha 8 hadi 12 kuhusu "Magaidi" kuhamishwa kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine *(extradition)*, inaweza kutumiwa na Mataifa yenye nia za kimaslahi na kimkakati kufanikisha kulalamikia namna wafungwa wa kiarabu na kadhalika kutoka Afghanistan na Pakistan wanavyoteswa kule *Guantamano Bay*, Cuba na Majeshi ya Marekani. Huko Marekani inakataa kuwatambua wapiganaji wa Al-Qaeda kama mateka wa kivita na inataka dunia isilaani mateso hayo. Watetezi wote wa haki za binadamu, bado wanaishutumu Marekani kufuatia unyanyasaji wa hali ya juu wa wafungwa hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Kimataifa inayostaarabika haiwezi kuendelea kuliachia Taifa moja kubwa kujivisha nafasi ya Polisi wa Kidunia *(Global Cop)* na kutumia misuli yake kuyachagiza na kuyafolenisha Mataifa madogo madogo kwa lengo la kujipatia faida iliyokithiri *(Super Profit).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Kimataifa pia haina nafasi maalum ya kumwendeleza au kumdekeza yeyote yule anayetumia visingizio vyovyote kukatisha maisha ya watu wasio kuwa na hatia, hasa akina mama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, si jambo jema pia kwa hao wanaodaiwa kuwa ni "Magaidi" kumuua yeyote anayekatisha mbele yao, kwa kudaiwa ni mmoja katika wanaokwamisha maslahi yao ya kisiasa, kiitikadi, kidini na kadhalika. Mauaji ya watu wasio na hatia hayawezi yakahalalishwa na kitu chochote kile na ni lazima yalaaniwe kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linalojitokeza katika nchi nyingi za Kiafrika, hasa zile zenye ugaidi wa aina fulani katika demokrasi ya kiushindani, wakati mwingine ni kule kuubandika Upinzani wa kawaida wa kisiasa chapa ya ugaidi wa Kitaifa na Kimataifa. Wananchi wakiandamana mitaani kwa amani kabisa na Wapinzani wakiandaa mikutano mikubwa ya hadhara, hivyo vyote wakati mwingine huvishwa joho la ugaidi, kwa lengo la kuwafanya wachukiwe na watu wa ndani ya nchi husika au Jumuiya ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wa nchi na nchi katika upelelezi na mambo ya Kisheria ni lazima utangulize mbele heshima ya kila Taifa, badala ya Taifa moja kuliamrisha na kulipigisha kwata Taifa jingine huru. Hii tabia ya nchi moja kujaza makachero wake kibao katika nchi nyingine ni kitendo cha kuidhalilisha nchi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia hii ya wakubwa pia ijitahidi kukwepa mambo yanayowazalisha hao tunaowaita "Magaidi". Wakubwa kabisa wa ulimwengu huu wajitahidi sana kukwepa mambo yanayowazalisha hao wanaoitwa magaidi. Ni kweli kuwa magaidi wakati wowote ni tatizo. Lakini vitendo vinavyozalisha magaidi ni tatizo zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, Kambi ya Upinzani inaunga mkono kuridhiwa kwa Mkataba huu na inaipongeza sana Serikali kwa kuleta kwa wakati unaofaa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia. Naomba kabla ya kuanza niwapongeze wenzetu Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuwakilisha Wabunge katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Nawaomba waende wakafanye kazi nzuri pale Chuoni. Ni Chuo ambacho kimetuzalisha sisi wote, sisi ambao tumepitia kwenye huu mkondo wa Elimu ya Chuo Kikuu ndani ya nchi yetu kwa wakati ule tuliopitia, kwa hiyo, tunawaomba mfanye kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, kwa kujali wananchi wake na kwa kutii matakwa ya Katiba. Suala la ugaidi ni suala la usalama wa Taifa, ni suala la usalama wa raia. Katika Katiba yetu, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 14, kila mtu aliye kwenye nchi hii anayo haki ya kuishi na anayo haki ya kupata ulinzi kutoka kwenye Taifa

letu. Hakuna mtu yeyote ambaye ata-*exercise* zile haki zake za kibinadamu katika nchi hii kwa njia ambayo ataweza kumwumiza raia mwingine wa nchi hii. Moja kati ya njia za kutumia uhuru wa mtu na kuumiza mwingine ni hii njia ya ugaidi kwa ajili ya kulazimisha nchi, Serikali au raia kukubaliana na msimamo wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu na Serikali ya Tanzania ilishatambua umuhimu wa kutii hayo matakwa ya Katiba. Mwaka 2002, tulipitisha sheria ya kupigana na Ugaidi. Wakati ule tunaipitisha hatukuwa tumeridhia huu Mkataba japokuwa ulikuwa umeshasainiwa na Rais wetu. Hiyo haidhuru na hakuna jambo lolote baya lililotokea kwa sababu huu Mkataba hauhusu kupigana na ugaidi ndani ya nchi bali unahusu mashirikiano ya Serikali za *SADC* katika kupigana na ugaidi katika eneo letu la *SADC*. Kwa hiyo, hakuna kitu chochote kinachofanya ile sheria na huu Mkataba vipingane au tuonekane kwamba, tulikimbia haraka mno kabla ya kufikia makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkataba huu ibara ya 4(2)(a), wamekubaliana viongozi wetu kwamba, nchi zote za *SADC* ziwe na wajibu wa kuzuia nchi zao kutumika kama vituo vya kupanga au kuendeshea ugaidi. Sasa hivi ugaidi ulio mkubwa zaidi ni ugaidi wa Kimataifa. Wakati tukipitisha ile sheria ya kuzuia Ugaidi, tulikuwa tunapata Upinzani kwamba, sheria ilikuwa inapinga haki za binadamu. Tumeona jambo ambalo limetokea Kenya. Kenya wamekuwa wanapinga sana sheria kama yetu lakini ni juzi tu, mtu amekamatwa kwa kushukiwa ni gaidi anasindikizwa Polisi akajilipua na askari akafa. Kwa hiyo, katika kupigana na ugaidi ni lazima kuwe na hatua ambazo sio za kawaida, sio jinai ya kawaida, ni jinai ambayo inaweza ikaondoa maisha ya mtu mara moja. Kwa hiyo, huwezi kuchukua haki za binadamu chini ya sheria ya jinai katika kupigana na ugaidi kwa sababu hujui ni lini atakuua. *(Makofi)*

Yule maskini marehemu askari wa Kenya, hakuwa amejua kwamba yule gaidi angejilipua. Lakini hata hivyo, ninayo *concern* juu ya haya makubaliano ya kuruhusu *investigation* zifanywe kuruhusu Polisi wa nchi moja kufanya kazi ndani ya nchi nyingine. Ni wazo zuri kushirikiana. Lakini ningeshauri kwamba, nchi zetu ziepuke *scenario* kama *scenario* ya Marekani kupeleka *FBI* katika nchi nyingine, wao ndio wanakuwa wakamataji na badala ya kupitisha wale washtakiwa kwenye mikondo ya sheria katika nchi ile, wanaamua kutorosha watu ambao wanawashuku Magaidi. Ninafurahi sana kwamba, katika Mkataba huu kuna makubaliano kwamba, Gaidi yeyote atakayeshukiwa atashughulikiwa kwa sheria ya nchi ile ambayo amekamatwa na kama ni kupelekwa kwenye nchi nyingine basi zile sheria za *extradition* za ile nchi ambayo amekamatwa huko zitatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hivyo, sina maana katika nchi za *SADC* tuna mbabe kama Marekani. Mimi nafikiri katika nchi za *SADC* tunaishi maisha ya undugu sana na haitatokea kitendo kama kile kilichotokea Malawi kwa washukiwa kutoroshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningeomba kumalizia kwa kusema kwamba, ninaunga mkono hii hoja na tumechelewa mno kuridhia huu Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Afrika dhidi ya Ugaidi wa mwaka 1999. Mimi kabla ya yote, naunga mkono Mkataba huo mia kwa mia. *(Makofi)*

Nawashukuru pamoja na kuwasifu Waziri wa Mambo ya Ndani, pamoja na Naibu wake, kwa kufanya kazi nzuri ambayo kusema kweli sisi sote tunaishuhudia na nawaombea kwa Mwenyezi Mungu, awape nguvu waendeleze kazi nzuri. *(Makofi)*

Namsifu pia Mzee Malecela, ambaye kusema kweli amewasilisha maoni ya Kamati na nayaunga mkono maoni yote aliyoyasema na kwamba, kusema kweli yamelenga pale ambapo tunakusudia suala la ugaidi kuufyeka kabisa na kuumaliza. Ahsante sana namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kusahau wale waliochaguliwa kutuwakilisha katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Professa Mwakyusa na Mheshimiwa Ruth Msafiri, wote tunawaomba wakatuwakilishe vizuri na wakatoe picha ile ya Bunge hasa lililokomaa na la kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda sasa nianzie pale alipoishia Dr. Lamwai. Kwamba, tukio lililotokea Malawi la kuchukuliwa watuhumiwa watano, watuhumiwa wale wakapelekwa Zimbabwe pamoja na Sudan kuhojiwa na kuchunguzwa, kwa bahati mbaya sasa ikaonekana kwamba, hawahusiani kwa karibu au kwa mbali na kikundi chochote cha ugaidi au na ugaidi wa namna yoyote na kuachiwa ni kitendo ambacho kusema kweli kinasikitisha na kinatia mashaka. Kwa nini nasema hivyo?

Wale walikuwa ni walimu, walikuwa wanafundisha elimu ya dini pale Malawi, Elimu ya Kiislamu, wengine wamekwenda kufanya kazi kama ni wahubiri wa dini ya Kiislamu. Sasa hii inaonyesha kana kwamba, hawa wahubiri au Waislamu wanaofundisha katika shule au vyuo inaonekana kwamba, wao wakati wote wanaweza wakafanya ugaidi kana kwamba yule anayekwenda kufundisha au kuhubiri uislamu wakati wowote anaweza kufanya ugaidi. Sasa hili ni tukio ambalo kusema kweli zito na baya. Kuhusishwa ugaidi na uislamu au na mwislamu anayefanya kazi ya dini. *(Makofi)*

Hili ni jambo baya kweli kweli na lazima tulikemee hasa hasa likitokea katika nchi moja ambayo hii Itifaki leo tunayoizungumzia yaani katika nchi 14 kati ya zile za *SADC.* Kusema kweli ni jambo zito na ni jambo ambalo haliwezi kuvumiliwa. Hata hiyo, *Convention* yenyewe tunakuwa tunaizungumza iko wazi kabisa katika sehemu ya 3 (2) ibara ya 2 ikielezwa kwamba: *"state parties shall adopt any legitimate measures aimed at preventing and combating terrorist acts in accordance with the provision of the convention and their irrespective national legislation in particular. They shall do the following".* Kuna mambo pale (a), (b) (c), nataka kusoma (d). *"Strengthen the protection and security of persons. Diplomatic and consular, commissions premises of regional and international organizations accredited to a state part, in accordance with the relevant conventions and rules of international law".*

Sasa kwa maana hii mimi nasema kwamba, hawa watu ni lazima wahifadhiwe wale ambao wanaokwenda katika nchi nyingine isiwe kwa tuhuma ndogo tu basi tayari imeshachukuliwa kwamba wao wanataka kufanya uhalifu, mpaka kuwe na sababu ingawa Mheshimiwa Lamwai, amesema hapa kwamba, hawezi kushughulikia na sheria ndogo yoyote ya jinai kwa sababu lile ni jambo lililokuwa ni la hatari kama ilivyotokea Kenya. Ni kweli ! Lakini pamoja na hivyo tuhuma zile ziwe hasa nzito za kuweza kuona kwamba, kweli huyu anataka kufanya ugaidi na si tu kwa sababu ni kwamba yeye umemwona ana ndevu ndefu, anavaa kofia hivi, amevaa kanzu sasa huyu ni gaidi. Hili jambo halikubaliki, ni jambo halifai kabisa. Au ana sharubu hivi eeh. Sasa katika hali hii nasema na hili ni jambo ambalo linavunja moyo.

Mimi nataka niwaambie Dini ya Kiislamu inapinga ugaidi kwa aina zote za ugaidi na iko kali sana. Nataka kuwaambieni hapa mimi nimesoma Kiarabu, nataka kuwambieni aya hizo za *Qoran* pamoja na hadithi za Kiongozi wa Dini ya Kiislamu akipinga kabisa matukio yoyote ya ukatili na ugaidi na anayefanya hivyo si Mwislamu. Mimi nataka kusoma aya. Katika sura ya 3 aya karibu ya 146 inasema wazi tu *"Mankatala nafsani fakaanama katalani ndassa jamiani. Waman-ayahaya fakaanama ayanasa jamiani".* "Mtu mwenye kuua nafsi moja (mtu mmoja) ni kana kwamba ameua watu wote duniani na mtu anayeihoisha na kumfanya hai binadamu mmoja kana kwamba amewafanya hai binadamu wote duniani au ulimwenguni". *(Makofi)*

Ni wazi kabisa hizo ni *regulations* na hadithi za Mtume, ambaye Waislamu sisi tunamfuata amesema hadithi ziko chungu nzima karibu 60, ninazisoma 3 tu. Anasema hivi: *"Al Muslim mansaliman-nasa bilisanii wayadihi".* "Muislamu ni yule aliyewasalimisha watu kwa ulimi wake na mkono wake" (Hadithi ya Mtume Muhammad - *S.A.W.*). Watu wawe salama huyo ndiyo Mwislamu, hakuna vingine. Halafu kuna nyingine *"Layuminu ahadukum hata yuhibu liakhini manyahibbu linafsihi".* Hii imesemwa katika dini nyingine. "Hawezi kuwa mmoja wenu anaamini anajitia yeye Mwislamu au muumini mpaka ampendelee ndugu, ampendelee mwenzake lile analopendelea mwenyewe" (Hii ni Hadithi ya Mtume Muhammad *S.A.W.*). *(Makofi)*

Pia hadithi ya mwisho *"La dharar wala dhirar",* "Mtu asifanyiwe dhara wala asimdhuru mwingine wala yeye asidhuriwe aishi katika salama. (Hii ni Hadithi ya Mtume Muhammad *S. A. W.*). Kwa hiyo, uislamu uko mbali kabisa na ugaidi. Sasa mimi naona ajabu kwamba, Waislamu sisi tuna balaa gani jamani, hakuna sababu yoyote ya kuhusisha uislamu na ugaidi, ni kitu ambacho hata hapa Tanzania wamekamatwa Masheikh pamoja na wahubiri kule Tanga, pamoja na Iringa na kadhalika, kwa sababu tu wanafundisha dini. Hili jamani lazima tulikemee, tulipinge kwa nguvu zote, litatuletea matatizo. *(Makofi)*

Hata mtu akionekana Muislamu kama mimi msomi hivi, wakati mmoja nilipokuwa Chuo Kikuu cha Edinburgh, alipita mtu mkubwa tu akaniuliza aah wewe Mswahili uko hapa unafanya nini? Sasa mimi nikashangaa Mswahili maana yake nini, Mswahili anayezungumza Kiswahili au nikajua Mswahili maana yake Muislamu ambaye kusema kweli yeye wakati wa sasa hata akisoma anaonekana ni mshamba tu, mtu limbukeni tu. Eeh ndio! Hapa hapa wakati fulani jamaa mmoja nje hapa aliniita Professa Maji Marefu, hii Maji Marefu amelipata wapi? Mbona kebehi hii ya *yakhe yakhe,* Muislamu hata akisoma akifika wapi ni *yakhe* tu. Ni mtu wa kawaida wala hana lolote au chochote. Sasa hili jambo litaweza kutufarikisha, watu tuko pamoja, Taifa moja hebu tukubaliane tuwe na msimamo mmoja jamani. Tusidharauliane wala tusishutumiane. *(Makofi)*

Baba wa Taifa ametuasa na wasia ule lazima tuuchukue, tukitaka tuwe Taifa moja ni lazima twende pamoja na kusiwe na *second class citizens,* watu wa tabaka la pili. Lazima tuangalie hizi tofauti za dini, lazima tuzizungumzie, tukizungumza ndio ziondoke kusiwe mtu anazungumza akaidharau dini nyingine, huo ndio udini mkubwa. Watu wengine wakajiona bora kuliko wengine, wa dini fulani wakajiona bora kuliko wengine, huo ndio udini mkubwa kweli kweli kuliko vingine, lazima tuukemee. Lazima tuwe pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha mwisho ni kwamba, utaona sisi tuna bahati mbaya kidogo. Wakati ule alipokuwa Naibu Waziri Mkuu, cheo hicho kilikuwepo wakati wa Ndugu Mrema, alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, alikuwa wakati huo Naibu Waziri Mkuu. Alimwita kichaa Mheshimiwa Lamwai, leo alikuwa mwenzake *NCCR- Mageuzi* sasa ameshakuwa CCM. Sasa wenzetu wa Iran walitusaidia kule Rufiji Segeni ili kuweza kuanzisha kilimo cha umwagiliaji ikawa wameleta *container* la vyombo vya umwagiliaji pamoja na ujenzi wa nyumba nafuu. Yule bwana alisema kwamba, Waislamu wanaleta silaha kutaka kufanya Jihad, kwa hiyo, ikawa sokomoko kubwa kabisa ma-*container* yale yakaangaliwa na haikuonekana silaha hata moja, kumbe ni vyombo tu. Ikaingia balaa mradi wenyewe ule mpaka leo hata huo mradi wa umwagiliaji unakwenda ovyo ovyo tu. Hata ule ujenzi wa nyumba za gharama nafuu ukasimama kabisa.

Sasa nasema jamani mtuone sisi wananchi wenzenu ikiwa katika hali hiyo ya ujenzi wa Taifa tunataka kujenga pamoja. Hiyo *TANU, TAA,* tumeanza wote. Sasa suala la ugaidi lisihusishwe na uislamu na mwislamu yeyote. Mkimwona gaidi huyo maana yake ni kwamba, hata uislamu hana. Hata ikiwa ni Mwislamu basi mkisikia ni gaidi uislamu hana. Kwa hiyo, asihusishwe kabisa na uislamu. Ikiwa hivyo mbona hapa kifungu cha mwisho kinachozungumza hapa kifungu namba 3 kwa kusaidia wale waliokuwa wanahujumu kwa mfano, kule Angola nani aliyekuwa anamsaidia Savimbi kwa ajili ya kuihujumu Serikali halali ya *MPLA* ya Angola pale?

Mheshimiwa Naibu Spika, nani aliyekuwa anamsaidia Mobutu Seseseko, nani aliyefanya vile? Sasa wale waliokuwa wametokea Palestina kule na ugaidi wa kujilipua mabomu sio wanataka kujiondoa isipokuwa wamevamiwa hawa wamechukuliwa ardhi yao, wamedhulumiwa ndiyo kwa maana sasa hakuna njia yoyote kwa njia ya Baraza la Usalama wameshindwa, kwa njia zozote za usalama wameshindwa. Njia ya sasa ya *violence* wameona hiyo njia pekee ya kufikia Waisrael. *USA* ingemshauri ndugu yake yule Muisrael ili aweze kuacha uhalifu ule.

Lakini kwa vile hakumshauri, ndiyo kwa maana *United States* inaandamwa kila mahali kwa sababu ni kwamba, Muisrael pale ameshindwa kumshauri. Sasa wale hakuna njia ni kujilipua wamekata tamaa katika maisha yao. Isifikie hatua hiyo, msitufikishe hapo jamani Waislamu, msitufikishe kwamba tukate tamaa na maisha, tunataka sisi tuwe raia wema, watu wa kuchangia maendeleo katika nchi mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJI AHAMADI H. MPEME:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, inayoitwa Azimio la Kuridhia Mkataba wa Udhibiti wa Magaidi. Pia niwashukuru na kuwapongeza watoa hoja kwa hoja nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumza machache kwa sababu aliyenitangulia, Mheshimiwa Profesa Mndengereko, amezungumza mengi ambayo ningetaka niyachangie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ugaidi ni tatizo ambalo linasambaratisha uchumi wa dunia lakini pia linatia mashaka ya maisha ya binadamu duniani. Suala la kujiuliza hasa ugaidi ni nini. Mwenyekiti alipokuwa anatoa hoja pale nilimshukuru aliposema neno ugaidi halijatafsirika vizuri.

Neno ugaidi litafsirike kwa makini, ili basi tunapotunga sheria ile sheria imlenge gaidi. Sasa hatuelewi gaidi ni yupi hasa. Kwa sababu kuna mwingine anaua tena watu wengi haitwi gaidi. Lakini kuna mwingine anatenda kitendo labda cha kuashiria kuua watu wachache huyu anaitwa gaidi. Sasa gaidi ni yupi?

Gaidi ni yule aliyeua watu wengi, aliyeua kutumia njia za kisiasa, gaidi ni jambazi, gaidi ni nani haieleweki. Sasa tunapojadili kujua yupi ni gaidi ili tuweze kujadili vizuri inakuwa ni matatizo. Sasa ili sheria iweze kubeba mkondo wake vizuri, neno gaidi basi litafutiwe tafsiri iliyokuwa imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia lazima tuangalie chanzo cha ugaidi duniani hasa ni kitu gani. Nini chanzo cha ugaidi katika ulimwengu huu. Chanzo cha ugaidi katika dunia ni kwa sababu ya hitilafu ya kwamba, kuna nchi zingine zinatakiwa ziitwe mabwana, nchi zilizokuwa wababe. Ni ubabe.

Kuna nchi zinazokuwa babe zinataka zionekane sana mbele kuliko nchi zingine zozote zile. Sasa kwa maana hiyo zile nchi ambazo ni changa, ambazo zinapiga hatua za maendeleo, hizi nchi babe hazitaki zile zionekane zinaendelea. Zinatafuta kila namna ya kuzidhibiti ili zisipige hatua za maendeleo.

Sasa chanzo cha ugaidi kimeanzia hao kwamba, zile nchi zinazoendelea hazikubali na hizi zilizoendelea wanafanya mambo ya kudhalilisha zile nchi ambazo zinatakiwa ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi kamili ni pale Marekani ilipoombwa kwamba, isiivamie Iraq kwa sababu haikuwa na misingi ya kuivamia Iraq. Wakakiuka Azimio Namba 1441 la *United Nations,* Azimio ambalo lilikuwa ni la kukagua silaha zile zilizodhaniwa kwamba, Iraq ina silaha za maangamizi.

Lakini kwa sababu Mmarekani ni mbabe akajua kwamb,a Iraq hakuna silaha akabadilisha akasema anaiomba *UN* sasa impe ruhusa aivamie Iraq kabla hata taarifa ya ukaguzi wa silaha kali haijapatikana.

Lakini pamoja na *UN* kumwomba kwamba, asiivamie Iraq mpaka taarifa ipatikane, hakukubali. Sasa huo tunasema ni ubabe na ubabe wa namna ile ndiyo chanzo cha ugaidi duniani. *(Makofi)*

Lakini tatizo linalopatikana hakuna hata nchi moja katika ulimwengu ambayo inamshutumu Muamerika kwa kitendo kile, kitendo cha mauaji ya watu wasio na hatia, wamepoteza roho, watoto wadogo wamefariki na nchi imesambaratika.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunafikiri kwamba, vifaa si fedha, vifaa ni fedha, ni lazima na vyenyewe vifanyiwe udhibiti wa karibu. Ni lazima vile vile ajira zichunguzwe ili kuweza kupata wafanyakazi waaminifu. Kwa namna hiyo majopo yanayofanya *interviews* ni lazima yawe na watu ambao ni madhubuti, ambao wanaweza wakaajiri watu ambao ni waaminifu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Balozi za nje zifuatiliwe kwa karibu. Nashukuru juzi hapa Mheshimiwa Waziri alisema sasa utaratibu wa kuwapeleka Wahasibu utaanzishwa upya, ninaomba hili lifanyike ili kuweza kuokoa fedha za Taifa. Vile vile wakati wa manunuzi hasa Kitengo hiki cha Chakula cha Dharura, kwa kweli upotevu huu wa shilingi bilioni 12 unaonyesha kwamba, manunuzi hayafanywi kwa makini. Manunuzi ni lazima yafanywe kwa makini, bei zichunguzwe, *risk factors* lazima zizingatiwe na kadhalika. Vile vile lazima kuwe na *on the job training.* Kila saa ni lazima wafanyakazi waweze kuwekwa pamoja na kupewa mbinu mpya na kupewa *the do's and don'ts.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaomba kuunga hoja mkono na ninampongeza Waziri, kwa namna ambavyo kwa kweli anafanya ufuatiliaji wa Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi angalau nizungumze kwa muda usiozidi dakika 10. Lakini nataka pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Makatibu Wakuu wote na *Accountant General,* pamoja na *Controler and Auditor General,* kwa kazi nzuri waliyotufanyia kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kwa kuanzia hapo sasa tunasema nchi itakwenda. Haya yote ya nyuma nadhani tuyasahau tuanze sasa na sura mpya. Mheshimiwa Mramba, tutakupa kila aina ya msaada ufanye kazi yako vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na machache ya kuzungumza kwa nini tumefikia hapo. Sisi ambao tumekaa ndani ya Bunge kwa kipindi kirefu, hii hata Waziri alipokuja niliona kama kitu kipya kwa sababu najua sheria za zamani kuanzia *notice* za *Government* za tangu mwaka 1961, 1970 zote zilikuwa zinaelezea Waziri ndiye atakuwa na madaraka peke yake ya kufuta upotevu wowote ule. Lakini pia ilimpa madaraka zaidi Waziri kukasimu madaraka kwa watu wengine. Sasa hii tabia ya uliyokuja nayo Mheshimiwa Waziri, ya kuanza sasa tuwe tunapitia kwenye vyombo vya Bunge ambavyo ndio vyombo halali vya wananchi, mimi nadhani itatujengea heshima kwa Watanzania na Watanzania waone kwamba, hakuna kitu chochote tunakificha ndani ya nchi hii. Tunakiweka wazi kama kuna matatizo tutakaa tuyazungumze wote kwa pamoja. Mimi nakushukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Sasa mimi nilikuwa na ushauri wa aina mbili. Kada ya *Auditors* bado nadhani ni tofauti na *Auditors* wa zamani. *Auditor* wa zamani ilikuwa ukisikia *Auditor* anakuja lazima ujiandae. Siku hizi *Auditor* anapokuja kwanza unamwandalia hata pa kulala. Anakuja kukukagua wewe hata unamwandalia wapi atalala, chakula atakula wapi na jioni mnywe pombe wote pamoja. Kada hiyo nadhani tuiangalie upya tena kwa jicho maalum. Tuipe uzito, tuipe kila aina ya msaada wafanye kazi yao vizuri, wasidanganywe na fedha ndogo ndogo wanazopewa ndiyo wanatufikisha hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano, katika Halmashauri yangu ya Mji wa Sumbawanga. Mfano hai, mwaka 1999 na namwomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu anisikie. Mji wa Sumbawanga ulipoteza shilingi 59,480,303 na zilipotea kutokana na watumishi watatu. Wa kwanza alikuwa Mhasibu, wa pili Mchumi na wa tatu alikuwa wale ambao walikuwa wanaitwa ndio Maafisa Mipango. Walipoteza fedha hizi kwa njia mbili, kwanza ni kughushi, pili kuiba. Nadhani baadhi ya mali kama nondo, mabati, saruji, mbao walikuwa wanaiba. Lakini kipindi chote hicho hakuna aliyekuja kugundua mpaka baada ya miaka miwili kwa sababu *Auditors* walikuwa hawafanyi kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Kesi hiyo imechukua miaka minne inachunguzwa na kwa bahati mbaya Mkurugenzi amefariki, ambaye ndiye aliyehusika wamebakia watatu. Hivi kweli kipindi cha miaka minne unafanya uchunguzi mpaka sasa, hivi tunataka tusikie fedha hizi tuje tuzilete Bungeni zifutwe? Mimi nitaomba shauri hili, Serikali ilivalie njuga. Kesi yake ni namba 247 ya mwaka 1999 na tunajua upotevu wa vifaa hivi umekwishawasilishwa kwa wote wanaohusika, lakini hatua haijachukuliwa mpaka sasa. Leo hii wanaendelea kulipwa nusu mshahara miaka minne fedha za wananchi. Hivi tatizo liko wapi? Fedha za wananchi zimepotea na tusipoangalia watarudishwa kazini. Hakuna kitu ambacho Watanzania wanashindwa kutuelewa, wanamwona mtu anaiba na anaanza kujenga na majumba makubwa halafu baada ya muda wanamrudisha kazini na anapita akijigamba ya kwamba mtanifanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kesi nyingi zinazochelewa ni zile kesi ambazo zina fedha nyingi ili wagawane watu. Kesi ya Fedha za shilingi milioni 2 au milioni 3 inakwisha haraka sana na mtu anafungwa haraka. Lakini kukiwa na mamilioni itachukua hata miaka minne wagawane kidogo. Sasa ni vizuri tukaliangalia kwa sababu unaweza kuja kutuchafua baadaye tukaonekana na sisi Wabunge hatusaidii kukemea matatizo yanayojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nini tufanye? Kwanza, nashauri *Auditors* waendelee na utaratibu wa *surprise checks.* Mwaka 1967 kwa taarifa yako Mheshimiwa Spika, kulikuwa na Mwalimu mwenzangu anaitwa Sanga, ameshafariki. Tuliporudi kutoka Marekani kwenye kozi aliambiwa *Auditors* wako ofisini kwake wanaangalia alikuwa anasimamia maziwa ya pale shuleni. Aliposikia tu hiyo siku ya pili alikwenda kujitundika akajinyonga. Kwa sababu *Auditors* walikuwa hawana utani wakikushika una kosa pale wanakuadhibu. Wa pili, mwaka 1976 Mwalimu mwenzangu tulikuwa tunafundisha naye Ukiriguru alifanya *forgery*. Alikwenda Uganda akapata *imprest* alipokuwa ana-*retire imprest* kwa kila mahali palipo na sifuri alikuwa anaongeza sifuri ili apate fedha zaidi. *Auditors* wakamshika akafungwa miaka 7 kwa kosa la kuongeza sifuri kwa mfano shilingi 40/= ikawa shilingi 400/= akafungwa miaka 7. *Auditors* wa zamani hawakuwa na utani kwa fedha za umma. Ni vizuri *Auditors* watusaidie kubadilisha mazingira haya tuliyonayo, wasimamie kila senti ya wananchi itumike kwa kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mimi napenda kuwashukuru wote waliohusika. Namshukuru Mwenyekiti wetu, amewasilisha vizuri sana taarifa hiyo. Lakini nataka kumshukuru pia Mheshimiwa Dr. Slaa, wa Kambi ya Upinzani, wameliona hilo. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tumeyachunguza yote na bahati nzuri wahusika walileta hata mafaili yote tukaridhika kwamba, kwa haya kwa niaba ya Wabunge tutakubali. Haya mengine tusubiri yatakuja baadaye. Sasa hatua tuliyofikia nadhani naomba Wabunge kwa kweli tuunge mkono hoja na Azimio la Mheshimiwa Waziri ya kwamba, huu ni mwanzo mzuri tuendelee na tuna imani baada ya muda hatutakuja kuanza kushughulikia mabilioni ya fedha. Tutashughulikia fedha ndogo ndogo ambazo labda mtu amepotea au amekufa hiyo nadhani tutaipitisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Spika, kwa hakika nimesimama ili kuunga mkono hoja hii iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri hapa. Lakini kwanza, nikushukuru kwa kunipa ruhusa siku ya Ijumaa nikaenda Rufiji nikashuhudia ufunguzi wa daraja lile la Mkapa. *(Makofi)*

Imepigwa hatua kubwa pale tumetoka kwenye historia ngumu sana kufika hatua ile kila mtu anashangilia na mimi nilikuwa mmoja katika wale tuliopewa ruhusa ya kwenda kushangilia. Chama cha Mapinduzi na Serikali yake, awamu zote tatu, wamefanya kazi hii. Ingelikuwa kama sio ndani ya Bunge ningesema CCM Juu! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimesema nasimama kuunga mkono hoja hii lakini labda niseme moja au mawili tu. Kuna busara kubwa sana kwenye suala zima hili la kuwasilisha hii hoja ya kufuta hizi hasara na potevu. Kimsingi ukiangalia hesabu hizi ukiziona na *figures* zilizoko ndani humu ni kubwa. Kama ukisema kwamba, kuna deni hapa Serikali inadai basi una kila sababu ya kujenga matumaini kwamba, Serikali ikifanya jitihada ya ziada hapa fedha hizi zikarudi basi zitasaidia sana kwenye jitihada yetu ya maendeleo. Sasa tunachozungumza hapa kwa kweli ni kwamba, hakuna fedha zenyewe hizi. Kwa sababu hizi fedha ziko kwenye makaratasi haya kwa muda mrefu. Kimahesabu hapa tunachozungumza nadhani hoja ya Mheshimwa Waziri ni kwamba, anataka kusafisha vitabu kimahesabu ndani ya Serikali. Sasa hii hoja ni ya msingi sana lazima tuiunge mkono na mimi naomba wenzangu tuiunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri hapa. Nimesikiliza hotuba iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ambayo imepitia hii hoja kwa kweli tuna kila sababu ya kuunga mkono hoja hii, tufute haya ili tupate kwa kuanzia. Tumefanya mengi katika jitihada yetu ya kuhakikisha kwamba, mambo yetu yanakwenda sawa. Tumetunga Sheria ile *Public Finance Act* ya mwaka 2001, msingi wake ni Utawala Bora. Utawala Bora ni pamoja na mambo yetu kukaa sawa kimahesabu vile vile. Tumetunga mpaka na Kanuni ya 43, ambayo inatumika leo kumfanya Waziri apate ruhusa hii ya kufanya hii kazi, dhamira yake ni hiyo hiyo. Tumeweka ule mfumo wa *Intergrated Financial Management System,* ili mfumo ule uweze kufanya kazi lazima upate pa kuanzia. Sasa hivi kuna uchafu mwingi ndani ya

mahesabu ya vitabu vya Serikali na hata hii mifumo tunayoizungumza itashindwa kufanya kazi. Waziri ameleta hapa, Kamati imepitia na mimi nataka nichukue nafasi kumshukuru sana Waziri huyu, Manaibu wake wawili na timu yao. Nataka nichukue nafasi kumshukuru sana huyu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na timu yake. Kwa pekee kabisa nataka kumshukuru na kumpongeza sana *Accountant General,* Mama Nyoni. Wale ambao hawaamini wakiwemo na wanawake wenyewe kwamba, majukumu makubwa haya yanafaa kupewa wanawake, basi wakaangalie kazi inayofanywa na Mama Nyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanatafuta kazi, lakini kuna kazi zinatafuta watu na pale kwa Mama Nyoni kazi imepata mtu. Kwa kweli ameisaidia sana Kamati ile. Wamesaidia kuainishia yale madai ambayo hayawezekani kabisa kulipika, yale maduhuli ambayo hayawezi kukusanyika kabisa na Kamati hii imezingatia yale yote. Nilichofurahi zaidi na kufarijika ni kwamba, sio kila lililopelekwa kwenye Kamati ile basi limepitishwa kwa maana ya kuja kutoa idhini hapa kwamba Mheshimiwa Waziri akayafute, hapana. Ukitazama utakuta kwamba, ilikuja karibu shilingi bilioni 216, lakini Kamati ikisaidiwa sana na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, imesema katika hizi shilingi bilioni 216 hizi shilingi bilioni 143 rudini nazo mkafanyie kazi, tutaruhusu hizi shilingi 72 bilioni kwenda kuomba wenzetu watuunge mkono ili zifutwe tumpe idhini hii Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nadhani ni la msingi na sote nadhani makofi haya naona kwamba tunaungana pamoja na tutampa idhini yeye Mheshimiwa Waziri. Lakini lazima niseme moja, ili tuweze kufanikiwa kwa hapa tunaposema tunataka tuanze na *Clean Certificates* ziweze kufanikiwa ni lazima tutambue kwamba, kuna matatizo mengi yaliyotufikisha hapa, ni upungufu katika usimamizi na ufuatiliaji kwenye Serikali. Kuna upungufu mkubwa. Ili tuweze kufanikiwa tunatakiwa sasa hali ibadilike sana vinginevyo hatutaweza kutoka hapa tutarudi tena na maombi ya namna hii tena baadaye na halafu itazaa hoja kubwa miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachosema ni kwamba, ukitazama hili jedwali ambalo tumepewa kuna kitu kimoja naomba nikiseme kwa kifupi sana, kila kesi iliyoletwa hapa imetolewa sababu kwa nini inaombewa kufutwa sasa. Nyingi zimekuwa wizi, upotevu, uzembe na vitu vingine. Lakini nimeangalia mimi hapa kila wizi uliotokea katika kile kipengele kinachohusu Polisi kifungu cha 28, kila wizi uliotokea pale basi faili limepotea na hakuna kilichofanikiwa hata kimoja. Lakini kila wizi uliotokea kwenye Idara ya Mahakama, utasikia mtu ameshafungwa. Tofauti iko kubwa sana hapa. Sasa kama kweli Polisi wangelikuwa wanafanya kama ilivyofanyika kwa upande wa Mahakama, tulikuwa na kila sababu ya kuamini kwamba, hivi mwendo tunaokwenda nao huu ndio utakaotusaidia. Inanitia wasi wasi sana hawa Polisi. Maana yake inaonekana Polisi anaiba fedha halafu anapotea wanasema tumemtafuta kwao Wanging’ombe haonekani. Wewe unajua kwake ni Wanging’ombe unasema kuwa haonekani na unakwenda kufunga faili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika na hizo fedha ni fedha nyingi za Serikali. Sasa mimi nasema kama inawezekana kufanyika kama inavyofanyika kwa upande wa Mahakama, kama ilivyojionyesha kwenye jedwali hili, Polisi kama hamuwezi basi nitangulie kwa kusema mjirekebishe tutakuja kuchukuana na upepo sana hapa.

Mheshimiwa Spika, nimezingatia sana ushauri wako wa kusema kwamba, kwa sababu muda wako umekuwa mchache, naona afadhali nisiendelee kusema nimalizie hapa kwa kuunga mkono hoja hii na kuwaomba wenzetu Wabunge wote walioko hapa ndani, tuungane pamoja kuunga hoja hii, tumpe idhini hii Mheshimiwa Waziri madeni haya yafutwe. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono hoja, lakini upotevu na hasara kubwa ya mabilioni ya fedha unaonyesha kwamba, bado kuna udhaifu mkubwa katika utaratibu na mfumo wa udhibiti wa mali na fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, sina uhakika kama Serikali ilifanya tathmini kufahamu udhaifu huu unatokana na nini. Je, ni ukosefu wa wataalamu wa fedha na wa Bohari katika Idara mbalimbali za Serikali; je, ni wataalamu kukosa uwezo wa kuzuia upotevu; je, ukiukwaji wa makusudi wa taratibu za fedha za Bohari; je, ni udhaifu wa usimamizi wa Idara za Serikali; je, ni utaratibu wa kulindana na adhabu ndogo?

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba, pamoja na kwamba tutakubali kufuta, basi Serikali ikae chini ifanye tathmini ili ipate jawabu la kudumu angalau la kupunguza upotevu wa fedha na mali za Serikali. Hii itatusaidia vile vile kuona kama taratibu mpya zilizoanzishwa na Serikali hivi sasa na sheria hizi tulizopitisha hivi sasa, je, zimesaidia kwa kiasi gani kuzuia upotevu au kupunguza upotevu. Mimi natoa hoja kwamba, kuna haja ya kuona kwamba sasa upotevu hauongezeki ila unapungua. Katika nchi maskini kama yetu, kama wengine walivyosema, kufuta mabilioni ya fedha ni jambo ambalo lazima liwekewe mkakati litokomezwe. Kama mkakati huo utahusu kurekebisha sheria, basi Serikali ilete sheria hizo Bungeni ili tuzirekebishe.

Kama ni suala la utaalamu wa hesabu na bohari, basi Serikali irekebishe na ipange upya wataalamu wa hesabu na bohari. Kila inapowezekana basi kuwa na mafunzo. Lakini kama inahusu kuweka vyombo vya kisasa na mifumo inayotumia teknolojia ya kisasa kutambua wizi kabla haujatokea, basi Serikali itafute vifaa hivyo na itumie mifumo hiyo. Ikiwa ni pamoja na kufanya kitu wanachokiita *(Tests),* majaribio ya mara kwa mara ya kupima uaminifu na uadilifu wa wafanyakazi katika maeneo nyeti, maeneo muhimu katika Idara mbalimbali za Serikali. Siku hizi wenzetu wana utaratibu huo wa kuwapima mara kwa mara uaminifu na uadilifu wa wafanyakazi wao katika sehemu zile muhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi kama nilivyosema, sina pingamizi lolote la Azimio hili, ninaliunga mkono mia kwa mia. Naiomba Serikali iimarishe zaidi udhibiti wa fedha za Serikali na mali yake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi na waliochangia kwa kuzungumza. Niseme tu kwamba, nakubaliana na wote waliozungumza au kuandika. Yale yote waliyosema ni kweli na yale yote waliyoshauri ni kweli. *(Makofi)*

Jambo ambalo limetufanya tukaja hapa ni sheria mpya ambayo kazi yake kubwa imekuwa ni kuleta uwazi katika kuzungumzia wizi ulioko katika jamii kuhusiana na mali na fedha za Serikali. Tumeweka uwazi na Waheshimiwa Wanakamati wa *PAC,* wamejionea wenyewe na ni kweli kwamba, bado tuna mlundikano wa kesi kama hizi tulizoleta hapa kushughulikia. Lakini ni kweli kabisa kwamba, baada ya sheria hii ya ununuzi wa mali za Serikali na uwekaji wa fedha za Serikali, baada ya sheria hizi mbili, tunaona mabadiliko katika picha hii ambayo tunaizungumza hapa sasa hivi. Hii ni picha ya miaka ya 1980, 1990 mpaka mwaka 2002. Sisi tunaona mabadiliko. Lakini vile vile tunaona hali ambayo hairidhishi sana, ya kwanza kama vile kulikuwepo Wakaguzi wa zamani wakali. Lakini vile vile mimi naona kama kuna mmomonyoko wa maadili miongoni mwa watumishi. Kuna mmomonyoko usiolingana na ule wa zamani. Maana zamani Wakaguzi wakali na waweka hesabu wakali. Sasa hivi sisi tunaona kwa ujumla wake kuna mmomonyoko wa maadili. Ya pili matokeo ya kutumia teknolojia nayo yanasaidia watu kufanya mambo ya kijanja, ingawa na teknolojia tunayotumia sisi pia inawadhibiti sana, kama nilivyoeleza wiki hii wakati wa hotuba ile ya Sheria ya Fedha.

Tuna mtandao na tunafundisha watu wengi. Kama nilivyosema, mwaka huu wa fedha tunakusudia kufundisha Wahasibu wapya 650. Walio mafunzoni sasa hivi wengine 630 wa ngazi zote shahada ya juu mpaka *CPA (Professional)* wote hawa. Lakini liko tatizo kama ambavyo tumekuwa tukisema hapa muda mrefu la namna ya kuwalipa Wahasibu hawa ili waweze kubaki kazini. Jambo hili kama nilivyokuwa nimeiahidi Kamati ya Fedha, lazima niendelee kulivalia njuga na natumaini kwamba, wenzangu katika Baraza la Mawaziri, watanielewa ninapokwenda kule kuomba *Privilege* kwamba, haiwezekani tukawa Waingereza wanasema wewe unakuwa *"penny wise and pound foolish".* Unang'ang'ania tu vitu ambavyo vitakupa faida ya senti, lakini unaacha hasara ya 20 ikiendelea kutiririka, haifai. Kwa hiyo, jambo hili tunalo, natumani tutalipatia jibu.

Kinachotisha sasa hivi na ni vizuri nianze kulisema hapa ni jambo jipya kabisa la wizi wa mitandao. Katika Serikali sasa hivi kuna wizi wa mitandao. Watu wanashirikiana kwenye Ofisi fulani na walio kwenye Ofisi nyingine na pengine walio nje kabisa utatu haramu, sio utatu mtakatifu, utatu haramu

wa kuiibia Serikali upo. Ndiyo jambo jipya tunaliona na tunapambana nalo. Uzuri ni kwamba, tunagundua kutokana na mtandao tulionao.

Sisi Hazina sasa ndio tunasema tunaona taa nyekundu pale, nenda pale. Au tunatangulia sisi wenyewe leo tunapeleka wale wakali baadaye. Kwa hiyo, hii ndiyo baraka iliyoko kwamba, pamoja na mmomonyoko huu ulioko wa maadili, hali hii itakuwa tofauti.

Pili, ukiona kwenye Wizara ya Fedha, nyingi ya fedha zilizokuwa zimepotea wakati ule zilikuwa kabla ya Mamlaka ya Mapato kuundwa zilikuwa ni za kodi. Lakini baada ya Mamlaka kuundwa na wenyewe wakawa na mitandao na utaratibu wao mzuri wa kuhifadhi hesabu, kwa kweli wizi uliokuwepo kwenye maeneo hayo ya kodi na Mamlaka ya Kodi umekiuka sana na karibu umekwisha. Ila sasa kinachotawala ni *corruption,* kama mlivyokuwa mnasema hapa.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, toka niombe mnipe habari nimekwishapata habari 6 ambazo nazishughulikia kutoka hapa hapa ndani, habari 6 za watu wabaya. Habari nyingine mbili za wezi tu na watu wanaokwepa kodi. Nafikiri leo kazi za kuwashughulikia hao zinaanza. Nyingine zilianza jana na nyingine zinaendelea leo. Nawaomba huko mliko mnyamaze, mkisikia mambo yanafanyika msimtafute Waziri, ooh kuna ndugu yangu, kuna mtu mmoja gari limekamatwa. Gari limekamatwa likichukua sukari ya magendo anakuja kwa Waziri, ooh naomba unisamehe, mimi ni mtu maskini, kule kwetu ndiyo hivi nimemalizika. Nataka nitoe taarifa kwamba, Waziri hatashughulikia jambo lolote linalohusu mkwepa kodi au mwizi au mtu *corrupt,* wala msiniletee. *(Makofi)*

Kama ana hoja aende kwenye Baraza la Kodi au kuna Kamati ile ya Kodi *(Tax Board and Tax Appeals Board),* aende kule akajitetee. Kwa hiyo, kuanzia sasa tutakuwa *very strict* katika kufuatilia hawa watu ambao wanakula hongo wanashirikiana na watu wengine kuhujumu Shirika, Serikali na wale wanaoshirikiana nao tukiwakamata kwa mujibu wa sheria hakuna cha msalie mtume. Hili jambo naweza nikalisema hapa kabisa na wajue hawa kwamba, nawapa taarifa. Mimi nitakuwa natoa taarifa kila tunapokamata watu kutokana na habari. Kama ni mtumishi mbaya tukimkamata tukimpeleka kwenye sheria au tukimfukuza tutatangaza kwamba tumekamata hawa na hawa. Watu pia tutakaowakamata huko mtaani kwa habari tulizopewa, kila tukipewa habari tutatangaza. Vita vimeanza, natoa taarifa msije kwangu nendeni kwenye vyombo vya sheria mkajitetee huko. Hii kazi lazima tuifanye. *(Makofi)*

La pili ambalo nataka kusema ni kwamba, kweli kama ingelikuwa ni katika hali nyingine sio ndani ya Bunge la Mheshimiwa Spika, ana macho makali, sisi hapa ungekuta ningelikuwa nimeomba tusali na tulie kama walokole. Tulie kwa sababu ni fedha nyingi hapa. Sisi tunakuja kuzungumza habari za shilingi 72 bilioni zilizopotea. Tungelia machozi hata Waziri wa Fedha, akisoma ile hotuba ungekuta amemalizia kwa kulia na kujipangusa. Kwa bahati nzuri sina machozi mengi, lakini ilitakiwa iwe hivyo kuonyesha tumesikitika. Ni fedha nyingi daraja la Rufiji linalosifiwa hapa ni shilingi bilioni 34. Leo tunafuta shilingi bilioni 72 na bado kuna nyingine tutakazokuja kufuta ni mbaya mbaya. Ni mbaya kabisa na kama kuna watu wa kuchomwa wale tunaosema watachomwa mbele ya safari, nafikiri hawa watu wote waliohusika huko mbele ni kubaya sana watachomwa tu. Kwa nini Bwana Mungu, asisikie kilio chetu cha kuwaibia maskini shilingi bilioni 72, umeibia maskini. *(Makofi/Kicheko)*

Mwisho, niseme kwamba, tufarijiane. Ukweli hii sio hasara tupu. Kuna watu ambao, kuna baraka zinatokana na fedha hizi tunazofuta. Kwa mfano, kama fedha za *SGR* zimekuwa mbaya. Lakini kuna watu waliopona njaa, angalau hilo tujifariji. Mtaona huku kwenye vitabu hivi kuna fedha zinazohusiana na Aga Khan. Ilikuwa wakati ule akijenga hoteli za kule Serena Arusha, kwenye maeneo ya utalii kule. *Withholding tax* ya yule mjenzi haikulipwa.

Mheshimiwa Spika, lakini zilikuwepo sababu. Lakini angalau hoteli zimekuwepo na zinasaidia utalii leo. Kwa hiyo, sio hasara kwa nchi, tunazo zile *assets* na watalii wanaingia huko. Nasema tusikitike lakini tujifariji kwamba, *it was not a total loss,* kwa namna fulani tumefaidika.

Mheshimiwa Spika, ningependa nimalizie tu kwa kusema kwamba, ninashukuru Waheshimiwa Wabunge mmetuelewa katika Wizara ya Fedha. Kama alivyosema Mheshimiwa Lutavi, tunataka kufagia vitabu vya hesabu ili hesabu za Serikali zisomeke vizuri zaidi kwani kila mwaka zinatoka zile zile na matatizo ni yale yale. Tukifagia na kuziondoa, vitabu vya Serikali ya Tanzania vitaanza kusomeka vizuri zaidi, lakini mapambano yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha Kufuta au Kusamehe Madai liliridhiwa na Bunge)*

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge

**MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kazi kubwa na nzuri anayowafanyia Watanzania. Ufunguzi wa daraja la Mto Rufiji, ambalo limepewa jina lake, ni ushahidi tosha wa kazi yake nzuri ambayo anaendelea kuifanya. Daraja hili ni ukombozi kwa Watanzania wote na hasa kwa sisi Wananchi wa Kusini imetupa faraja kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, ambao hivi karibuni wamechaguliwa katika chaguzi mbalimbali na pia Waheshimiwa Wabunge, ambao wamefanikiwa kurudi tena Bungeni kutokana na maamuzi ya Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wenzetu, Mheshimiwa John Samwel Malecela na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwa kufunga ndoa. Ninawatakia maisha yenye upendo na furaha tele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwape pole nyingi Mheshimiwa George Kahama na Mheshimiwa Janet Kahama, kwa msiba mkubwa uliowapata wa kufiwa na mtoto wao mpendwa. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kanuni za Bunge inaundwa chini ya Kanuni ya 67 ya Kanuni za Bunge. Majukumu yake yameainishwa katika fasili ya pili ya Kanuni hiyo ya 97 kama ifuatavyo: -

(i) Kufikiria na kutoa mapendekezo juu ya kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge;

(ii) Kuchunguza na kutoa tafsiri juu ya pendekezo lolote linalohusu Kanuni ya Bunge ambalo limepelekwa kwa Kamati hiyo na Spika au Mbunge yeyote; na

(iii) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya lalamiko lolote kuhusu uamuzi wa Spika ambalo limepelekwa kwake na Mbunge yeyote.

Mheshimiwa Spika, kufuatia majukumu hayo, Kamati ya Kanuni za Bunge ilikutana hapa Dodoma tarehe 5 Agosti, 2003 kupitia mapendekezo na kufanya marekebisho katika Kanuni kadhaa za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha marekebisho hayo, naomba kwanza, niwatambulishe Wajumbe wa Kamati hii ambao ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Pius Msekwa, ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Mheshimiwa Frank G. Magoba, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Philip S. Marmo, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Prof. Henry R. Mgombelo, Mheshimiwa George F. Mlawa, Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Sophia M. Simba, Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa na mimi Mheshimiwa

Juma J. Akukweti, pia ni Mjumbe na ni Makamu Mwenyekiti. Katibu wa Kamati hii ni Ndugu Nenelwa Mwihambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wa Kwanza wa Bajeti tangu Bunge lifanye mabadiliko ya Kanuni hususan namna ya kushughulikia na kupitisha Bajeti ya Serikali. Katika kipindi hicho tumepata uzoefu wa aina mbalimbali. Jambo lililojitokeza waziwazi ni muda mchache wa kupitisha makadirio hayo katika Kamati ya Matumizi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, Kamati inapendekeza marekebisho katika Kanuni ya 21(4) ambayo inazungumzia hoja ya kuongeza muda kwamba, yaweza kutolewa ili kutoa nafasi kwa majadiliano kuendelea. Muda unaopendekezwa kuongezwa ni dakika zisizozidi 30 baada ya muda wa kawaida wa kuahirisha vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha Wabunge waweze kufuatilia kwa makini majadiliano yanayoendelea na kuepusha uwezekano wa vipaza sauti kuingiliana na mionzi inayotoka katika simu za mkononi, Kamati yangu inapendekeza Kanuni ya 53(e) ifanyiwe marekebisho ili Wabunge wazime simu zao kabla ya kuingia katika Ukumbi wa Bunge. Tutakumbuka Kanuni ya sasa inapiga marufuku kuingia na simu Bungeni. Kwa hiyo, inafanyiwa marekebisho, ukiingia nayo uizime. *(Makofi)*

Kamati pia inapendekeza Kanuni ya 87(5) ifanyiwe marekebisho ili Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge wawe na uwezo wa kuchagua Makamu Mwenyekiti ili kufanikisha shughuli za Kamati hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulingana na taratibu zetu, Kamati za Kudumu za Bunge zinawasilisha Bungeni taarifa za shughuli zilizofanyika kila ifikapo mwisho wa mwaka. Hata hivyo, kabla ya muda wa kuwasilisha taarifa Bungeni kuwadia, Kamati katika kutekeleza shughuli zake, imebaini mambo fulani ambayo inayaona ni muhimu yafanyiwe kazi na Wizara husika. Hivyo, Kamati yangu inapendekeza Kanuni ya 88(11) ifanyiwe marekebisho ili Kamati ziweze kutoa taarifa ya ushauri kwa maeneo ambayo yanahitaji kushughulikiwa kwa haraka kabla ya kutoa taarifa kamili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inapendekeza marekebisho katika nyongeza ya 11 ya Kanuni za Bunge kuhusu taratibu za uteuzi na uchaguzi katika chaguzi mbalimbali Bungeni, kwa kuweka vipengele kwa ajili ya chaguzi zinazohusu makundi ya Wabunge Wanawake au Wabunge wa Kambi ya Upinzani, kama inavyoonekana katika mapendekezo ambayo yamegawiwa.

Hayo ndiyo mapendekezo ya marekebisho yaliyotolewa na Kamati yangu. Naamini kuwa marekebisho haya yataboresha utendaji kazi wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Bunge kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe, ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati hii, kwa uongozi mahiri katika Kamati na Wajumbe wote wa Kamati ya Kanuni za Bunge hasa kwa ushirikiano na umakini mkubwa walioonyesha wakati wa kufikia mapendekezo haya.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wao, kwa kunipa ushirikiano mkubwa wakati wote uliponipa nafasi ya kuongoza Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ni matarajio yangu kuwa, Waheshimiwa Wabunge, wataipokea kwa dhati na kuikubali hoja hii iliyopo mbele yetu ili tuweze kuboresha Kanuni za Bunge na kuimarisha uendeshaji bora wa shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nisome Azimio lenyewe:-

KWA KUWA kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2), moja ya majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge ni kufikiria na kutoa mapendekezo juu ya kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge;

NA KWA KUWA Kamati ya Kanuni za Bunge ilikutana Dodoma tarehe 5 Agosti, 2003 kufikiria mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni kama ilivyoonekena kwenye kiambatanisho cha kwanza kwa kauli moja kupitisha mapendekezo ya marekebisho hayo;

KWA HIYO BASI kwa mujibu wa Kanuni ya 121(1) ya Kanuni za Bunge toleo la 2003, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linalokutana katika Mkutano wake wa 12, linayapokea na kuyakubali mapendekezo ya marekebisho katika Kanuni za Bunge Toleo la 2003 kama ilivyoonekana katika kiambatanisho cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, hoja zinazoletwa na Kamati hazina msemaji yeyote wa Upinzani wala wa Serikali, tunaingia kwenye mjadala moja kwa moja. Ninao wasemaji wanne, ombi langu ni lile lile kwamba, waseme kwa ufupi ili wote wapate nafasi.

Kabla hatujaanza mkutano, nilipata michango ya maandishi ikisema kwamba, ile namba 7 katika ukurasa wa pili wa mapendekezo mliyonayo haieleweki, inaelekea kwamba, ni maneno yametundikwa tu, hayakukamilika. Lakini napenda nimsaidie mtoa hoja kueleza kwamba, haya hayaning’inii tu peke yake, haya ni maneno yanawekwa katikati ya maneno mengine yaliyopo kwenye Kanuni hiyo.

Kanuni ya 88(2) inasema hivi: “Mwenyekiti ataongoza vikao vyote vya Kamati. Endapo Mwenyekiti hayupo kwenye mkutano wowote, (sasa maneno yanaongezeka) Makamu Mwenyekiti ataongoza shughuli za mkutano huo. Endapo Mwenyekiti na Makamu wake wote hawapo, (sasa tunaendelea na Kanuni kama ilivyo) Wabunge waliohudhuria watachagua mmojawapo miongoni mwao kuongoza mkutano huo.”

Sasa, wa kwanza kuchangia atakuwa ni Mheshimiwa Mohammed Missanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii ya kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye mada hii ya Marekebisho ya Kanuni. Kwa sababu wamesema tuokoe wakati, niende moja kwa moja kwenye yale ambayo nakusudia kusema.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kutuongoza vizuri katika Bunge hili. Pia, nikushukuru kwa ubunifu mkubwa ulionao katika Bunge hili, ubunifu ambao umesababisha kuhuisha Kanuni zetu za Bunge, pamoja na Kamati yetu ya Kanuni. Kwa hiyo, ninakupongeza na kuipongeza sana Kamati yetu kwa kazi nzuri ambayo inatufanya tuwe karibu sana na Mabunge mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ninataka niliseme ni kwamba, katika kifungu cha 49(1) cha Kanuni za Bunge, kinatoa muda wa kusema Bungeni ...

**SPIKA:** Lakini hilo halimo kwenye mapendekezo, zungumzia mapendekezo yaliyowasilishwa.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kimsingi ninakubali mapendekezo, lakini nilitaka nitoe *suggestion* kwa Kamati kama inaweza kuboresha mapendekezo mengine.

**SPIKA:** Hapana, kuna njia ya kufanya hivyo, unaiandikia Kamati.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, kama ni hivyo kwa mwongozo huo basi nisitishe tu maelezo yangu, nitafuata utaratibu uliousema. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nikupongeze sana kwa kuliongoza Bunge letu vizuri sana ukiwa pamoja na timu yako ya Naibu Spika na Wenyeviti wetu wawili, ambao kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana katika kikao hiki cha Bajeti na vile vyote ambavyo vimepita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina mgogoro na mapendekezo yaliyopendekezwa katika kifungu cha 2, 3, 4, 6, 7, 8, 9 na 10. Lakini kidogo kutokana na utaratibu uliokuwepo hapa wa Kamati ya Matumizi wakati wa kujadili hoja ya Waziri wa Nishati na Madini, ninaona kipengele cha kwanza kuwa kinapendekeza kubana majadiliano katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge letu kuna vitu vingi sana vinabana maongezi na tutakapoongeza hiki hatutakuwa tunawatendea haki Wananchi wetu. Ningekuwa na nafasi ningeeleza vizuri ni vitu gani ambavyo mimi mwenyewe kama Mbunge, ninaona vinabana majadiliano na haviwapi Wananchi haki ya mjadala katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nipendekeze kwa Bunge lako Tukufu kwamba, likatae pendekezo 1(a) na kukiacha kifungu hicho kama kilivyo katika Kanuni za sasa. Ninapenda pia nipendekeze katika kipengele cha 5 kifanye marekebisho madogo, isomeke: "Hali kadhalika, wakati Bunge liko katika Kamati ya Matumizi, isipokuwa kama itatolewa hoja ya kuongeza muda wa kikao cha Kamati hiyo kwa mujibu wa Kanuni ya 21(4) ya Kanuni hizi, zikibaki dakika kumi tu kabla ya muda wa kuahirisha Bunge kwa siku hiyo na Kamati bado haijamaliza kufikiria mafungu yote yanayohusika na hakuna Mbunge aliyetoa hoja ya muda wa ziada kuongezwa...". Ningependekeza hiyo iongezwe hapo: "na hakuna Mbunge aliyetoa hoja ya muda wa ziada kuongezwa", Mwenyekiti atafunga mazungumzo yoyote yaliyoruhusiwa katika aya za (b) na (c) za Kanuni hii na papo hapo atawahoji kuhusu mafungu yaliyosalia kama yapo.

Mheshimiwa Spika, nadhani mapendekezo haya ya Bunge kuacha kifungu cha 1(a) kibaki kilivyo ni ya msingi kabisa ambayo yatalifanya Bunge kuwa na nafasi ya kuihoji Serikali katika mapendekezo yake ya Bajeti. Kama mabano haya yataongezwa katika mazungumzo ya Wabunge, Kanuni hizi zitakuwa zimewabana sana Wabunge na Kanuni hizi kwa kuwabana sana Wabunge hazifanyi Bunge hili kufanya kazi yake ya kuisimamia Serikali kwa dhati na pia kutoa mawazo ya Wananchi wanaowawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda nirudie kabla sijaketi ili suala hili liwe kwenye mawazo ya Wabunge kwamba, kwanza napendekeza kwamba, kifungu cha 1 Kanuni ya 21(4) sehemu (a) ibaki kama ilivyo katika Kanuni za sasa, isifanyiwe marekebisho yanayopendekezwa. Pili, kifungu cha 81(6) kinachopendekezwa sasa kikubaliwe tu baada ya kufanyiwa marekebisho ya mstari wa 7 kuongeza pale mafungu yote yanayohusika na hakuna Mbunge aliyetoa hoja ya muda wa ziada kuongezwa.

Mheshimiwa Spika, ninawashauri sana Waheshimiwa Wabunge, wakubali mapendekezo yangu. Baada ya mabadiliko haya, basi tukubali mapendekezo ambayo yameletwa na mtoa hoja. Kama tutakubali tu kubadilisha, tutakuwa tunalitendea Bunge isivyo haki na Wananchi wetu kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda tena nikupongeze sana kwa uwezo wako mkubwa wa kuongoza Bunge, lakini napenda nichukue haki hii ya kuweza kutoa mapendekezo ya mabadiliko hayo. Ahsante sana.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kukupongeza wewe mwenyewe, Naibu Spika, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Kanuni za Bunge, kwa kutuongoza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwa ufupi sana. Naungana moja kwa moja na mawazo ya Mheshimiwa Prof. Maghembe kwamba, tukubali kimsingi, lakini tufanyie marekebisho. Kanuni za Bunge kwa kweli ni Chombo kinachoongoza Shughuli za Bunge na ni Chombo kinachotoa kielelezo cha demokrasia shirikishi na ningependa niseme kabisa kwamba, ni vizuri haya mabadiliko tungekuwa tunapata

mapema zaidi kuliko ilivyokuwa leo. Ninaamini kabisa kama tungefanya hivyo tungekuwa na mchango mkubwa sana kutoka kwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu isije ikafika mahali tukawa tunajibana sisi wenyewe. Kifungu hiki cha marekebisho namba 5, yaani hiyo Kanuni ya 81 na 86 inaweza kutuadhiri vibaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii, lakini pamoja na mabadiliko ambayo Mheshimiwa Prof. Maghembe, amependekeza na ningeomba Wabunge hili tulione ili tuweze kupanua demokrasia yetu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, Kanuni siyo Msahafu wala Biblia au Koran, ambazo hazibadiliki. Kwa hiyo, utaratibu wa Kamati yako kuleta mabadiliko mara kwa mara ni sahihi kabisa, wala hatuna matatizo nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo linalokuja ni pale ambapo sisi wenyewe tunaingiza vitu ambavyo vinatufunga miguu, mikono na mdomo, mbele ya safari tutakuja kusema tumetunga sisi wenyewe Kanuni ambazo zinatuumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimejiandaa vizuri, lakini bahati mbaya muda hauko nasi. Napenda nisirudie maneno aliyosema Mheshimiwa Prof. Maghembe katika ile Kanuni ya 21.

Mheshimiwa Spika, pili, nina wasiwasi sana katika hii Kanuni ya 53 ambayo inasema: "Mbunge hataruhusiwa kutumia simu ya mkononi", ni sawa. Sasa hivi tuna teknolojia nzuri tu ya kutosha ambayo itaweza kuzimisha simu zote zisiweze kupiga kelele. Tatizo hapa ni kelele ambazo zingekuwa zinatokea mara kwa mara kwa ajili ya kutumia hizo simu. Tungeweka teknolojia na isingekuwa na haja ya kuweka kitu cha namna hii katika Kanuni zetu kwa sababu teknolojia ni kubwa na ambayo inaweza kuepusha vitu vya namna hii.

Mheshimiwa Spika, kusingekuwa na haja ya kusema kwamba, simu zizimwe au mtu asiingie na simu. Sasa hivi kuna watu wana simu na hazina mlio, anaweza akapata simu na akaiona kwamba ni ya dharura au vinginevyo, akatoka akaenda kusikiliza. Lakini vile vile, mtu anaweza akaweka *vibration* kwenye simu yake na ikaendelea kupokea *messages* na Bunge likaendelea. Sasa, ili kuepusha vyote hivi, hakuna haja ya kuweka Kanuni kama hii katika Bunge lako kubwa kama hili. Ni kuweka tu teknolojia ambayo inaweza ikanyamazisha na kutoingiliana na mawasiliano mengine.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu mwingine uko katika ule mstari wa nne, Kanuni ya 81(2)(a) hasa pale inaposema: "...pale ambapo Mwenyekiti ataona kuwa inafaa." Kwa kweli Mwenyekiti ni Mwenyekiti, lakini Mbunge na yeye ana nafasi ya kuhoji na kuisimamia Serikali hapa hapa Bungeni, hana sehemu nyingine yoyote ambapo angeona aishauri au aihoji Serikali. Sasa, unapompa nafasi kubwa Mwenyekiti aone inafaa, anaweza akaona inafaa mahali popote akatumia kifungu hicho kuburuza Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri neno hilo: "Ataona kuwa inafaa", liondolewe, iwekwe moja kwa moja kwamba: "Itakapofika wakati wa kujadili ifuate kama Kanuni inavyosema na Mwenyekiti asipewe nafasi ya kuona inafaa." Kwa sababu hawezi 'kuona inafaa' yeye peke yake, kuliko sisi ambao tuko wengi 'tunaona inafaa' tuendelee kuzungumza katika Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote tunayasema kwa sababu tunabanwa sana na wakati. Muda wote tumekuwa tukibanwa na wakati na nafasi ya kusema ni ndogo, lakini sisi wenyewe tunakuja tunarudia kwa sababu hatuna nafasi ya kutosha kuishauri na kuisimamia Serikali. Mara nyingine tunachangia kwa mchango wa maandishi, Waziri pale anakuwa hajakujibu, unapokuja kwenye Kamati ya Matumizi bado muda hautoshi na Mwenyekiti anasema inafaa Bunge liishe. Sasa, ni wapi ambapo Mbunge ataeleza dukuduku lake ambalo anaona linafaa katika kushauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri hii ya kwanza aliyoielezea Mheshimiwa Prof. Maghembe, isikubalike na ile ya 4 "... kama Mwenyekiti ataona kwamba inafaa" na yenyewe isikubalike.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja, ahsante.

**SPIKA:** Kutoa hoja! *(Kicheko)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Hoja ya kutokubalika. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya Mheshimiwa mtoa hoja kuja, labda nisaidie kidogo kufafanua hii habari ya kusema Kanuni zinawabana. Liko *book* hapa sijui Katibu umeliweka wapi, *Parliamentary Practice.* Hebu linyanyue tulione. Huu ndio mwongozo wa Shughuli za Mabunge yanayofuata taratibu zetu.

Waheshimiwa Wabunge, katika mwongozo huu kuna mambo mawili. Kwanza, muda wa kusema Mbunge umewekwa katika Mabunge karibu yote, ni dakika ngapi. Sisi tuna dakika 15, wengine wana dakika 10 na wengine wana dakika 5. Muda wa kusema unatawaliwa na Kanuni katika Mabunge yote, binafsi nimetembelea mengi na ninayajua.

Pili, muda wa kumaliza kikao cha Bunge unatawaliwa na Kanuni katika Mabunge yote. Bunge la Uingereza mwisho wao ilikuwa ni saa 4.00 usiku, isipokuwa itakapotolewa hoja ya kuendelea. Sasa, katika Bunge la Uingereza wameingia Wabunge Wanawake wengi wakalalamika kwamba, saa 4.00 sisi tuna kazi za kufanya nyumbani, waume zetu wanatusubiri, hapana kukaa hapa mpaka usiku wa namna hiyo. Kwa hiyo, wamerudi nyuma, sasa wanamaliza mapema zaidi. *(Kicheko)*

*Point* ninayotaka kusema ni kwamba, Kanuni zinazotawala muda wa kusema na muda wa kumaliza Bunge kwa siku hiyo imo katika Kanuni za Mabunge mengi sana. Si suala la kubana, ni suala la kufanya Bunge lifanye kazi tofauti na mikutano ya hadhara au mikutano ya Vyama vya Siasa, wao wanajiendea tu kienyeji. Bunge linakwenda kwa taratibu zilizowekwa na hizi mbili ni muhimu sana.

Hoja ya kuongeza muda imekuwepo katika Kanuni zetu miaka yote na siku zote hoja ilipotolewa ilikataliwa, Wabunge walisema: "Tumechoka tunataka kwenda" na ninayo mifano kwa nini inakataliwa. Tulipokuja kufanya utafiti kwa nini inakataliwa ni kwamba, inatolewa hoja *open handed,* Bunge liendelee mpaka tutakapomaliza, inaweza ikawa ni saa sita au saa nane usiku, basi ndio Kamati ya Kanuni ikasema tuweke kama vile Kanuni ya Kuahirisha Bunge inavyosema kwamba: "Kama kuna hoja ya kuahirisha Bunge na kuna mtu anataka kuchangia hoja, basi atafanya hivyo ndani ya dakika 30 zikiisha dakika 30 Spika anaahirisha moja kwa moja."

Waheshimiwa Wabunge, dakika 30 zimeshakubalika ndio maana tukaziweka hapa. Siku za nyuma ilikuwa ni kikwazo, mtu anatoa hoja ya kuongeza muda Bunge linakataa. Hii sasa inatoa nafuu kwamba, kwa kuwa ni nusu saa tu nadhani Bunge litakubali ili tumalize hoja iliyoko mbele yetu. Kwa hiyo, haya mapendekezo yana misingi hiyo, siyo kuwabana.

Pia, ninaomba niendelee kueleza kwamba, kazi ya watu 300 kusimamia Serikali haiwezekani. Ndio maana Mabunge yote sasa, angalau ya *Commonwealth* ninayoyafahamu yanahamia katika kuimarisha Kamati za Bunge ndio zifanye kazi hiyo.

Kamati ni za watu wachache wachache, Kanuni zake ni tofauti na Kanuni za Bunge zinaweza kufanya kazi nzuri zaidi, Maafisa wa Serikali wanaingia kwenye Kamati, lakini Bungeni hawaingii, anakuwa ni Waziri peke yake.

Mfano ni Marehemu Mheshimiwa Ernest Nyanda, alikuwa Waziri wakati fulani, nadhani wa Nishati, basi kwa kanuni za zamani za kuhoji bila mwisho, Marehemu, Mungu aiweke roho yake pema

peponi, wakati wa Spika Mzee Adam Sapi Mkwawa, akasema: "Mheshimiwa Spika, mimi nimechoka", basi hakutaka tena kuendelea kuhojiwa. Sasa utamfanyaje? *(Kicheko)*

Kwa hiyo, tunaweka Kanuni za kuwezesha Bunge lifanye kazi Kikatiba tofauti na vyombo vingine visivyokuwa vya Kikataba. Kwa hiyo, tukazanie kuihoji Serikali ndani ya Kamati zetu, ndiyo maana zimeundwa kufuatana na Wizara mbili au moja, huko ndiko tukazanie zaidi kule hakuna *time limit,* tuna siku 60 kwa mwaka. Tukazanie huko ndiko tutalisaidia Bunge letu lifanye kazi kwa ufanisi. Lakini tuking'ang'ania tufanye kazi humu ndani haitawezekana. Mimi naomba hilo lieleweke kwamba, tunaimarisha kanuni za kudumu maalum kwa ajili hiyo, kuwapa Wabunge fursa ya kuihoji Serikali kwa karibu zaidi na kupata majibu yanayoaminika. Ukimvamia Waziri hapa yeye pengine hana uhakika, hawezi kumwuliza Katibu Mkuu, kwa sababu amekaa nyuma ya kioo, unapata majibu ya kubabaisha tu. Kwa hiyo, ni vizuri tuone malengo ya mabadiliko haya. Ni kuimarisha kazi za Bunge.

Nashukuru Mheshimiwa mtoa hoja *(Makofi)*

**MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kutoa shukrani kwa kuchangia hii hoja. Pengine kabla sijaendelea niwataje wachangiaji. Nilikuwa na wachangiaji watano, watatu wamechangia kwa kusema humu ndani na wawili wamechangia kwa maandishi. Waliopata nafasi ya kusema humu ndani ni Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura na Mheshimiwa Lucas Selelii. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Leonard Derefa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri yaliyo ya msingi yote umepata nafasi ya kuyajibu na mimi nisingependa kuendelea kwa sababu yaliyo ya msingi kwa kweli yamejibiwa. *(Makofi)*

Isipokuwa nirudie moja tu ambalo Mheshimiwa Spika, umelieleza kwa ufundi sana. Nia ya Kanuni hii ni kuliwezesha Bunge kufanya kazi yake ya Kikatiba kwa makini, ndiyo nia kubwa na nia ya Kamati hiyo ilikuwa ni hiyo kuboresha hizi Kanuni ili kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge, kufanya kazi yao ambayo wamepewa kwa mujibu wa Katiba. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Spika kwamba, kazi hiyo nayo ina muda maalum, haiwezekani ikafanywa mwaka mzima.

Kwa hiyo, kwa muda huo lazima pia mpangiane namna ya kuendesha hizi shughuli ambazo mmepewa mbele yenu. Kwa mfano, hili ambalo Mheshimiwa Profesa Maghembe, amelieleza nia ya kifungu kile kubana haikuwa nia ni kubana. Nadhani mtakumbuka uzoefu tulioupata hapa kwenye Kamati kwamba, mnafika karibu mnamaliza watu hamsini wamesimama, sasa mnafanyaje, muda mnao mpaka saa 1.45 watu waliosimama 50. Kwa hiyo, Kamati ikaanza kufikiria ili kuboresha siyo kwa maana ya kubana, hapana, kwa maana ya kuboresha ikasisitizwa humu ndani kwamba, pamoja na kwamba hili lilikuwepo ndani ya Kanuni lakini pia lirudiwe kwamba, Mbunge yeyote, katika hatua hiyo anaweza akasimama akatoa hoja ya kuongeza muda ili kuwapa nafasi Wabunge zaidi.

Kwa hiyo, nia haikukusudia kubana ila ni kuongeza. Sasa sijui utafikiri ilikuwaje. Lakini hiyo ndiyo nia ya Kamati ile. Sasa mmeongeza muda tayari, Mbunge amesimama ametoa hoja, wote mmekubali mnaongeza muda, muda uliongezwa umekwisha. Sasa mnafanyaje, Bunge lina muda maalum mnafanyeje? Kwa hiyo, likatolewa wazo na hii ilikuwepo hata kabla ya mabadiliko hayo, kule nyuma ilikuwepo ilikuwa inaitwa *guillotine* kwamba, mfike mahali mpitishe. Lakini ni baada ya kuongeza muda tena. Kwa hiyo, ndiyo nia iliyokusudiwa kwamba, mfike mahali Mwenyekiti akiona muda uliobaki basi apitishe hayo mafungu kwa ujumla. Lakini pia hata kama Mwenyekiti akiona kwamba apitishe mafungu kwa maana ya kifungu kama ilivyoonekana kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani, ama ilivyoonekana kwenye *Foreign* kwamba, tusingehoji kila *Embassy,* lakini bado aendelee kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge, kuendelea kuhoji, si kwamba akihoji kwa ujumla wake basi watanyamaza, hapana, wanayo haki kabisa kwa mujibu wa Katiba kuhoji vile vifungu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema umeeleza vizuri zaidi, yale yaliyokuwa na utata ni hiyo, lakini karatasi ambazo nimepata kwa maandishi Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Leonard Derefa, wana tatizo la muda kwamba, muda wa kusoma uliotolewa kwa Waziri ni mdogo. Lakini hili

ulilitolea ufafanuzi vizuri kwamba, kweli muda ni mdogo, lakini ndiyo maana zile hotuba zinagawiwa mapema ili kuwapa fursa Waheshimiwa Wabunge kuzisoma vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini nikuhakikishie kwamba, haya yote yaliyotolewa, Kamati yako nadhani itapata nafasi ya kujaribu kuyatazama upya na kuyazingatia haya mapendekezo ambayo Waheshimiwa Wabunge, wote wameyasema na yote haya nadhani katika Kikao kijacho yatatazamwa na pengine mkaona mabadiliko yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa ya Kamati ya Kanuni za Bunge yalikubaliwa na Bunge)*

**Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje kuhusu Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Bunge la Afrika Mashariki**

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE:** Mheshimiwa Spika, kwa utamaduni tu, awali ya yote na mimi napenda nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Serikali kwa ujumla, kwa kufanikisha ujenzi wa Daraja la Mkapa huko Rufiji. Mafanikio hayo ni makubwa sana katika Sekta za Ujenzi na Mawasiliano katika nchi yetu. *(Makofi)*

Pili na mimi napenda kwa niaba ya Kamati, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge, waliochaguliwa kuingia katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tunawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa salamu hizo, kwa mujibu ya Kanuni ya Bunge Namba 96(2) Toleo la 2003, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Taarifa ya Kwanza ya Waheshimiwa Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jimbo la Tanzania, kama ilivyoambatishwa kwenye taarifa hii ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, sasa ikubaliwe na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kanuni hii ndiyo inayoweka utaratibu wa kufikisha Bunge taarifa za wawakilishi wetu kama vile Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wawakilishi wetu katika Chombo cha Wabunge cha Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC Parliamentary Forum)* na Mwakilishi wetu katika Bunge la ushirikiano baina ya nchi za Afrika, *Caribbean* na *Pacific (ACP)* na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(European Union) (The ACP - EU Consultative Parliament).* Tunatarajia kwamba, taarifa za Wawakilishi wetu watatu katika *SADC - PF* yaani Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa na Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine na Mwakilishi wetu katika Bunge la *ACP-EU,* Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, zitawasilishwa Bungeni katika Mkutano ujao. Hivi karibuni Kamati ilipokea na kujadili taarifa nzuri sana ya Mwakilishi wetu katika Bunge *ACP-EU,* Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Waheshimiwa Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliwasilishwa mbele ya Kamati yangu ya Mambo ya Nchi za Nje na Mheshimiwa Balozi Isaac Sepetu na Mwenyekiti wa Bunge wa Tanzania katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa niaba ya Wabunge wenzake Mjini Dar es Salaam tarehe 28 Mei, 2003 na kwa taarifa kamili, tazama kiambatanisho cha kwanza kama kilivyoonyeshwa kwenye taarifa hii.

Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati tumeonyesha kwenye taarifa hii, ambao ni pamoja na mimi Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine. Kwa sababu ya kuzingatia muda sitawasoma wote.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Tanzania, waliohudhuria mkutano huo wameonyeshwa katika taarifa yetu ukurasa wa tatu.

Lakini leo tunafurahi kwamba, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, yupo hapa na sisi kwenye *Speaker's Gallery,* pamoja na Mheshimiwa George Nangale, naye amehudhuria kwa ajili ya kutolewa kwa taarifa hii. Mheshimiwa Abdulrahman O. Kinana, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, hakuweza kuhudhuria mkutano huo kwa kuwa alikuwa safarini.

Mheshimiwa Spika, maudhui ya taarifa. Kamati yangu ilielezwa kwamba, Bunge la Jumuiya ya Afrika likiwa na Wabunge 27 wa kuchaguliwa na Mabunge ya nchi zao na Mawaziri watatu wenye jukumu la kusimamia mambo ya nchi za nje *(ex-official),* lilizinduliwa tarehe 30 Novemba, 2001 likiwa na majukumu yafuatayo huko Arusha:-

Kwanza, kutunga sheria zinazohusu masuala yote ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuwasiliana na Mabunge ya Nchi Wanachama kuhusu masuala ya jumuiya, kujadili na kupitisha Bajeti ya kila mwaka ya Jumuiya, kukagua taarifa za kamisheni za ukaguzi wa Mahesabu ya Jumuiya na taarifa zingine zozote zinazoletwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya na kujadili masuala yote yale yanayoihusu Jumuiya na kupeleka mapendekezo kwa Baraza la Mawaziri.

Pili, baada ya kuanza kazi zake, Bunge hilo la Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliunda Kamati ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake, Kamati hizi ni kama zilivyoonyeshwa katika ukurasa wa tano.

Mheshimiwa Spika, tatu, katika kutekeleza majukumu yake, mpaka sasa Bunge hili, limefanya mikutano tisa ambayo ilijadili masuala mbalimbali yakiwemo ya kumchagua Spika wa Bunge na kujadili Bajeti ya Jumuiya, pamoja na kushughulikia masuala mbalimbali yanayohusu Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Katika kutekeleza majukumu yake, Bunge pia limeweza kufanya shughuli mbalimbali nje ya Bunge, shughuli hizi ni warsha, semina mbalimbali, pamoja na ziara za kujielimisha katika maeneo mbalimbali yaliyo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa taarifa tuliyopewa, pamoja na mafanikio haya, Bunge hili linakabiliwa na matatizo makuu matatu yafuatayo:-

Kwanza, Mawaziri husika hawapeleki Miswada ya kutosha katika Bunge hivyo kufanya Wabunge wajishughulishe zaidi na Miswada binafsi.

Pili, Mawaziri hawashiriki kikamilifu katika Bunge hili kutokana na kuwa na majukumu mbalimbali katika nchi zao.

Tatu, ufinyu wa Bajeti wa Jumuiya ambao unakwamisha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Bunge.

Nne, kukosekana kwa *initial* sahihi kuhusu nafasi ya Bunge la Afrika Mashariki katika Utawala wa Jumuiya ikilinganishwa na mihimili mingine ya Utawala yaani Serikali Kuu na Mahakama katika uongozi mzima wa Jumuiya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadili Taarifa hii kwa kina, Kamati ilitoa maoni na ushauri ufuatao:-

Moja, Kamati ilitoa pongezi kwa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa juhudi inazofanya hususan kubaini hali ya maendeleo na matatizo ya Jumuiya na kuandaa Miswada binafsi ili kuliwezesha Bunge kuendelea na kazi zake baada ya kukosa Miswada kutoka kwa Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, pili, Kamati inashauri kwamba, kwa kuwa Wabunge wa Bunge hili wamechaguliwa na Wabunge wa Mabunge ya Nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kamati inashauri kuwa, Taarifa mbalimbali zinazohusu utendaji wa Bunge hili ziwe zinawasilishwa mara mbili kwa mwaka kwa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje na Taarifa kufikishwa Bungeni mara moja kwa mwaka ili ijadiliwe na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa upande wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, Kamati inapendekeza kwamba, Mkataba uliounda Jumuiya ya Afrika Mashariki ungebadilishwa ili taarifa za Bunge hilo, kama chombo cha Jumuiya ziwasilishwe kwa Wakuu wa Nchi badala ya Baraza la Mawaziri kama ilivyo sasa. Hatua hii italijengea Bunge uwajibikaji mkubwa zaidi na mawasiliano ya moja kwa moja baina ya nguzo kuu tatu za nchi zetu. *(Makofi)*

Nne, baada ya kubaini uchache wa Miswada inayowasilishwa katika Bunge hili pamoja na mahudhurio hafifu ya Mawaziri katika Mikutano ya Bunge, Kamati iliafiki ushauri wa Waheshimiwa Wabunge hao kuwa Serikali yetu pengine ingeteua Waziri pekee atakayeshughulika na Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na Bunge lake au iunde mfumo unaofanana na lengo hili. *(Makofi)*

Tano, Kamati inashauri vile vile kwamba, Bunge hili lipewe nguvu zaidi katika kutekeleza majukumu yake. Aidha, Serikali ya Tanzania ijishughulishe kwa nguvu sawa kwa majukumu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na zile katika Jumuiya ya Uchumi ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika *(SADC),* kwa lengo hasa la kuimarisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Sita, Kamati inapendekeza vile vile kwamba, Bunge la Jumuiya liwe makini na liangalie madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na maingiliano ya raia wa nchi zetu kabla ya kufikia uamuzi wa kuunda umoja kamili *(Federation)* ya Afrika Mashariki. Aidha, mahusiano baina ya raia wa nchi hizi yaangaliwe vizuri ili kuzuia matatizo yanayoweza kujitokeza katika maeneo ya ardhi, ajira na usalama kabla ya kufikia azma ya shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki na saba, ili kuvutia asasi mbalimbali za Jumuiya kuweka makao yao hapa nchini hususan katika Mji wa Arusha, miundombinu ya mji huo iendelee kuboreshwa kama kivutio cha washiriki wa mikutano kutoka katika nchi za Kenya na Uganda na wengine kutoka kote duniani. Aidha, Serikali tunapendekeza itoe ardhi haraka pindi haja ya kujenga taasisi za jumuiya inapojitokeza ili kuleta maendeleo ya kuvutia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nane Kamati imeshauri vile vile kwamba, ili kuleta uwiano katika uchumi, zoezi la ubinafsishaji katika nchi zetu, lingeweza kuoanishwa ili asasi muhimu kama vile usafiri wa reli na anga uwe unamilikiwa kwa pamoja kama ambavyo ingewezekana pale ambapo tungeweza kufanya hivyo. Lakini sasa tunavyozungumza kuna mambo mengi sana ya ubinafsishaji yameshachukuliwa hatua, sidhani kama tunaweza tukarudi nyuma. Lakini pendekezo hili lilikuwa linalenga kuangalia asasi kama usafiri wa reli kama ambavyo reli ya kutoka Musoma kwenda Arusha imependekezwa na asasi zingine za sura hiyo. Aidha, matumizi na usimamizi wa mazingira ya maji ya Ziwa Victoria yaangaliwe upya kwa pamoja ili kunufaisha nchi zetu tatu kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie na pendekezo la tisa nalo ni kwamba, katika kuongeza ushirikiano na majadiliano ya pamoja katika kutatua matatizo yanayoikabili Jumuiya ya Afrika Mashariki na Bunge lake, Kamati inashauri kuwa Kamati za Mabunge ya Jumuiya, ziwezeshwe kukutana mara kwa mara kutafuta namna ya kuimarisha ushirikiano. Hii ni pamoja na mashauriano kupitia Kamati mbalimbali yanayofanywa katika Kamati za Mabunge ya Jumuiya *(The Inter Parliamentary Committee for East Africa),* pamoja na Kamati zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kusema kwamba, Kamati kwa kweli inampongeza sana Mheshimiwa Abdulrahman Kinana, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa kwanza wa Bunge la Jumuiya ya Afrika. Aidha, Kamati inampongeza Mwenyekiti wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Isaac Abraham Sepetu na Waheshimiwa Wabunge, wenzake wote, kwa kuandaa na kuwasilisha taarifa yao ya kwanza mbele ya Kamati yangu kwa ufanisi mkubwa ili ifikishwe mbele ya Bunge lako Tukufu, kama ambavyo imeambatishwa pamoja na taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lijadili Taarifa hii ya Waheshimiwa Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na mapendekezo ya Kamati yangu na kuyakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kikao hiki kinaongozwa na Kanuni ambazo zilikubaliwa. Kwa hiyo, naomba niwakumbushe Kanuni zinazotawala hoja hii. *Regulations to provide for the procedures for the Tanzania Members of East African Legislative Assembly to submit regular report to the Tanzania Parliament.*

Kanuni ndogo ya 3 inasema: *"Such reports shall be primarily for the information of Members of Parliament."*

Kanuni ya 5: *"All such reports shall be laid on the table of the house for Hansard records only, and shall not be debated in the House itself."* Kwa hiyo, pendekezo la Kamati yetu limekiuka Kanuni hiyo. *"For primarily for the information of Members of Parliament, the report shall be laid on table for Hansard record only and shall not be debated in the House itself"* Kwa hiyo, ndiyo kinachotofautisha Bunge na vikao vingine vya kienyeji, Bunge lina Kanuni zake. Kwa hiyo, hakuna *debate.* Waheshimiwa Wabunge, tumepokea taarifa na itaingia kwenye *record* za Bunge hili. *(Makofi)*

Kwa yale mapendekezo yaliyotolewa na Kamati, Kanuni yetu inasema hivi: *"The Tanzania Members of the East African Legislative Assembly, may if they consider desirable to do so, present any special report or make any appropriate consultations with the Committee on any matter which is relevant to the work of the East African Legislative Assembly."* Haya mapendekezo tunachukulia chini ya Kanuni hii kwamba, ilikuwa ni *consultation* baina ya Wabunge hao na Kamati yetu ili Kamati iwasaidie kuboresha kazi yao katika Bunge lao, siyo katika Bunge hili. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, sasa tumefikia mwisho wa Kikao cha Asubuhi. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi 11.00 jioni.

*(Saa 6.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**KATIBU WA BUNGE, NDUGU KIPENGA M. MUSSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi na Mbili sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Kwa taarifa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu atoe Hoja ya Kuahirisha Bunge mpaka Mkutano mwingine. Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge lako Tukufu umekamilisha shughuli zote zilizokuwa zimepangwa. Jumla ya Maswali 407 ya msingi na mengine mengi ya nyongeza ya Waheshimiwa Wabunge yalijibiwa na Serikali katika Mkutano huu. Aidha, Bunge lako Tukufu limepitisha Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2003/2004 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara zote, Ofisi na Taasisi za Serikali. Vile vile Bunge limepitisha Miswada mitatu na kuridhia Maazimio kumi na moja.

Mheshimiwa Spika, naomba na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi na Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini kwa kuchaguliwa kuwa Wawakilishi wa Bunge letu katika Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Napenda vile vile nitumie fursa hii kutoa salamu za rambirambi na pole kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata msiba katika kipindi hiki, nao ni Mheshimiwa Thomas Nyimbo aliyefiwa na mama yake mzazi, Mheshimiwa Raphael Mlolwa aliyefiwa na mama yake mzazi, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, aliyefiwa na baba yake mzazi na Waheshimiwa Balozi George Kahama na mkewe Mheshimiwa Janet Kahama kwa kufiwa na mtoto wao na wengine ambao sikuweza kuwataja. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu wote mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Serikali kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao na ushauri kwa Serikali katika maeneo na Sekta mbalimbali. Serikali imepata michango mizuri iliyotolewa kwenye hotuba za Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge na vile vile ipo michango mizuri ya maandishi. Sote ni mashahidi jinsi idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge walivyochangia kwa njia hii ya maandishi. Utaratibu huu umeiwezesha Serikali kupata michango mizuri zaidi. Napenda kuwahakikishia kuwa kila Wizara imenukuu vyema masuala yote muhimu yaliyohitaji ufafanuzi wa Serikali. Masuala ambayo ufafanuzi wake haukutolewa ndani ya Bunge hili, Waheshimiwa Wabunge wataletewa taarifa hizo na Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika. Aidha, zile ahadi zilizotolewa na Serikali na ambazo zinahitaji utekelezaji, Serikali imezichukua na taarifa ya utekelezaji itatolewa kwa Waheshimiwa Wabunge kama ambavyo tumekuwa tukifanya kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Mkutano huu wa Bajeti ya mwaka 2003/2004 ukiendelea, tulipata fursa ya kuwa na Semina kuhusu juhudi zetu za mapambano dhidi ya umaskini. Kwa kutambua kuwa Bajeti ya Serikali ni nyenzo muhimu ya kupambana na umaskini, Serikali imechukua hatua muhimu katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 za kuhakikisha kuwa maamuzi ya kibajeti yanayochukuliwa yanajielekeza kwenye vita dhidi ya umaskini. Kwa mfano, Bunge limeidhinisha mapendekezo ya Serikali ya kuendelea kutoa kipaumbele katika ugawaji wa fedha katika maeneo ya kilimo, elimu, afya, barabara na maji. Pamoja na juhudi hizi za Serikali, lazima tukubali kuwa bila juhudi za mtu mmoja mmoja, vita dhidi ya umaskini haviwezi kufanikiwa.

Katika Bajeti ya Mwaka 2003/2004 tumetenga fedha kwa ajili ya mipango ya kuendeleza kilimo katika ngazi ya Wilaya. Kilimo ndiyo Sekta inayotegemewa zaidi na sehemu kubwa ya wananchi wetu. Kwa vile fedha hizi zitapelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri ni wajibu wa viongozi na Watendaji wa kila Wilaya kuandaa programu zitakazoweza kukibadili kilimo katika ngazi ya kaya. Fedha hizi siyo za kuendeshea Semina au Mikutano isiyo na mwisho. Jukumu la kila Mkuu wa Wilaya na kila Mkurugenzi wa Halmashauri ni kuhakikisha kuwa kwa uwezo huu mdogo unaofikishwa Wilayani, sasa wataalamu wataweza kuwafikia wakulima wengi zaidi na kuwasaidia. Mara nyingi viongozi wanapotembelea wakulima hushuhudia kilimo duni ikiwa ni uthibitisho wa jinsi wataalam wetu wa kilimo na hata viongozi wa utawala walivyo mbali na wakulima. Serikali inapeleka fedha nyingi Wilayani kwa ajili ya kuendeleza kilimo, lakini kama viongozi na wataalamu hawatakuwa karibu na wananchi kuwaongoza na kuwasaidia na wananchi nao kutumia utaalamu wanaopewa, kilimo chetu hakitabadilika na hali ya umaskini itaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo kama Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM), miradi ya afya, miradi ya barabara, maji na mingineyo. Ninapenda kusisitiza kuwa ni lazima fedha hizi zote zisimamiwe kikamilifu na taarifa zote za kweli zitolewe kwa wakati. Katika mradi wa MMEM, fedha za awamu ya pili, yaani za Mwaka 2003, kiasi cha jumla ya Sh.58,192,447,069/= tayari zimepelekwa katika Halmashauri zote isipokuwa zile Halmashauri zenye matatizo ya ama kutokamilisha ujenzi au zimeshindwa kukamilisha stakabadhi halisi yaani *Original Receipts.* Zile Halmashauri ambazo hazijakamilisha ujenzi ni Halmashauri za Wilaya ya Kilwa, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Halmashauri ambazo hazijatoa stakabadhi halisi ni Halmashauri za Manispaa ya Arusha na Iringa, Halmashauri za Wilaya za Ngorongoro, Ludewa, Kiteto, Iramba, Sikonge na Masasi. Halmashauri hizo zote zinapewa hadi mwisho wa mwezi huu yaani Agosti, 31 kuiwasilisha viporo wanavyodaiwa. *(Makofi)*

Ninapenda kusisitiza kuwa utaratibu wa matumizi ya fedha hizi ni kama ulivyokuwa kwa awamu ya kwanza ambapo fedha zilipelekwa moja kwa moja katika Kamati za Shule na Kamati hizo ziliamua ni nini cha kipaumbele katika Shule yao ndani ya shughuli zilizokubalika na mpango na kuiwekea mipango ya utekelezaji. Katika awamu ya kwanza, wapo waliokosea utaratibu huo na kuweka Wakandarasi wao ili wajenge Shule Vijijini na wananchi kubaki watazamaji. Hiyo siyo sahihi na isirudiwe tena na wala kisingizio cha wananchi kutokuwa na utaalamu wa kujenga hakikubaliki.

Kama wananchi hawawezi kujenga matofali, wanaweza kubeba mchanga, mawe, wanaweza kuchimba msingi wakielekezwa na muhimu zaidi wana uwezo na haki ya kushiriki katika kupanga na kusimamia miradi yao. Aidha, bei zinazotolewa na Wizara ni za dira na za juu. Inatarajiwa kuwa kwa kushirikisha wananchi, majengo yatajengwa kwa bei nafuu zaidi hivyo kupata majengo mengi au madawati mengi zaidi kuliko ilivyokadiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wametoa dukuduku zao na ushauri kuhusu Sekta ya Madini. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, Sekta hii inakuwa kwa kasi sana na ilikuwa kwa asilimia 15 Mwaka 2002 na kuliingizia Taifa kiasi cha Dola za Marekani milioni 431 mwaka huo wa 2002. Madini kama ilivyo kwa raslimali nyingine nchini ni mali ya Taifa na mapato yatokanayo na madini yanachangia katika kutunisha Hazina ya Serikali. Aidha, kuwepo kwa migodi na raslimali nyinginezo ni bora zichangie katika kuinua ubora wa maisha ya wananchi wetu. Vile vile, ni muhimu kuwa sheria na taratibu zote zinafuatwa katika umiliki, uchimbaji na biashara nzima za raslimali hizi.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge lako Tukufu na hasa katika Mkutano huu, tumeshuhudia malalamiko mengi dhidi ya baadhi ya Kampuni zinazochimba madini. Hata hivyo, ukitathmini hoja hizo utaona kuwa mengi ya malalamiko hayo yametokana na utendaji mbaya wa viongozi au Watendaji badala ya matatizo ya Kampuni yenyewe. Kama nilivyoahidi wakati wa kuhitimisha Hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Serikali itahakikisha kuwa matatizo ya msingi kama fidia kwa wananchi wa Geita yanatatuliwa kwa haraka, matatizo ya maeneo ya Tarime yanashughulikiwa na mengine ya mahusiano ya kawaida yanapatiwa ufumbuzi. Matatizo ya jumla yanayoendana na sura ya Mikataba yetu ya uchimbaji hasa kwa siku za baadaye pia yataangaliwa na Serikali. Ninapenda kusisitiza kuwa wawekezaji hawa wamefika nchini kwetu baada ya Serikali kuwakaribisha na hivyo ni Washiriki wenzetu katika ujenzi wa uchumi wetu. Ni vyema tuishi nao kwa uelewano na kushirikiana na penye hitilafu utatuzi utafutwe kwa mazungumzo na maelewano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza programu yake ya kufikisha umeme katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya huduma za uzalishaji na matumizi ya majumbani. Moja ya ahadi za Serikali ni kuhakikisha kuwa Makao Makuu yote ya Wilaya yanapatiwa umeme. Hata hivyo, kutokana na uwezo mdogo wa kibajeti wa Serikali na Shirika la Umeme - *TANESCO* kasi ya utekelezaji wa kazi hii ni ndogo kuliko matarajio ya wananchi. Serikali imesikia maelezo ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu umuhimu wa kuwapatia wananchi nishati ya umeme ili kupunguza athari za mazingira kutokana na matumizi makubwa ya kuni. Aidha, upatikanaji wa umeme wa uhakika ni kichocheo kikubwa cha maendeleo. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa hakuna upendeleo wowote katika kusambaza huduma za umeme nchini na lengo la kuboresha shughuli na mapato ya *TANESCO* ni hilo hilo la kusambaza umeme kwa kasi zaidi. Aidha, Serikali itaongeza kasi katika kuanzisha chombo na mfuko wa kusimamia na kugharamia miradi ya umeme Vijijini kama alivyokwishatangaza Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizi za kusambaza umeme, bado tunalo tatizo la msingi kuwa umeme wetu kwa sehemu kubwa unatokana na chanzo cha maji yaani, *Hydro-Generated Electricity.* Upatikanaji wake huathirika sana hali ya hewa inapokuwa mbaya. Hivi sasa maji katika mabwawa makuu ya Mtera, Kidatu na Nyumba ya Mungu yamepungua sana. Mito nayo pia ina maji machache sana na kipindi cha kiangazi ndiyo kinaanza. Hivi sasa tayari *TANESCO* inatumia mtambo wa *IPTL,* vinginevyo tungeanza mgawo wa umeme, jambo ambalo lina athari kubwa sana kwa uchumi na ustawi wa jamii yetu. Pamoja na hayo, napenda kusisitiza jambo moja muhimu la sote kuwa waangalifu na matumizi ya umeme ili umeme mdogo uliopo utumike kwa ufanisi zaidi. Tusiwashe taa au vyombo vya umeme wakati hatuvihitaji.

Mheshimiwa Spika, kuingia kwa Kampuni ya *IPTL* katika uzalishaji wa umeme kumeleta utaratibu mpya wa uzalishaji umeme unaomilikiwa na Makampuni Binafsi yaani *Independent Power Plants (IPP).* Katika muda mfupi ujao Kampuni ya *Songas* nayo itaingia katika utaratibu kama huu wa kuzalisha umeme na kuuingiza katika gridi ya Taifa. Tunayo vile vile programu ya mradi wa Mchuchuma ambao nao utakapojengwa utazalisha umeme na kuingiza katika gridi ya Taifa. Hizi zote nazo ni *IPP* nyingine. Umeme wa *IPP* kwa kawaida ni ghali lakini hutuokoa wakati wa matatizo ambapo vinginevyo

gharama yake ingekuwa kubwa zaidi kwa uchumi. Nina uhakika mwaka huu Watanzania tutaona manufaa ya utaratibu huu wa kutumia *IPP* kwa maana ya *IPTL* tuliyonayo kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kuhakikisha kuwa umeme wa gridi ya Taifa unasambazwa maeneo mengi nchini, tunao wajibu vile vile wa kushirikiana na Taasisi zetu zenye utaalamu wa nishati mbadala ili tuweze kueneza teknolojia hii katika maeneo mengi kadri iwezekanavyo. Matumizi ya umeme nuru yaani *solar* yanaweza kutauta matatizo ya nishati kwenye majengo ya huduma kama vile Shule, Zahanati na kadhalika. Katika Mikoa yenye mifugo mingi, matumizi ya bayogesi yanaweza kabisa kuanzishwa na kuenezwa. Tatizo tulilonalo ni la uelewa mdogo wa kuona nishati mbadala kama nishati isiyotosheleza. Uwezo wa Serikali kusambaza umeme wa gridi ya Taifa kwa kasi unategemea uwezo wetu wa kibajeti. Lakini nishati mbadala, ni nishati iliyopo na isiyoisha na inayoweza kutumika kwa kutumia teknolojia rahisi.

Mheshimiwa Spika, kila Halmashauri ikiweza angalau kuwa na programu ya kusambaza kwa awamu nishati ya umeme nuru, matumizi ya bayogesi, nishati ya upepo na kadhalika katika maeneo ya huduma tutaweza kupiga hatua kubwa kwani hata wananchi wa kawaida wataweza kujifunza na kuanza kutumia teknolojia hizo. Kwa mfano, katika Mikoa ya ukame kama Shinyanga, Mwanza, Singida, Dodoma, Arusha, ambapo mifugo ni mingi sana na miti ni haba sana, nishati ya bayogesi ingeweza kutoa jawabu kwa mahitaji ya nishati ya kupitia na hivyo kuokoa mazingira ambayo yanaendelea kuteketea hasa kwa watu kukata sana miti kwa ajili ya kuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu sera ya uchumi zilizokuwepo huko nyuma ambapo njia zote kuu za uchumi ziliendeshwa na dola. Hata hivyo, sera hizo zilibadilika na tukawa na Sera za Uchumi Huria ambazo ziliambatana na mageuzi yaani, *reforms* katika uchumi wetu. Katika mageuzi haya, Sekta Binafsi ndiyo inayoachiwa kumudu uchumi, Watanzania wengi kushiriki katika uchumi wao, ajira kuongezeka na mapato ya Serikali nayo kuongezeka. Hivyo, sera hizi zinaitoa Serikali katika shughuli za kufanya biashara moja kwa moja na badala yake Serikali inakuwa mhimili wa uchumi. Hii inaipa Serikali nafasi ya kutosha na raslimali za kutekeleza majukumu ya msingi ya dola hasa ya ulinzi na usalama na huduma za jamii. Hivyo, tuliamua kubinafsisha Mashirika yetu ya Umma, kuwavutiawawezizaji wa ndani na nje na kukuza Sekta Binafsi ili kutekeleza sera hizo zenye lengo la kuboresha uchumi na maisha ya Watanzania ili hatimaye kujenga uchumi unaojitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wametoa mawazo kuhusu namna bora ya kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji bila kuathiri maslahi ya umma. Serikali inapenda kukubaliana na Hoja hizo. Hata hivyo, ni vyema Watanzania tuelewe vile vile kuwa katika dunia ya leo ya utandawazi, kila nchi inajaribu kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji. Kwa hiyo, upo ushindani mkubwa sana. Wawekezaji wawe wa ndani au wa nje, ni watu wanaovutiwa na faida itakayopatikana kutokana na kuwekeza raslimali zao. Sisi tumeweka masharti mbalimbali yanayowabana, lakini vile vile tumeweka masharti yanayowavutia. Ongezeko la uwekezaji katika nchi yetu na ongezeko la ajira na mapato ya Serikali ni ushahidi wa kutosha kuwa tunafanya vizuri katika kutekeleza sera zetu. Mashirika ya nje na nchi marafiki, nao wanakiri juu ya mafanikio haya ya utekelezaji wa sera zetu. Jambo la msingi ni Watanzania tushirikiane na wawekezaji hawa ili nasi tushiriki katika kujenga uchumi na kujifunza kwa kasi kubwa mbinu za kisasa za uzalishaji na za biashara. Sera ya uchumi huria na dhana ya kubinafsisha Mashirika ya Umma kwa watu binafsi zote ni ngeni kwa Watanzania. Tunahitaji muda wa kuelimishana na pia wa kuvumiliana.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa katika suala la uwekezaji yapo matatizo yanayojitokeza na yanayowahusu wadau wote. Napenda nilihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa kila mara tumejaribu kuyatatua matatizo hayo kwa mazungumzo na wahusika wote. Pale tulipobaini kasoro, zilirekebishwa ipasavyo. Hata hivyo, ili tuweze kuyatatua matatizo hayo, tunahitaji ushirkiano uliojengwa kwa mashauriano ya mara kwa mara. Majadiliano siku zote husaidia sana katika kutoa ufumbuzi wa matatizo na wala tusitafute njia za mkato. Suala hili linahusu Serikali, wawekezaji au wenye raslimali zao nchini, wafanyakazi na wananchi wanaoishi karibu na maeneo yenye wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kujengeka kwa Sekta Binafsi na kuanza kuchukua nafasi yake kama kiongozi wa ukuaji wa uchumi kumeanza vile vile kutoa changamoto kubwa kwa wafanyakazi na vyama vyao,

Serikali na hata kwa wananchi wa kawaida. Kwa upande wa wafanyakazi tumeanza kushughudia migogoro katika maeneo ya kazi ikiongezeka. Misuguano na migogoro katika maeneo ya kazi huathiri tija na kuleta usumbuzu kwa wale wanaostahili kupata huduma. Kwa bahati nzuri Taifa letu limejiwekea taratibu za kutatua migogoro inayojitokeza kwa njia ya maelewano. Tunavyo vyombo madhubuti na vyenye uwezo na taaluma ya kuwawezesha waajiri na wafanyakazi kutekeleza wajibu wao kwa pamoja na kwa maelewano.

Matatizo haya kwa sehemu kubwa yanatokana na hulka ya binadamu ya kuogopa na ikabidi kupinga mabadiliko mapya hata kama yangekuwa ni ya manufaa kwake. Aidha, ni wazi kuwa mabadiliko haya ya sera yamekuja na mabadiliko katika mazingira ya kazi na hata katika maslahi. Kwa mfano, wafanyakazi lazima watambue kuwa mazingira ya kazi sasa ni tofauti na yale yaliyokuwepo chini ya Mashirika ya Umma. Kampuni binafsi inaangalia zaidi faida, iwe Kampuni ya Mtanzania au Mwekezaji kutoka nje. Viwango vya tija vinavyodaiwa kutoka kwa wafanyakazi ni tofauti sasa lazima vitakuwa tofauti na ubora wa kazi pia utakuwa ni tofauti. Haya yote ni sehemu ya mabadiliko ambayo ni lazima tuyakubali. Hata hivyo, Vyama vya Wafanyakazi na hatimaye Serikali wanalo jukumu la kutetea haki za wafanyakazi pale ambapo zitaonekana zinaminywa. Wito wangu leo ni kuwataka wafanyakazi na waajiri kutumia vyombo vyao rasmi vya majadiliano kikamilifu kutatua matatizo yanayojitokeza katika sehemu zao za kazi kabla matatizo hayo hayajaleta athari kwa uzalishaji au hata kuathiri amani na utulivu mahali pa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo hisia na hata hoja zinazojengwa kwamba ubinafsishaji unaua au kupunguza ajira. Ukweli ni kwamba ubinafsishaji si lazima usababishe upotevu au upunguzaji wa ajira na mara nyingi huwa ni kinyume chake, yaani huongeza na huboresha ajira. Kwa mfano wafanyakazi wengi walipoteza ajira zao hata kabla sera ya ubinafsishaji haijaanza kutekelezwa kwani Mashirika yapatayo 70 yalikuwa yamefungwa na hivyo kuwafanya wafanyakazi husika kutokuwa na ajira kabisa. Baadhi ya Mashirika hayo sasa yamefufuliwa na yanafanya kazi katika viwango vya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nitaje mifano michache. Viwanda vya Nguo karibu vyote nchini vilikuwa vimefungwa kabla ya ubinafsishaji. Hali hiyo imebadilika sana kwa viwanda vile ambavyo vimekwishabinafsishwa. Kwa mfano, Kiwanda cha *Sungura Textile* sasa kimefunguliwa na kimeajiri wafanyakazi wapatao 2000. *Mwanza Textile* ina wafanyakazi 626, *Kilimanjaro Textile* ina wafanyakazi 450 na kadhalika. Kiwanda cha Madawa cha Arusha kilikuwa kimefungwa kwa miaka mitatu kabla ya kubinafsishwa kwa Watanzania mwaka 1997 na hivi sasa kimeajiri wafanyakazi 91. Kabla ya ubinafsishaji Kiwanda cha Mablanketi cha Dar es Salaam nacho pia kilikuwa hakifanyi kazi. Sasa kimefufuliwa baada ya kupata mwekezaji Mtanzania mwaka 1997 na kimeajiri zaidi ya wafanyakazi 80. Kiwanda cha Bora nacho kilikuwa kimefungwa kabla ya kubinafsishwa. Sasa kimeanza kufanya kazi na kimeajiri zaidi ya wafanyakazi 400 na kadhalika.

Viwanda vya sukari vimeongeza ajira ya wakata miwa na wakulima wadogo yaani *out growers,* watengenezaji wa bidhaa zinazotumia sukari na kadhalika. Wakulima wa mazao mengine kama tumbaku na chai nao wameajiajiri na kuongeza uzalishaji baada ya kuhakikishiwa soko katika viwanda ambavyo vimefufuliwa na kuendelezwa baada ya ubinafsishaji.

Vile vile, wote tumeshuhudia kushamiri kwa biashara ya kufyatua na kuuza matofali kutokana na uzalishaji wa saruji kuongezeka na kusambazwa nchi nzima kwa uhakika. Watanzania wengi sasa mapato yao yanategemea biashara ya kutengeneza na kuuza matofali, ujenzi wa nyumba na kadhalika. Kwa upande mwingine, inakadiriwa kwamba mapato na maisha ya zaidi ya Watanzania 300,000 hutegemea sana usambazaji na ugawaji wa bidhaa za Kampuni za bia na sigara kutokana na ongezeko kubwa la uzalishaji baada ya Kampuni hizo kubinafsishwa. Bila shaka idadi kubwa zaidi ya Watanzania wameajiriwa katika Sekta nyingine ambazo zinafanya kazi kwa ufanisi baada ya ubinafsishaji kufanikiwa. Wito wangu kwa Watanzania ni kuwa tuuangalie ubinafsishaji kwa mtazamo mzuri na wenye lengo la kutusaidia kujenga uchumi wa kisasa unaoendeshwa na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, dhana ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi ni moja ya vipengele muhimu sana katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000. Kazi tunayofanya sasa na katika kipindi hiki kilichopo mbele yetu ni kuweka mazingira yatakayotoa fursa kwa Watanzania kumiliki na

kuendesha shughuli za uchumi. Watanzania tunaowazungumza ni wale wote ambao ni wanyonge na ambao hali zao ni duni. Serikali ilianzisha mikopo ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Mikopo hii imekuwa kichocheo kikubwa kwa wale waliokopa katika kuanzisha shughuli za uzalishaji mali.

Kwa mfano, katika Mkutano huu ilitolewa taarifa kuwa Mfuko wa Wafanyabiashara Wadogo unaoendeshwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO)* umetoa mikopo 15,539 yenye thamani ya Shilingi bilioni 5.33. Kinachotia matumaini ni kuwa sasa baadhi ya wananchi wanaokopa wanatambua kuwa fedha hizo ni deni na siyo ruzuku kutoka Serikalini. Kwa mfano kiwango cha urejeshaji mikopo katika Mfuko wa Wafanyabiashara Wadogo kimepanda kutoka asilimia 60.7 mwaka 1994/95 hadi asilimia 86.7 mwaka 2002/2003. Mfuko huu na mingine itaendelea kutumiwa na Serikali kama sehemu ya kujenga uwezo wa kuwasaidia Watanzania kujikwamua kiuchumi. Napenda kusisitiza wito kwa wakopaji kuzingatia kurudisha mikopo ili kupata idadi kubwa zaidi ya Watanzania watakaokopa.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji nao umetumika kama njia ya kuwawezesha Watanzania kiuchumi. Kumekuwa na hisia kuwa ubinafsishaji wa mashirika ya umma umewaacha pembeni Watanzania walio wengi. Mtazamo huu nao siyo sahihi kama tulivyowahi kutoa takwimu ndani ya Bunge lako Tukufu. Viwanda na mashirika yaliyonunuliwa na Watanzania peke yao ni kama robo ya mashirika yote yaliyobinafsishwa, yaliyobinafsishwa kwa ushirika wa wageni na Watanzania na/au Serikali ndiyo mengi zaidi na yaliyobinafsishwa kwa wageni peke yao ni chini ya asilimia kumi. Aidha, ushiriki wa Watanzania katika kumiliki hisa kwa kupitia kituo cha uwekezaji cha *Dar es Salaam Stock Exchange (DSE)* nao pia ni mzuri. Watu wengi wameelewa umuhimu wa kumiliki hisa katika makampuni yaliyoko katika *Dar es Salaam Stock Exchange.* Kwa mfano, katika kampuni ya bia *(TBL)* Watanzania mmoja mmoja zaidi ya 23,000 ni wanahisa, katika kampuni ya Sigara *(TCC)* zaidi ya Watanzania 7,508 ni wana hisa, katika kampuni ya Saruji Tanga zaidi ya Watanzania 14,228 ni wanahisa, katika kampuni ya *DAHACO* zaidi ya Watanzania 41,025 ni wanahisa, katika Benki ya *CRDB,* Watanzania zaidi ya 11,000 ni wana hisa. Hii ni jumla ya hisa 96,761 zinazomilikiwa na Watanzania katika kampuni hizo tano tu. Katika kuboresha ushiriki huu na mingine katika uchumi, Serikali hivi sasa inakamilisha sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Sera hiyo itafuatiwa kwa karibu sana na Muswada wa Sheria wa uwezeshaji Watanzania ambao itawasilishwa katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kifupi kilichopita Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo limeweza kuandaa maonyesho ya bidhaa za viwanda vidogo kikanda. Mimi nimebahatika kuona baadhi ya bidhaa zinazotengenezwa na viwanda hivi. Yapo mabadiliko makubwa yanayoanza kujitokeza katika ubora wa bidhaa hizi hususan katika eneo la usindikaji wa vyakula na eneo la ushonaji. Wale waliobahatika kutembelea maonyesho ya Saba Saba katika viwanja vya Mwalimu J. K. Nyerere mwaka huu watakubaliana nami kuwa huko tunakoelekea ni kuzuri. Wazalishaji wadogo wameanza nao kutambua umuhimu wa ubora wa bidhaa zao. Bidhaa bora zinazozalishwa nchini zitaweza kabisa kushindana na bidhaa zinazotoka nje hivi sasa. Jukumu la wataalam wetu hususan Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO)* ni kuendelea kuwasaidia wazalishaji hawa kwa kuwakutanisha na wananchi wengi kadri iwezekanavyo kwa kuwasaidia kuandaa maonesho ya bidhaa zao mara kwa mara.

Aidha, tuanze sasa kuangalia soko la nje. Nguo bora za pamba zina soko kubwa sana Marekani na Ulaya katika kipindi hiki cha kiangazi. Ni vyema tuongeze bidii katika utekelezaji wa mkakati wetu wa kutumia kikamilifu fursa zinazotolewa na mpango wa Marekani wa *AGOA,* ule wa nchi za Ulaya wa *EBA* na ule wa Canada wa *PACT.* Nchi yetu bado ipo nyuma sana katika kufaidika na fursa hizi, wakati inazo bidhaa ambazo zinaweza kuingia katika masoko haya. Tunao utashi wa kisiasa na kwamba Serikali ipo tayari kuwasaidia wazalishaji wa ndani ya nchi wanaopenda kuingia katika masoko hayo. Sisi viongozi tuwasaidie wazalishaji hawa ili waweze kuvuka vikwazo mbalimbali wanavyokumbana navyo ili kuyafikia masoko hayo ya nje na pia kumudu ushindani ulipo katika masoko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upunguzaji wa kero za wananchi, moja ya ahadi kuu katika ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 ni kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi. Katika kutekeleza ilani hiyo, Serikali katika Bajeti yake ya 2003/2004 imechukua hatua ya kuondoa baadhi ya kodi zenye kero kwa wananchi na kuziwekea viwango maalum kodi zingine. Uamuzi huu ni matokeo ya kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na Serikali ya kuboresha mapato na kusimamia matumizi ya Serikali. Baada ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato *(TRA)* ukusanyaji wa kodi umeimarishwa, mianya ya ukwepaji kodi imezibwa

kwa kiasi kikubwa na mazingira yanayowezesha walipa kodi kufahamika na kuwajibika yamewekwa. Haya yote yameongeza mapato kutoka shilingi kati ya 25-30 bilioni mwaka 1995 hadi shilingi 100 bilioni hivi sasa kwa mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kujenga uwezo huu, huwezi kufuta kodi vinginevyo uamuzi wa aina hiyo ungekwamisha utekelezaji wa shughuli za Serikali na shughuli za maendeleo ya wananchi. Baada ya kuona hali hii ya mafanikio, Serikali ilifanya utafiti wa kuona ni kodi gani ambazo zingeliweza kufutwa na ni zipi ambazo zingelirekebishwa. Lakini muhimu zaidi mapato ya kujazia mapengo yatakayojitokeza yangelipatikana wapi. Kazi hizo zote tumezifanya na matokeo yake ndiyo haya ya kufuta baadhi ya kodi na kurekebisha zingine ili kuwapatia nafuu wananchi hasa wa kawaida. Hili siyo jambo jipya kwa serikali yetu kuondoa kodi. Serikali imekwisha wahi kufuta kodi zote katika pembejeo na zana za kilimo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikusudii kuchangia katika mabishano kuhusu kufutwa kodi ya maendeleo ni sera ya nani. Lakini kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawajui, basi wananchi wanajua kuwa ni nani walimchagua Mwaka 2000 na ni nani sera zake zinatekelezwa na Serikali na ni nani aliyekuwa akifanya juhudi hizi zote hadi tukafikia mafanikio haya. Ninapenda kuwahakikishia wananchi kuwa Serikali yao kwa kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, itaendelea kuboresha maisha yao kama tulivyoahidi na huu ni mwanzo tu na ni uthibitisho wa usahihi wa uamuzi wa Rais wetu Mheshimiwa Benjamin Mkapa, aliposema kuwa ni lazima tukubali kubeba mzigo mzito sasa kwa ajili ya neema ya baadaye. Kauli zake nyingi tunaziona katika utekelezaji na wananchi wetu wanafurahia matunda yake. Hakuna haja ya kugombea mali na mwenyewe yupo. Alipolihutubia Bunge lako Tukufu taredhe 30 Novemba, 1995, Rais Benjamin Mkapa alisema nanukuu: *(Makofi)*

"...... kuweka mpangilio mzuri wa shughuli za uchumi ili kuongeza mapato ya Serikali ni moja ya wajibu wa kwanza wa Serikali. Bila mapato ya kutosha, Serikali haiwezi kuwa na uwezo wa kujiendesha na wakati huo huo ikiweza kutoa huduma za kawaida kwa watu wake. Mwisho wa kunukuu." *(Makofi)*

Ni wazi basi kuwa dhamira ya Rais wetu na usahihi wa sera za Chama tawala ndizo zilizotufikisha hapa leo. Tangu wakati huo, hatua zote tulizozichukua zililenga kuongeza uwezo wa Serikali kutoa huduma bora kwa wananchi katika pande zote za nchi yetu. Tumeongeza mapato yetu ya ndani kutoka shilingi 448,373 milioni mwaka 1994/1995 hadi matarajio ya makusanyo ya shilingi 1,393,026 bilioni katika mwaka huu wa fedha. Hili ni ongezeko la asilimia 211. Bado hata hivyo tuna safari ndefu. Tunaelewa kuwa mapato yetu ya ndani ni asilimia 12.3 tu ya Pato la Taifa ambayo ni madogo kuliko jirani zetu wa Kenya ambao wamefika asilimia 24. Kwa hiyo, suala muhimu sio kufuta kodi tu, bali pia kupanua wigo wa kodi ili wote wenye stahili ya kulipa kodi walipe pamoja na kuziba mianya yote ya ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 4 bilioni kama ruzuku kwa Halmashauri zote nchini kutokana na uamuzi huo wa kufuta kodi zenye kero. Hivi sasa Serikali imekamilisha kuandaa utaratibu utakaotumika katika kutoa ruzuku hiyo kwa Halmashauri na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa atatangaza utaratibu huo ili wote tuweze kufahamu kila Halmashauri inapewa kiasi gani cha fedha. Kufutwa kwa kodi zenye kero na kutolewa kwa ruzuku kwa Halmashauri ni changamoto kwa uongozi wa Halmashauri zetu kuongeza bidii ya kukusanya kodi zile ambazo hazijafutwa. Kila Halmashauri inao wajibu sasa wa kuhakikisha kuwa mapato yote yanayostahili kukusanywa kutoka katika vyanzo vingine yanakusanywa. Kutolewa kwa ruzuku kusiwe kigezo cha Wakurugenzi wa Halmashauri kutosimamia zoezi hili kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekwisha fafanua idadi na aina za kodi zinazotozwa na Halmashauri na ambazo ama zimefutwa au zimewekewa viwango maalum. Hata hivyo, ninapenda kuweka msisitizo tu kwenye ufafanuzi wa baadhi ya kodi chache sana.

Kodi ya Maendeleo imefutwa kabisa kwa watu wote ikiwa ni pamoja na kwa wafanyabiashara, wakulima na wafanyakazi. Kwa wale ambao walikuwa hawajalipa kodi hizo, hawatadaiwa tena na wale waliokwisha lipa, nao hawatarudishiwa. *(Makofi)*

Kodi ya pili, nataka kuzungumzia kodi ya mifugo, kodi zote za mifugo zimefutwa isipokuwa kodi itakayotozwa ukishamwuza na kununua ng'ombe mnadani na kodi ya kuhamisha mifugo *(movement permit)* itayotozwa na Serikali Kuu.

Hii maana yake ni kuwa ng'ombe anayechungwa halipiwi kodi, ng'ombe anayepelekwa mnadani halipiwi kodi isipokuwa akishanunuliwa, ng'ombe anayesafiri kwa miguu yake yaani mfugaji anayehama na mifugo yake kutoka Wilaya moja hadi Wilaya nyingine au mkoa mmoja hadi mkoa mwingine mradi ana *movement permit* halipi kodi ya Halmashauri anakopitia au anakofikia. Ng'ombe anayesafirishwa kwa gari au garimoshi halipiwi kodi mradi wawe na *movement permit.*

Aidha, mchuuzi au mfugaji anapofikisha ng'ombe wake katika mnada wa kati *(secondary market)* kama Pugu halipishwi kodi. Kodi itatozwa tu baada ya ng'ombe huyo kuuzwa mnadani na siyo anapofikishwa mnadani. Kwa kodi zote za nyuma ambazo hazikulipwa nazo hazitadaiwa tena na zilizolipwa hazitarudishwa.

Baada ya kodi hizo kuondolewa, kuna taarifa sasa zinazoonyesha kuwa baadhi ya Halmashauri hazioni sasa faida ya kuwa na wafugaji hivyo kuanza kuwanyanyasa kwa kudai kodi za nyuma lakini hasa kwa kuwalazimisha wapunguze mifugo yao wakati mwingine kwa asilimia hata zaidi ya 80 vinginevyo wafunge virago. Haya yote ni marufuku. Upunguzaji wa idadi ya mifugo hauna uhusiano na kufutwa kwa kodi ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona nilifafanue zaidi eneo hili kwa sababu lina matatizo mengi. Wiki hii nimewasikia wafugaji na wachuuzi wa mifugo wakilalamikia sana jambo hili. Jambo lingine lililolalamikiwa ambalo siyo la kodi ni polisi kuwashusha vijana wanaosindikiza ng'ombe katika malori yaliyopakia ng'ombe kwa kisingizio kuwa malori hayasafirishi binadamu.

Serikali tumekuwa tunahimiza sana usafirishaji wa mifugo kwa njia ya malori au gari moshi badala ya kuwatembeza. Ng'ombe wakiwa ndani ya lori au gari moshi, ni lazima wawepo watu wa kuwahudumia vinginevyo huumizana hata kuuana wakati gari linapotingishika hasa gari linapofunga breki au kuongeza mwendo. *(Makofi)*

Hivyo ninawaagiza polisi wasiwabughudhi vijana hao ili mradi idadi yao inaonekana ni sahihi *(reasonable)* kwa idadi ya ng'ombe waliopo kwenye gari. *(Makofi)*

Napenda nirudie sehemu hiyo, hivyo ninawaagiza polisi wasiwabughudi vijana hao wanaosindikiza magari ili mradi idadi yao inaonekana ni sahihi yaani *reasonable* kwa idadi ya ng'ombe walioko kwenye gari. *(Makofi)*

Kodi ya ushuru wa mazao itatozwa kwa kisichozidi asilimia tano ya bei ya soko ya zao lile. Kwa hiyo, hatutozi tena mazao kwa bei moja ya kudumu. Kodi ya mazao ya msitu kama magogo, mbao zitokazo msituni, mkaa, kuni za biashara, nguzo za biashara, zitatozwa nazo ushuru usiozidi asilimia tano (5). *(Makofi)*

Ushuru hautatozwa pia kwa magari ya abiria yanayoshusha na kupakia watu katika vituo vya kawaida isipokuwa katika vituo vikuu tu *(Central Bus Stands),* na Eneo la mwisho ambalo nataka kulitolea tu ufafanuzi. Ushuru hautatozwa kwa watu wanaofanya biashara ndogo ndogo ambao hufika asubuhi kuuza chochote walichonacho bila kuwa na meza maalum katika masoko rasmi.

Mheshimiwa Spika, nimesema ushuru hautatozwa kwa watu wanaofanya biashara ndogo ndogo ambao hufika asubuhi kuuza chochote walichonacho bila kuwa na meza maalum katika soko rasmi. Hawa ni wakinamama wanaouza maandazi, wanaouza michicha, vijana wanaochoma mahindi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kodi zilizofutwa na zingine kurekebishwa ni nyingi na Waziri mhusika atapeleka waraka maalum wenye ufafanuzi kwa Halmashauri zote. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wanao

waraka wa Waziri wa Fedha wenye ufafanuzi wa kutosha, hivyo wanaweza kutumia waraka huo kusaidia kuwaelewesha watendaji katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, siku ya Jumamosi tarehe 2 Agosti 2003, Mheshimiwa Rais Mkapa alifungua daraja kubwa na zuri la Mto Rufiji, daraja lililopewa jina lake mweyewe la Daraja la Mkapa. Sote tutakumbuka kuwa ujenzi wa daraja hili na barabara ya Kusini vimekuwa wimbo kwa miaka mingi sana. Ilani za CCM nazo zimeandika mara kadhaa juu ya dhamira ya utekelezaji wa daraja na barabara hiyo. Sasa daraja limekamilika na barabara nayo inajengwa. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imetekelezwa siku hiyo na wananchi walishangilia sana, lakini wana wa Kusini walishangilia zaidi maana ndiyo hasa wenye harusi.

Ninaamini wapinzani wakiongozwa na viongozi wao nao walishangilia sana lakini nina hakika wana CCM walishangilia zaidi kwa sababu ndiyo mwali wao. Kama kuna mtu aliyebeza jambo lile, basi hajui analolifanya. Daraja hili ni jambo kubwa katika uhai wa nchi yetu na maendeleo ya wananchi wetu wote. Sote tujivunie mafanikio yale hata kama ni utekelezaji wa sera za CCM. Hivi wakati CCM ikiwa madarakani tutalipata jambo lipi linalotekelezwa na Serikai yake ambalo sio utekelezaji wa Ilani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilishangaa sana kusoma katika baadhi ya vyombo vyetu vya habari kuwa CCM wasiteke nyara sherehe za ufunguzi wa daraja. Hivi zile bendera zote alizoziona mwandishi huyu ni za CCM tu? Hivi mwandishi alitaka CCM wakajifiche wakati wa Sherehe. CCM watasherehekea jambo la mafanikio na watasikitikia jambo la fedheha. Walisherehekea kwa kuonyesha furaha yao kwa mafanikio ya Ilani ya Chama chao kutekelezwa na wala hawakuteka nyara sherehe. Ninawaomba Watanzania tuwe kitu kimoja katika mambo makubwa na muhimu kama yale ya Daraja la Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya nchi yetu yanakabiliwa na ukame mkubwa hivi sasa. Upungufu wa chakula umeanza kujitokeza, lakini vile vile hali ya upatikanaji wa maji hususan kwenye mabwawa na mito imeanza kupungua kwa kasi sana. Ni wazi kuwa katika muda wa kuanzia sasa hadi msimu mwingine wa mvua utakapoanza itatubidi kuchukua maamuzi thabiti ya kukabiliana na hali hii. Kuhusu hali ya upungufu wa chakula, takwimu ambazo Serikali inazo zinaonyesha kuwa katika msimu wa mwaka 2002/2003 uzalishaji wa mazao utafikia tani milioni 7.5 wakati makisio ya mahitaji ya chakula kwa Mwaka 2003/2004 ni tani milioni 8.37.

Kwa hiyo, upo upungufu wa takriban tani 800,000. Hata hivyo, kutokana na albaki ya mazao ya msimu uliopita na chakula walichonacho wafanyabiashara inakadiriwa kuwa kutakuwepo na pengo halisi la upungufu la tani 350,000 za chakula. Aidha, kutokana na hali hii watu 1,939,693 wanakabiliwa na upungufu mkubwa wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itachukua hatua za haraka kutafuta kiasi cha tani 77,489 za chakula ili kuweza kuwasaidia wananchi hao wanaokabiliwa na upungufu wa chakula. Sehemu ya kiasi hiki kitatoka katika Hifadhi ya chakula ya Taifa na kingine itabidi tuombe kutoka kwa wahisani. Ili angalau Serikali iweze kubeba baadhi ya gharama, mahindi kutoka Hifadhi ya Taifa yatauzwa kwa bei nafuu kidogo kwa kaya zenye uwezo mdogo.

Endapo tutafanikiwa kupata chakula kutoka kwa wahisani chakula hicho kitatolewa kwa utaratibu wa chakula cha kazi ambapo wananchi watakaohusika chini ya utaratibu huo itabidi wafanye kazi za maendeleo au kwenye mashamba yao kwa lengo la kujitayarisha zaidi kwa msimu ujao wa kilimo. Wafanyabiashara watahusishwa kwa karibu sana katika kuagiza chakula ili kuziba pengo litakaoljitokeza. Inakadiriwa kuwa wafanyabiashara wataagiza kiasi cha karibu tani 273,000.

Hali hii ya ukame na upungufu wa chakula imezikumba pande zote mbili za muungano wetu. Serikali zetu mbili zinashirikiana ili kuhakikisha kuwa tunaidhibiti hali hii na hivyo kuwezesha upatikanaji wa chakula katika maeneo yenye upungufu na vile vile kujitayarisha kwa msimu ujao wa kilimo. Hata hivyo, ipo baadhi ya mikoa ambayo itajitosheleza kwa chakula. Kwa msingi huo, natoa wito kwa wananchi ambao bado wanacho chakula wakihifadhi vyema ili kiweze kuwatosheleza hadi mavuno ya msimu unaofuata. Tunawashauri wananchi kuwa wasivutwe na bei nzuri ya mazao ya chakula iliyopo kwenye

soko sasa hivi wakauza chakula chote bali wauze kile ambacho tu ni ziada. Kwa wale wenye mifugo tuwahimize wauze baadhi ya mifugo yao sasa ili wajinunulie chakula na kuweka akiba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu wa chakula, upo uwezekano vile vile wa kuwepo kwa upungufu wa maji hususan katika maeneo yale yenye hali ya ukame. Ukame na upungufu wa mvua umesababisha vile vile maji kupungua kwenye mabwawa na mito. Kwa sababu hiyo maeneo yenye wakazi wengi hasa mijini ambayo vyanzo vya maji ni mito na mabwawa nayo yanaweza kukabiliwa na upungufu mkubwa wa maji. Wito wangu kwa wananchi ni kutumia maji kwa uangalifu sana hususan watu wa mijini.

Kwa jinsi hali ilivyo hivi sasa tutakuwa na upungufu wa maji. Ni vema basi tukawa waangalifu na tutumie maji vizuri ili yatuchukue muda mrefu zaidi. Pale hatua za dharura zitakapobidi kuchukuliwa, Serikali haitasita kufanya hivyo na tunawaomba wananchi washirikiane na Serikali yao kutafuta ufumbuzi wa matatizo yatakayojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala mengine muhimu, UKIMWI bado ni tishio kwa maisha ya Watanzania pamoja na ustawi wa Taifa letu. Tumechukua hatua mbalimbali za kukabiliana nao na Serikali imezieleza hatua hizo katika mkutano huu. Aidha, Serikali imeanza kuziwezesha Halmashauri zetu na asasi zisizo za Kiserikali ili ziweze kushiriki kikamilifu katika mapambano yetu dhidi ya janga hili. Mara kwa mara tumesikia ushauri na maelezo kuwa zipo nchi ambazo zimefanikiwa kupunguza kasi ya maambukizi, lakini sisi bado hakuna dalili za maambukizi kupungua. Wenye uwezo wa kupunguza kuenea kwa UKIMWI ni sisi wenyewe.

Kila Mtanzania mahali alipo akiamua kuvunja ukimya na kukataa tabia ambazo zinasababisha kuenea kwa UKIMWI tutaweza kufanikiwa. Kama hatuna dhamira ya dhati kutoka kwa kila Mtanzania binafsi, hata tupate uwezo mkubwa wa kibajeti bado UKIMWI utaenea. Wito wangu ni kuwa Watanzania tuache mchezo na maisha yetu, kauli zetu ziendane na matendo yetu ili tuweze kuudhibiti ugonjwa huu. Viongozi tuonyeshe njia kwa kutoa ushauri, elimu na kukemea kila inapobidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuendesha mapambano hayo, ni vema tutambue kuwa tunao waathirika tayari. Kwa msingi huo tuendeleze elimu itakayosaidia kuondoa unyanyapaa na vile vile kusaidia kuwalea na kuwatunza watoto ambao wazazi na walezi wao wamekufa kwa UKIMWI. Tuwasaidie wananchi watambue umuhimu wa huduma za ushauri nasaha ili waweze kuzitumia kwani husaidia katika kuwawezesha wananchi walioathirika na wale ambao hawakuathirika. Zipo hoja zinazotolewa kuhusu dawa za kuongeza maisha, lakini ni vema tukubali kuwa dawa hizo bado ni ghali na uwezo wetu katika ngazi ya mtu binafsi, Kaya na hata Serikali haiwezi kubeba gharama zake. Kwa msingi huo, tusisitize umuhimu wa lishe bora kama mkakati muhimu wa kuwasaidia walioathirika.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu Waheshimiwa Wabunge wamepata taarifa kuhusu harakati za Taifa letu za kupambana na mila na tabia zinazowadhalilisha wanawake. Ni kweli kuwa katika baadhi ya jamii nchini bado zipo mila na tabia za kudhalilisha wanawake kama vile kuwapiga, kuwakeketa, kuwanyima fursa mbalimbali za maendeleo na kadhalika. Hata hivyo, ni vema tukatambua juhudi zinazochukuliwa na Serikali na asasi zisizo za Kiserikali katika kupambana na mila hizi. Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza asasi hizo ambazo zimeshirikiana kikamilifu na Serikali na jamii kwa ujumla katika kutoa elimu na kuhamasisha wananchi, hususan wanawake wenyewe kukataa mila hizi na kuwa tayari kushiriki katika mapambano dhidi ya mila hizo. Ni kweli hata hivyo kuwa suala la mabadiliko ya mila na utamaduni wa jamii huchukua muda, lakini kwa kuendelea kutoa elimu na kuhakikisha kuwa tunawafikia wananchi wengi zaidi tutaweza kufanikiwa. Wajibu wa viongozi na hasa sisi wawakilishi wa wananchi ni kuwafikia na kusaidia kuweka mazingira muafaka yatakayowawezesha wahamasishaji kutekeleza wajibu huu mkubwa wa kutoa elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alipokuwa anawasilisha hoja yake ndani ya Bunge lako Tukufu, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete alitueleza kuwa katika muda mfupi ujao nchi yetu itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa mwaka wa Wakuu wa nchi za *SADC.* Mkutano huo utaanza tarehe 19 Agosti, 2003 hadi tarehe 26 Agosti, 2003. Aidha, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alipokuwa analihutubia Taifa tarehe 31 Julai, 2003 alitueleza vile vile kuhusu Mkutano huu na heshima ya Tanzania kuwa

Mwenyekiti wa *SADC* katika kipindi cha mwaka mmoja. Hii ni heshima kubwa kwa nchi yetu. Mkutano huu utafanyika Dar es Salaam na kwa msingi huo wananchi wa Dar es Salaam watakuwa wawakilishi wetu katika kuukaribisha ugeni huu mkubwa. Wito wangu kwa watu wa Dar es Salaam ni kuwa, kama ilivyo kawaida yao nawaomba wawakaribishe wageni wetu kwa kila aina ya shamrashamra. Napenda kutumia fursa hii kuupongeza uongozi wa nchi za *SADC* kwa kuipa nchi yetu heshima hiyo. Kama Bunge lako Tukufu lilivyoarifiwa Serikali itahakikisha kuwa Mkutano huu unafanyika kwa ufanisi wa hali ya juu ili kuendeleza sifa ya ukarimu wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka kesho Muungano wetu utatimiza miaka 40 tangu kuanzishwa kwake. Katika kipindi chote hiki, tumeweza kujenga misingi ya umoja na mshikamano wa Kitaifa kati ya wananchi wa Tanzania Bara na wananchi wa Tanzania Zanzibar. Kila mara tumetatua matatizo yaliyojitokeza kwa majadiliano na hakuna hata wakati mmoja tuliposhindwa kuelewana. Kila Mtanzania wa Bara na wa Zanzibar anakubali na kuamini kuwa Muungano wetu una faida nyingi na kubwa. Katika mazingira ya utandawazi ambapo mabadiliko ya kiteknolojia yamerahisisha mambo mengi, Mataifa mbalimbali yametambua umuhimu wa kuungana kama njia ya kuweza kutumia mabadiliko hayo kuleta maendeleo kwa watu wao. Kwa upande wetu Watanzania nasi tutumie mazingira haya ya utandawazi kuondoa kero na vikwazo vya Muungano na tuwapuuze wale ambao kwa kauli zao wanataka na wanatabiri kuvunjika kwa Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kero zinazojitokeza ni za Kitaasisi zaidi kuliko za wananchi wa kawaida. Mwananchi wa kawaida anayetoka Manzese Dar es Salaam au Malindi Unguja anapovuka bahari kwenda upande wa pili aidha kwa matembezi ya kawaida au kwa biashara anajisikia yupo ndani ya nchi yake na kwamba hawaelewi utabiri wa hao wanaozungumzia kuvunjika kwa Muungano. Kwa msingi huo, sisi ambao tumekabidhiwa dhamana ya uongozi na wananchi, tunao wajibu wa kusaidia kusukuma mbele maslahi ya Muungano na kila mara kujaribu kukwepa kauli ambazo zinaashiria kuwa Muungano wetu una matatizo makubwa. Tumeshuhudia kauli japo chache zinazotaka kujenga hisia kuwa kuna upande wa Muungano unaofaidi kuliko mwingine. Hizi sio kauli njema. Hakuna upande unaofaidi au upande unaopunjika. Tanzania ni nchi moja na pande hizi za Muungano zitasaidiana nyakati zote za shida na za raha kwa maslahi ya Watanzania wote. Matatizo hayako tu kwa Muungano, hata Tanzania Bara kuna matatizo, Tanzania Zanzibar kuna matatizo, ndani ya kila Mkoa mmoja mmoja kuna matatizo na hata katika kila Wilaya kuna matatizo. Yatokeapo hayo, wahusika hukaa pamoja na kutafuta suluhu na sio kutoka barabarani na kuimba matatizo. Na vivyo hivyo kwa Muungano tutaendelea kutatua matatizo yetu kwa mashauriano na kwa maelewano makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia sana juu ya kasi ya Serikali kuhamia Dodoma. Michango yao imeonyesha wasiwasi walionao na wengine kudhani kuwa labda hata kuna dalili za kutokutaka kuhamia Dodoma kwa makusudi. Ninataka kuwahakikishieni kuwa azma ya kuhamia Dodoma iko pale pale na sasa kasi inaongezeka zaidi. Mheshimiwa Rais tarehe 29 Julai, 2003 alipokuwa anazindua Mradi mkubwa wa Maji wa Mzakwe Dodoma, alisema wale ambao wanaonyesha dalili za kulegeza mwendo wa kuhamia Dodoma, wajue bado ana zaidi ya miaka miwili madarakani. Sote tunaiona dhamira ya wazi ya Mheshimiwa Rais kutaka Serikali ihamie Dodoma. Yeye mwenyewe amekuwa akitumia muda mrefu Chamwino na vikao vyake vingi anavifanyia hapa Dodoma. Pamoja na upungufu wa majengo na fedha za uhamisho, ninataka kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kuwa katika mwaka huu wa fedha tutafanya kila jitihada katika mambo yafuatayo: -

* Serikali itahakikisha kuwa Wizara zilizohamia hapa Dodoma zinaongeza kasi ya kuhamisha Idara zilizobakia Dar es Salaam; *(Makofi)*

* ` Juhudi zitafanywa ili Wizara angalau mbili zaidi zihamie Dodoma katika kipindi hiki; na *(Makofi)*

* Serikali inaangalia upya uamuzi wa baadhi ya Wizara na Ofisi wa kujenga Ofisi zao Dar es Salaam. Pale ambapo hapana sababu ya msingi, fedha hizo zitaelekezwa katika ujenzi wa Ofisi hizo Dodoma badala ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nikushukuru wewe binafsi na Naibu Spika, Mheshimiwa Juma J. Akukweti, Mbunge wa Tunduru kwa uongozi wenu thabiti katika Mkutano huu wa Kumi na Mbili

wa Bunge lako Tukufu ambao umekamilisha shughuli zake leo. Aidha, nawapongeza Wenyeviti Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini na Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kwa msaada mkubwa waliokupa katika kuongoza Vikao vya Mkutano huu. Umeendelea kuwa mwalimu mkubwa kwa kusaidia kuwaandaa viongozi wa kuweza kumudu kuongoza shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kuwa tunao viongozi wanaoweza kuliongoza Bunge kwa umahiri mkubwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile niwapongeze na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Serikali ambao wametekeleza majukumu yao kikamilifu na wakati mwingine kwa vipindi virefu na hivyo kuiwezesha Serikali kutekeleza kazi zake zote ndani ya Bunge lako Tukufu. Kutokana na juhudi yao ratiba yote ya shughuli za Bunge ilitekelezwa kama ilivyopangwa. Aidha, napenda niwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Kipenka Mussa, kwa huduma mbalimbali ambazo zimewawezesha Waheshimiwa Wabunge kutekeleza majukumu yao katika muda wa karibu miezi miwili sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kuvishukuru vyombo vyote vya habari kwa kazi yao nzuri wanayoifanya katika kuwafahamisha na kuwaelimisha wananchi kuhusu majadiliano na maamuzi yaliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano huu. Napenda kuwathibitishia kuwa Serikali inathamini sana kazi nzuri waliyoifanya na bila shaka Waheshimiwa Wabunge wataungana nami kuvipongeza vyombo vyote vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya muda wa karibu miezi miwili ya kuwa nje ya Majimbo yetu bila shaka sote tutapenda kurejea mara moja katika Majimbo hayo ili kukutana na wapiga kura wetu na kusaidiana na uongozi wa Wilaya kusimamia utekelezaji wa yale yaliyoamuliwa katika Mkutano huu na mengine mengi yanayohusu maendeleo ya wananchi huko Vijijini. Kwa msingi huo naomba niwatakie Waheshimiwa Wabunge wote safari njema mnapoelekea kwenye Majimbo na maeneo yenu ya kazi. Aidha, tukatoe elimu juu ya kodi zilizofutwa, zilizowekewa viwango na zilizobakizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 4 Novemba, 2003, Siku ya Jumanne, Saa Tatu Asubuhi, litakapokutana hapa Mjini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati wa maswali huwa natazama tazama saa na kuwaambieni ya kwamba muda wa maswali umekwisha, sasa leo nimetazama saa naona muda wa kuahirisha Bunge bado, kwa hiyo kaeni hapo hapo. *(Kicheko/Makofi)*

Kabla sijawahoji Waheshimiwa Wabunge kuna matangazo mawili. Moja, ni mwaliko wa Mheshimiwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, kwenye hafla ya kukamilisha Mkutano huu wa Kumi na Mbili katika Viwanja vyetu vya Burudani mara baada ya Kuahirisha Bunge.

Pili, linatoka *CRDB* wanasema, wale Waheshimiwa Wabunge wote waliopiga picha kwa ajili ya kupatiwa *Tembo Card, Card* zao ziko tayari sasa wanaweza kwenda kuzichukua ili waondoke nazo, sina hakika kama bado wapo katika chumba Namba 9, katika Jengo letu la Utawala.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 12.15 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 4 Novemba, 2003 Saa Tatu subuhi)*